# *SHUJAAZ* KAMA KAZI YA FASIHI YA KISWAHILI

**MBURU CHARLES KIARIE**

**Tasnifu inayowasilishwa katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Egerton**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**MACHI 2026**

## UNGAMO NA IDHINI

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na halijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kingine chochote.

**SAHIHI** **TAREHE: 10/3/26**

**Mburu Charles Kiarie**

**AD12/16551/18**

**IDHINI**

Tasnifu hii inawasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

**TAREHE: 18/Marchi/2026**

**Dkt. Raphael. M. Gacheiya**
Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu Chuo Kikuu cha Egerton.

**SAHIHI** **TAREHE: 13/03/2026**

**Prof. Abdulrahim. H. Taib Ali**
Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu Chuo Kikuu cha Pwani.

**HATILINZI**

**©2026 Mburu C. Kiarie**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kuhifadhi, kwa mfumo wowote ule au katika hata sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi na au Chuo Kikuu cha Egerton.

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mke wangu mpendwa Waithira Kiarii na watoto wangu wapendwa Mburu, Ngotho, Njuguna na Gathoni.

## SHUKURANI

Shukurani zangu kwanza ni kwa Mwenyezi Mungu muumba wa yote kwa kunipa uhai, kwa kunijalia wazo la kujiunga na masomo ya uzamifu na hela za kugharamia karo na matumizi mengine. Namshukuru Mungu kwa afya njema na fadhila zake zisizo kifani. Amenipa familia inayonielewa hasa nilipochukua hatua ya kushiriki masomo ya uzamifu.

Shukrani za kipekee ziendee Chuo Kikuu Cha Egerton kwa kunipa nafasi ya kupata masomo ya uzamifu, Shukrani ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Abdulrahim Hussein Taib Hussein na Dkt. Raphael Gacheiya kwa maelekezo na ushauri wao ambao siwezi kuupigia mfano. Nawashukuru pia Walimu wengine katika Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu walichangia kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha kazi hii. Mungu awabariki kwa wingi wa fadhila zake.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu wa uzamifu wa mwaka wa 2018 sasa Dkt. Melvin na Marehemu Judy Gaki (Mungu ailaze roho yake pema peponi), Mungu akubariki Bi. Melvin na akupe ufanisi maishani na aibariki familia yako pia.

Namshukuru mke wangu ambaye ni rafiki wa dhati, Mpenzi Miriam Waithira kwa motisha aliyonitia na maombi yake. Watoto wangu; Gad Mburu, Samwel Ngotho, Henry Njuguna na Elizabeth Gathoni. Mungu awabariki na atupe upendo, uvumilivu, amani na ufanisi katika familia yetu.

Wale wote walionisaidia katika kupiga chapa, kutoa nakala, kuhariri, na kunitia moyo lakini sijawataja nawaomba wapokee shukrani zangu za dhati. Nyote nawaombea mungu awabariki.

## IKISIRI

Fasihi andishi hushirikisha sio tu fasihi inayowasilishwa kwa njia ya maandishi bali pia fasihi ni sanaa inayotumia picha na michoro kuwasilisha ujumbe hasa pale picha na michoro hiyo inaambatanishwa na maneno yaliyoandikwa. *Shujaaz* ni toleo la katuni ambalo huchapishwa mara moja kila mwezi na kampuni ya *Well Told Story* na husambazwa na *Gazeti la Saturday Nation* kila Jumamosi ya kwanza ya kila mwezi. *Shujaaz* ni tofauti na fasihi andishi tuliyoizoewa katika kazi za kifasihi kwani *Shujaaz* ni fasihi ya kifani ya kipekee ambayo inatumia vyote maandishi, michoro, picha halisi, taarifa kuwasilisha tajiriba na ujumbe kwa jamii husika kama ilivyo fasihi yoyote ili. Hali hii ndiyo iliyozua ari ya utafiti huu. Madhumuni makuu ya utafiti huu ni kuthibitisha kuwa *Shujaaz* ni kazi ya fasihi ya Kiswahili ambayo inahusisha picha za watu halisi, michoro na teknolojia katika uwasilishaji wa ujumbe. Kuafikia lengo hili, utafiti huu umeweza: kutambua sifa bainifu za *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili, kuhakiki *Shujaaz* kama kazi ya fasihi kwa kutumia vigezo vya uhakiki wa fasihi, na kutathmini upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya Metausasa yake Robin na Timotheus (2016) Utafiti huu ni wa kithamano na data imekusanywa kutoka kwa 10% ya matoleo yaliyochaguliwa kimakusudi miongoni mwa matoleo 130 yaliyopo ya *Shujaaz* kufikia mwezi ya Januari 2021. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa ufasiri data iliyokusanywa kwa mwongozo wa mihimili mahsusi ya nadharia ya Metausasa. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo haya yanatarajiwa yataweka wazi kuwa *Shujaaz* ni kazi ya fasihi na yafaa kuthaminiwa, kusomwa na kuhakikiwa kama tanzu nyinginezo za fasihi. Kazi hii inatarajiwa kuwa mwongozo wa kutafitia kazi nyinginezo zinazofanana na kazi ya *Shujaaz.*

## ABSTRACT

Literary works no longer concern literature that is communicated only in written form but also literary works that use photographs and drawings that have written messages used by the characters in the photographs and drawings. This kind of literary work, include photo novellas and comic books like *Shujaaz*. *Shujaaz* is a comic print out, authored and published every month by *Well Told Story Company* and distributed by the *Saturday Nation Newspaper* every first Saturday of the month. This study was about *Shujaaz* as a literary work that combines the use of photos, drawings and technology. Specific objectives are; to identify the distinctive features of *Shujaaz* as a literary work, to analyse *Shujaaz* based on the basic elements of analysing literature and evaluating the uniqueness of *Shujaaz* as a Kiswahili literary work. Metamodern theory of Robin and Timotheous (2016) has guided this study to achieve the research objectives. This theory is ideal for this research as it have given the researcher the opportunity to interpret *Shujaaz* as literary work. Sampling has been purposive and a collection of 10% of the 130 available editions of *Shujaaz* by the month of January 2021 has been analysed. The research involved reading, collecting and analysing data guided by specific tenets of reseach theories. This research being a qualitative research, analysis of the data was interpretive in nature. The outcome of this study is expected to contribute to the ongoing discussion that *Shujaaz* is a form of literary work and hence should be treated as such and even studied like any other literary work. It is also expected that the findings will act as a guide in the study of similar literary works.

**YALIYOMO**

**UNGAMO NA IDHINI** ....... ii

**UNGAMO** ....... ii

**IDHINI** ....... ii

**HATIMILIKI** ....... iii

**TABARUKU** ....... iv

**SHUKURANI** ....... v

**IKISIRI** ....... vi

**ABSTRACT** ....... vii

YALIYOMO ....... viii

VIELELEZO ....... xi

**SURA YA KWANZA** ....... 1

**UTANGULIZI** ....... 1

1.1 Usuli wa Mada ....... 1

1.2 Mada ya Utafiti ....... 5

1.3 Madhumuni ya Utafiti ....... 5

1.4 Maswali ya utafiti ....... 5

1.5 Umuhimu na Sababu za Kuchagua Mada hii ....... 6

1.6 Upeo na Mipaka ....... 6

1.7 Ufasili wa Dhana ....... 7

**SURA YA PILI** ....... 8

**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA** ....... 8

2.1 Utangulizi ....... 8

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu kijitabu cha *Shujaaz* ....... 8

2.3 Tafiti kuhusu kijitabu cha Shujaaz kama Fasihi ....... 11

2.4 Msingi wa Nadharia........................................................................................................ 12

**SURA YA TATU............................................................................................................ 15**

**MBINU ZA UTAFITI.................................................................................................... 15**

3.1 Utangulizi.................................................................................................................... 15

3.2 Muundo wa Utafiti...................................................................................................... 15

3.3 Sampuli Lengwa.......................................................................................................... 15

3.4 Mbinu ya Ukusanyaji wa Data.................................................................................... 15

3.5 Mbinu za utafiti........................................................................................................... 15

3.6 Uchanganuzi wa Data.................................................................................................. 16

3.7 Uwasilishaji wa Data................................................................................................... 16

**SURA YA NNE............................................................................................................... 18**

**SIFA BAINIFU ZA *SHUJAAZ* KAMA FASIHI YA KISWAHILI.................................... 18**

4.1 Utangulizi.................................................................................................................... 18

4.2 Sifa za fasihi................................................................................................................ 18

4.3 Sifa za Shujaaz kama utanzu wa sanaa......................................................................... 18

4.4 Sifa za Shujaaz kama fasihi.......................................................................................... 21

4.5 Sifa za *Shujaaz* za kifani na maudhui........................................................................... 24

4.6 Hitimisho..................................................................................................................... 44

**SURA YA TANO............................................................................................................. 46**

**UHAKIKI WA *SHUJAAZ* KAMA FASIHI YA KISWAHILI........................................... 46**

5.1 Utangulizi.................................................................................................................... 46

5.2 Uhakiki wa kazi ya fasihi ya Kiswahili......................................................................... 46

5.3 Maudhui katika *Shujaaz*................................................................................................ 46

5.4 Fani katika Shujaaz...................................................................................................... 89

**SURA YA SITA** ........ 152

**UPEKEE WA *SHUJAAZ* KAMA KAZI YA FASIHI** ........ 153

**6.1** Utangulizi ........ 153

**6.2** Maudhui ........ 153

**6.3** Wahusika ........ 158

**6.4** Ploti ........ 163

**6.5** Mtindo ........ 164

**6.6** Umbo ........ 168

**6.7** Mandhari ........ 169

**6.8** Lugha ........ 176

**6.9** Ujanibishaji na upekee wa *Shujaaz* ........ 178

6.10 Hitimisho ........ 189

**SURA YA SABA** ........ **190**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ........ **190**

**7.**0 Utangulizi ........ 190

7.1 Muhtasari ........ 190

7.3 Hitimisho ........ 194

7.4 Mapendekezo ........ 195

**MAREJELEO** ........ 197

## ORODHA YA VIELELEZO


**Kielelezo cha 1: Chapta 12 uk 6.......... 28**

**Kielelezo cha 2: Chapta 57 uk 8.......... 29**

**Kielelezo cha 3:Chapta 88 uk 7.......... 31**

**Kielelezo cha 4: Chapta 88 uk26 .......... 32**

**Kielelezo cha 5: Chapta 88 uk 14.......... 37**

**Kielelezo cha 6: Chapta 88 uk 14.......... 38**

**Kielelezo cha 7:Chapta 88 uk31.......... 38**

**Kielelezo cha 8: Chapta 93 uk 30.......... 40**

**Kielelezo cha 9: Chapta 57 uk 8.......... 41**

**Kielelezo cha 10: Special Edition 03/03 uk 8-9..........44**

**Kielelezo cha 11: Chapta 27 uk 18.......... 44**

**Kielelezo cha 12: Chapta 27 uk 31.......... 46**

**Kielelezo cha 13: Chapta 93 uk 14.......... 58**

**Kielelezo cha 14: Chapta 88 uk 18.......... 59**

**Kielelezo cha 15: Chapta 88 uk 29.......... 61**

**Kielelezo cha 16: Chapta 93 uk 7.......... 62**

**Kielelezo cha 17: Chapta 68 uk 14.......... 65**

**Kielelezo cha 18: Chapta 88 uk 32.......... 67**

**Kielelezo cha 19: Chapta 33 uk 27.......... 68**

**Kielelezo cha 20: Chapta 33 uk 29.......... 69**

**Kielelezo cha 21: Chapta 33 uk 9.......... 70**

**Kielelezo cha 22: Chapta 93 uk 32.......... 71**

**Kielelezo cha 23: Chapta 88 uk 7.......... 72**

**Kielelezo cha 24: Chapta 78 uk 15.......... 73**

**Kielelezo cha 25: Chapta 98 uk 22.......... 73**

**Kielelezo cha 26: Chapta 57 uk 16.......... 74**

**Kielelezo cha 27: Chapta 33 uk 30.......... 75**

**Kielelezo cha 28: Chapta 98 uk 16.......... 77**

**Kielelezo cha 29: Chapta 68 uk8............ 78**
**Kielelezo cha 30: Chapta 109 uk 3............ 81**
**Kielelezo cha 31: Chapta 109 uk 6............ 82**
**Kielelezo cha 32: Chapta 109 uk 7............ 82**
**Kielelezo cha 33: Chapta 109 uk 8............ 83**
**Kielelezo cha 34: Chapta 109 uk 4............ 83**
**Kielelezo cha 35: Chapta 109 uk 20............ 84**
**Kielelezo cha 36: Chapta 109 uk 18............ 84**
**Kielelezo cha 37: Chapta 109 uk 16............ 85**
**Kielelezo cha 38: Chapta 109 uk 22............ 86**
**Kielelezo cha 39: Chapta 33 uk 19............ 87**
**Kielelezo cha 40: Chapta 33 uk 18............ 88**
**Kielelezo cha 41: Chapta 88 uk 19............ 88**
**Kielelezo cha 42: Chapta 88 uk 19............ 89**
**Kielelezo cha 43: Chapta 88 uk 20............ 90**
**Kielelezo cha 44: Special Edition 01/03 uk 11-12............91**
**Kielelezo cha 45: Chapta 102 uk 2............ 92**
**Kielelezo cha 46: Chapta 68 uk 5............ 97**
**Kielelezo cha 47: Chapta 68 uk 19............ 97**
**Kielelezo cha 48: Special Edition 03/03 Jalada............ 102**
**Kielelezo cha 49: Chapta 68 uk Jalada............ 103**
**Kielelezo cha 50: Chapta 109 Jalada............ 104**
**Kielelezo cha 51: Chapta 27 Jalada............ 105**
**Kielelezo cha 52: Special Edition 03/03 Jalada............ 106**
**Kielelezo cha 53: Chapta 102 uk 20............ 110**
**Kielelezo cha 54: Chapta 102 uk 21............ 113**
**Kielelezo cha 55: Chapta 102 uk 24............ 114**
**Kielelezo cha 56: Chapta 102 uk 22............ 118**
**Kielelezo cha 57: Chapta 12 uk 5............ 122**
**Kielelezo cha 58: Chapta 33 uk 30............ 123**

**Kielelezo cha 59: Chapta 68 uk 6** ........ **124**
**Kielelezo cha 60: Chapta 103 uk 15** ........ **125**
**Kielelezo cha 61: Chapta 33 uk 6** ........ **126**
**Kielelezo cha 62: Chapta 57 uk 8** ........ **127**
**Kielelezo cha 63: Chapta 57 uk 15** ........ **128**
**Kielelezo cha 64: Chapta 33 uk 9** ........ **128**
**Kielelezo cha 65: Chapta 109 uk 2-3** ........ **131**
**Kielelezo cha 66: Chapta 93 uk 3** ........ **137**
**Kielelezo cha 67: Chapta 57 uk 12** ........ **143**
**Kielelezo cha 68: Chapta 27 uk 31** ........ **144**
**Kielelezo cha 69: Chapta 33 uk 29** ........ **145**
**Kielelezo cha 70: Chapta 93 Jalada** ........ **147**
**Kielelezo cha 71: Chapta 78 Jalada** ........ **148**
**Kielelezo cha 72: Chapta 88 uk 25** ........ **149**
**Kielelezo cha 73: Special Edition 30/30 uk 9** ........ **150**
**Kielelezo cha 74: Chapta 88 uk 16** ........ **150**
**Kielelezo cha 75: Chapta 93 uk 29** ........ **151**
**Kielelezo cha 76: Chapta 78 uk 2** ........ **152**
**Kielelezo cha 77: Chapta 27 uk 25** ........ **153**
**Kielelezo cha 78: Chapta 27 uk 26** ........ **153**
**Kielelezo cha 79: Chapta 27 uk 27** ........ **154**
**Kielelezo cha 80: Chapta 98 uk 8** ........ **155**
**Kielelezo cha 81: Chapta 88 uk 7** ........ **158**
**Kielelezo cha 82: Special Edition 03/03 uk 8-9** ........ **164**
**Kielelezo cha 83: Chapta 57 uk 23** ........ **165**
**Kielelezo cha 84: Chapta 88 uk 13** ........ **166**
**Kielelezo cha 85: Chapta 33 uk 15** ........ **167**
**Kielelezo cha 86: Chapta 109 uk 11** ........ **167**
**Kielelezo cha 87: Chapta 68 uk 10** ........ **169**
**Kielelezo cha 88: Chapta 78 uk 8** ........ **169**

**Kielelezo cha 89: Chapta 57 uk 5......................................................................................... 170**
**Kielelezo cha 90: Chapta 93 uk 5......................................................................................... 171**
**Kielelezo cha 91: Chapta 27 uk 16-17.................................................................................171**
**Kielelezo cha 92: Chapta 93 uk 32....................................................................................... 174**
**Kielelezo cha 93: Chapta 109 uk 23..................................................................................... 175**
**Kielelezo cha 94: Chapta 33 uk 20....................................................................................... 175**
**Kielelezo cha 95: Chapta 93 uk 31....................................................................................... 176**
**Kielelezo cha 96: Chapta 57 uk 25....................................................................................... 176**
**Kielelezo cha 97: Chapta 109 uk Jalada...............................................................................177**
**Kielelezo cha 98 & 99: Special Edition 03/03 uk 2-3............................................................ 179**
**Kielelezo cha 100: Chapta 88 uk 6........................................................................................ 180**
**Kielelezo cha 101: Chapta 109 uk 15.................................................................................... 180**
**Kielelezo cha 102: Chapta 98 uk 12...................................................................................... 181**
**Kielelezo cha 103: Chapta 57 uk 12...................................................................................... 181**
**Kielelezo cha 104: Special Edition 03/03 uk 10....................................................................182**
**Kielelezo cha 105: Chapta 12 uk 24...................................................................................... 183**
**Kielelezo cha 106: Chapta 57 uk 8 ....................................................................................... 184**
**Kielelezo cha 107: Chapta 68 uk 14...................................................................................... 185**
**Kielelezo cha 108: Chapta 109 uk 11.................................................................................... 186**
**Kielelezo cha 109: Chapta 27 uk 10...................................................................................... 186**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Sehemu hii, inatanguliza kwa kuangalia fasihi ni nini, makundi ya fasihi yaliyopo na tanzu za makundi haya. Kisha kueleza sifa na umuhimu wa fasihi ya Kiswahili kwa jumla. Sehemu hii inaeleza mabadiliko ambayo fasihi imepitia hadi kufikia kuwepo kwa kazi kama ya *Shujaaz.* Kisha, vigezo vya kimsingi vya uhakiki wa kazi ya fasihi ya Kiswahili kwani utafiti huu ulihusu uhakiki wa *Shujaaz* kama fasihi. Sehemu hii hatimaye inaeleza kwa nini ni muhimu kutafiti kazi ya *Shujaaz* kama fasihi ya Kiswahili.

## 1.1 Usuli wa Mada

Fasihi, kulingana na Wamitila (2008), Eagleton (1983), Njogu na Chimera (2011) Mulokozi, 1996). Mazingwe (1991), Siyambo na Mazrui (1992), Ngugi (2018), Ngure (2003:1) Nkwera (1978) Mchuchuri (2017), ni sanaa inayotumia lugha kisanii kuelezea tajriba za binadamu katika jamii yake kwa njia ya kibunifu ili kuwasilisha ujumbe katika Jamii. Kwa hivyo, fasihi huakisi jamii; ni kioo cha jamii. Uhusiano huu hutokana na sababu kuwa mtunzi wa kazi ya fasihi ni kiumbe anayelelewa katika mazingira fulani ya kitamaduni, kiuchumi, kisiasa, ki-itikadi, kihistoria na kijiografia. Hivyo basi, fasihi huakisi kwa namna fulani mazingira hayo. Mtunzi wa kazi ya fasihi hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake, kwa sababu ana maslahi katika jamii hiyo. Kutokana na maelezo haya, kazi ya fasihi lazima itumie lugha kisanii kuwasilisha ujumbe wake. Ujumbe huo huhusu tajriba ya maisha ya jamii husika na uwasilishaji wenyewe uwe kwa njia ya ubunifu wa hali ya juu ili kufanikisha kueleweka kwake.

Fasihi ya Kiswahili hugawika katika matawi mawili makuu kama anavyosema Wamitila (2008). Anaeleza kuwa kuna fasihi simulizi na fasihi andishi. Fasihi simulizi inahusu fasihi inayosimuliwa kwa mdomo huku fasihi andishi ikiwa ni fasihi inayowasilishwa kupitia maandishi. Fasihi simulizi hugawika katika tanzu ambazo ni hadithi, mazungumzo, maigizo, ushairi simulizi na semi. Huku tanzu za fasihi andishi zikiwa ni riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Cha muhimu kutaja hapa ni kuwa mbali na kuwapo kwa matawi haya mawili ya fasihi, matawi haya huwa na sifa za kimsingi ambazo kulingana na Robinson (2019), Wilson World (2021) na Wamitila (2008) ni: Kwanza, fasihi hutumia lugha kuwasilisha ujumbe wake. Lugha yaweza kutumiwa kwa njia ya kuzungumzwa au kuandikwa. Lugha yenyewe hutumiwa kiufundi kwa kutumia tamathali za usemi

kwa wingi. Pili, huhusisha utendaji; uimbaji, utambaji, uigizaji, unenaji, usomaji, ukariri, uchoraji au kupitia picha. Tatu, huwa na wahusika tofauti ambao hutumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe wake. Wahusika huwa ni binadamu, wanyama au viumbe vilivyo hai au visivyohai. Wahusika hawa hutumiwa na msanii kuakisi tabia, falsafa, misimamo na matarajio ya watu katika jamii yake. Nne, huwasilishwa katika mandhari maalum. Yaani eneo au mahali mahususi, wakati mahususi na kuhusisha jamii/ jumuiya fulani mahususi. Mandhari hutegemea maisha ya jumuiya lengwa inapoishi, shughuli zake za kila siku za kijamii, kidini, kiuchumi na kisiasa. Tano, huwasilisha maudhui tofauti kutegemea dhamiria ya msanii kwa mujibu wa yanayotokea katika jamii. Sita, hupambwa kwa kutumia fani mbalimbali. Saba, kuhusisha hadhira hasa fasihi simulizi. Hadhira hutumiwa kufanikisha uwasilishaji wake. Kwa mfano, mwimbaji aweza kuongoza wimbo nayo hadhira ikaimba kipokeo na hapo wote wakashiriki katika uimbaji wa wimbo huo. Nane, hubadilika kadri jamii inavyobadilika.

Fasihi hutekeleza majukumu mbali mbali kama wanavyoeleza Sengo (2018), Wellek na Warren (1985), Ngugi (2018), Wamitila (2008) na Nidelson na Lynch-Brown (2003). Kwanza, fasihi huburudisha, hufurahisha, hutumbuiza na kusisimua jamii. Nyimbo, hadithi, maigizo, riwaya, mashairi na tanzu nyingine za fasihi hutungwa na kuwasilishwa kutekeleza jukumu hili. Wanajamii husikiliza, hutazama, hushiriki na hata husoma kazi za fasihi kwa nia ya kujiburudisha. Pili, fasihi huaadilisha jamii. Jamii imara hujengeka katika misingi ya maadili mema. Fasihi hufanikisha haya kwani wasanii huitumia kukusoa, kuelekeza, kuonya, kukanya, kushauri na kutoa nasaha kwa wanajamii kuhusu namna ya kuishi na kukabili mambo tofauti katika maisha. Tatu, fasihi huelimisha jamii. Fasihi hulenga kuielimisha na kuifunza jamii kuhusu majukumu ya wanajamii kuhusiana na shughuli za kijamii, kiuchumi, kisiasa pamoja na mambo kuhusu mazingira na majanga. Nne, fasihi huendeleza na kuhifadhi mila, itikadi, desturi na tamaduni za jamii. Kupitia fasihi jamii hupitisha mila na tamaduni zake kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Kwa mfano miviga tofauti kuhusu jamii husika hupitisha na kuhifadhi mila na tamaduni za jamii husika kila wakati wanajamii hiyo wanaposhiriki katika miviga hiyo. Tano, fasihi huwa ni kitambulisho cha jamii. Kila jamii ina upekee wa kuiwasilisha fasihi yake. Upekee huu huitambulisha jamii husika. Sita, fasihi ni chombo cha utetezi wa maslahi ya tabaka moja au jingine na kwamba mwandishi au fanani ni mtumishi wake. Mwandishi au fanani huwa na lengo

au dhamira fulani anayotaka kuionyesha hadhira. Lengo au dhamira hii itatokana na fani, itikadi ya siasa inayotawala jamii husika.

Katika kufafanua sifa za fasihi Wamitila (2008) alieleza kuwa fasihi hubadilika kadri jamii inavyobadilika. Jamii ya kabla ya ujio wa maandishi ilikuwa na fasihi simulizi kisha kama wanavyo eleza *Collectors Headquarter* (2020) fasihi ilianza na uwepo wa binadamu kama fasihi simulizi kisha ikaja michoro hieroglifu ya kule Misri. Baadaye katika karne ya 15 uchapishaji wa maandishi kule Gutenberg kuvumbuliwa na hapo fasihi ikawasilishwa kupitia maandishi. Kulingana na Gunda (2014) katika karne ya 19 fasihi ilianza kuhusisha michoro ya katuni au vibonzo. Mfano wa kazi zilizofana za katuni ni: *Batman, Superman* na *Adventures of Tin Tin*. Baada ya fasihi kuanza kuhusisha michoro mabadilko mengine yalitokea katika karne ya 20 ambapo kulingana na Flora (1985) fasihi ilianza kuhusisha picha za watu halisi katika uwasilishaji wake katika kile anachokiita fotonovela. Fotonovela zilizovuma ni: *Killing* ya kule Uitaliano, *Jackie* kule Uingereza na *Harvey Kurtzman's Help* kule Marekani. Kulingana na Kimani wa Wanjiru (2018) kati ya miaka ya 1990 hadi 2000 hapa Afrika kulikuwa na fotonovela kama vile *Lance Spearman, Son of Samsom* na *Big Ben.*

Kutokana na maelezo haya basi ni dhahiri kuwa fasihi ipo daima katika hali ya mabadiliko yanayotokana na mabadiliko ya jamii. Hasa mabadiliko yanayoletwa na maendeleo ya kiteknolojia. Fasihi imepitia mabadiliko kutoka fasihi simulizi, kisha fasihi andishi, kisha fasihi inayohusisha michoro na sasa fasihi inayohusisha picha. Ni muhumu kutaja hapa kuwa, muungano wa hayo yote ni kazi ya *Shujaaz* kwani ina husisha haya yote. Yaani, ndani mwake mna maandishi, mna michoro ya katuni, mna picha za watu halisi na mna nafasi ya mawasiliano kati ya hadhira na msanii. Utafiti huu unanuia kutambulisha sifa hizi bainifu za *Shujaaz.*

Utafiti huu unalenga kuonyesha namna ambavyo *Shujaaz* inaweza kuhakikiwa kwa kutumia vigezo vya fasihi kwa kuchunguza maudhui na fani zake. Katika kufanya hivi itabidi kuiweka *Shujaaz* katika mizani ya kifasihi ambayo ni vigezo vya uhakiki wa kazi ya fasihi, hasa fasihi andishi. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (2011), kwa vile kazi ya fasihi husawiri jamii katika mfumo mzima wa maisha ya jamii na shughuli zinazofanywa katika jamii husika, basi ni muhimu kuzingatia yafuatayo katika kupima kazi ya fasihi:

Ukweli wa mambo yanayoelezwa – mhakiki kama hakimu na daraja atawajibika kuthibitisha ukweli wa kutendeka kwa yaliyoelezwa katika kazi hiyo. Kama anahakiki habari kuhusu ubakaji au rushwa – Anapaswa kujiuliza, uwapo ni kweli kuwa mambo hayo yapo katika jamii. Uhalisia wa watu, mazingira na matukio katika jamii. Hapo mhakiki analinganisha wahusika wa kazi husika na watu halisi ili kuona kama jamii zungumziwa ina watu wanaotenda kama wahusika waliotumika. Umuhimu wa kazi hiyo kwa jamii husika lazima uzingatiwe. Jambo linalozungumzwa linaweza kuwa la kweli na lina uhalisia.

Vigezo ambavyo hutumika kupimia vipengele vya maudhui katika kazi ya fasihi vikiwa ni: dhamira, ujumbe, migogoro, mafunzo na falsafa. Navyo vigezo vya fani vikiwa ni: muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika, na mandhari. Uchunguzi wa *Shujaaz* basi kama fasihi utajikita katika vigezo hivi. Kwa kifupi *Shujaaz* ni toleo la kila mwezi ambalo lina muundo wake wakipekee unaohusisha maandishi, picha michoro na fasihi simulizi iliyoandikwa. Kazi hii ni muungano wa kazi za watunzi wanne ambapo kuna kazi ya D.J. Boiye, Maria Kim, Charlie Pele na Malkia. Kila ktunzi akiwa na nafasi yake katika kila matoleo. Mandhari ya kazi hii inahusu matukio ya nyakati hizi katika jamuiya za maeneo ya mjini na mashambani hasa katika makazi ya tabaka la wastani na lile la chini. Wahusika waliotumiwa kwa wingi ni vijana jambo linalotuelekeza kwa hadhira lengwa ambayo ni vijana na chamngamoto wanazopitia maishani katika shughuli zao za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Lugha inayotumika katika matoleo ya *Shujaaz* ni mchanganyiko wa kiswahili na Sheng pengine kutokana na hadhira lengwa.Watunzi wametoa nafasi kwa hadhira kuwasiliana na fanani kupitia kutuma maswali au maoni, mwishoni mwa kila sehemu kwa kutumia jumbe fupi za simu kupitia numbari 20308 bila malipo. Hili ni jambo ambalo halipo katika kazi yoyote ya fasihi ya Kiswahili isipokuwa katika *Shujaaz*. Hili ni jambo geni ambalo linadokeza upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi. Upekee huu unachochochea ari ya kutathmini *Shujaaz* kama kazi fasihi ya Kiswahili yenye upekee miongoni mwa kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili. Upekee huu upo katika muundo, mtindo, lugha, wahusika na mandhari ya kazi ya *Shujaaz*.

Kazi hii ya *Shujaaz* kwa kuitazama tu bila kufasili inayowasilisha na kuwakilisha inaweza kupuuzwa kuwa kazi ya kitoto isiyo na ujumbe mzito wowote lakini ikitazamwa kwa jicho la kifasihi na kufasiliwa hapo basi utangamua kuwa kuna mengi ambayo ni mazito na yanayozidi

burudani ya kusoma *Shujaaz*. Mambo hayo yanayoibuka unapoifasili *Shujaaz* yanachochea ari ya kutaka kuhakiki kazi hii kama matini nyingine ya fasihi.

**1.2 Mada ya Utafiti**

*Shujaaz* ni zao la mabadiliko ya fasihi na inahusisha mseto wa sanaa zikiwemo lugha, michoro na picha na teknolojia. Matumizi ya mseto huu wa sanaa tofauti katika kazi ya *Shujaaz* unaipa kazi hii upekee unaoitenga na kazi nyingine za fasihi. *Shujaaz* ilivyoumbika inadhihirisha sifa ambazo huenda zikawa bainifu kama ilivyowasilishwa, ikilinganishwa na kazi nyingine za fasihi andishi ambazo ni riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Uwezekano wa kuhakiki *Shujaaz* kwa vigezo vya fasihi andishi ni jambo ambalo linafaa kuwekwa wazi; ikichukuliwa kuwa *Shujaaz* ni mseto wa sanaa zinazopitisha ujumbe yaani michoro, picha, maandishi, matumizi ya rangi tofauti na hata uwepo wa nafasi ya hadhira na fanani kuwasiliana kwa kutumia ya teknolojia ya mawasiliano ya jumbe fupi. Kwa hakika *Shujaaz* inajitenga na fasihi andishi nyingine kimuundo na jinsi inavyowasilishwa na upekee huu ukifafanualiwa kwa undani zaidi huenda ukafaa kuleleweka zaidi wa kazi hii. Shujaaz kama matini ya fasihi inafaa kufasiliwa kama kazi ya fasihi.

**1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuonyesha kuwa *Shujaaz* ni kazi ya fasihi ya Kiswahili. Madhumuni mahususi yakiwa ni:

i) Kutambulisha na kuainisha sifa bainifu za *Shujaaz* kama kazi ya fasihi.

ii) Kuhakiki *Shujaaz* kama fasihi kwa kutumia vigezo vya uhakiki wa fasihi ya Kiswahili.

iii) Kubainisha na kutathmini upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili.

**1.4 Maswali ya utafiti**

i) *Shujaaz* ina sifa zipi bainifu zinazoibainisha kama kazi ya fasihi?

ii) Vigezo vya uhakiki wa kazi ya fasihi vinadhihirisha yapi vinapotumiwa kuhakiki

*Shujaaz* kama fasihi?

iii) Upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili unaweza kubainishwa na kutathminiwa?

### 1.5 Umuhimu na Sababu za Kuchagua Mada hii.

Utafiti huu unatarajiwa kuwa na manufaa anuai. Utafiti huu unatarajiwa kuwa na mchango wa kinadharia ambapo utachangia maarifa ya matumizi ya nadharia husika kwa minajili ya kuhakiki kazi za fasihi. Kiutekelezi, utafiti huu unatarajiwa kurahisisha uelewa wa kazi ya *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu pia yanatarajiwa kuwa mchango kwa tafiti nyingine zitakazohusu *Shujaaz*. Uhakiki wa *Shujaaz* unatarajiwa kuwa na matokeo yatakayokuwa mwongozo kwa yeyote ambaye angependa kujua maudhui na fani zilizotumiwa katika *Shujaaz.* Utafiti huu pia unatarajiwa kuonyesha upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi hasa katika suala la matumizi ya teknolojia na sanaa nyingine katika kazi ya fasihi.

### 1.6 Upeo na Mipaka

*Shujaaz* ni sehemu ya jukwaa la aina anuai za mawasiliano zikiwemo *Shujaaz FM Radio, Shujaaz TV* na kurasa katika mitandao ya kijamii ikiwemo *Facebook, Instagram, WhatsApp, Twitter, SMS, You Tube* na *www.Shujaaz.fm*. Upeo wa utafiti huu unajikita katika matoleo ya *Shujaaz.* Kwa vile matoleo ya *Shujaaz* yamefikia matoleo 130 kufikia Januari 2021 na bado matoleo yanatolewa kila mwezi, utafiti huu umeshughulikia matoleo 13 ambayo yameteuliwa kimaksudi kukidhi madhumuni ya utafiti huu. Utafiti umeshughulikia kubainisha sifa bainifu za *Shujaaz* kama kazi ya fasihi, kisha utahakiki kazi ya *Shujaaz* kwa kutumia vigezo vya uhakiki wa fasihi za Kiswahili na kisha kutathmini upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya mipaka iliyokwamiza utafiti huu ni wingi wa matoleo ya *Shujaaz* ambayo kufikia Januari 2021 yalikuwa 130 na bado yanazidi kuchapishwa kila mwezi. Ili kuweza kutatua kikwazo hiki, utafiti huu ulishughulikia matoleo 13 kati ya yale yaliyopo kufikia Januari 2021 kuwakilisha matoleo hayo mengine.

### 1.7 Ufasili wa Dhana

**Hieroglifu**: Picha au alama ya kitu inayowakilisha neon, sauti au silabi iliyotumiwa katika maandishi ya kale kama vile ya wamisri

**Shujaaz**: Utohozi wa neno Shujaa katika *Sheng*. Anwani ya kitabu cha katuni kinachoandaliwa na kuchapishwa na kampuni ya *Well Told Story* na ambayo ni neno la *Sheng* lililotoholewa kutoka neno la Kiswahili 'Shujaa'

**Mchongoano**: Ni kijipera cha mazungumzo kilichoasisiwa au kuhuishwa na vijana na watoto wa leo.

**Fotonovela** : Utungo unaotumia picha za wahusika kusimulia hadithi yake

**Ujinga ni?**: Ni kipera kingine cha sanaa jadiiya ya watumiaji wa Sheng na hudhamiria kuonyesha upuzi au upumbavu wa kushikilia imani fulani au kufanya vitendo fulani.

**Sheng:** Msimbo huu hutawala usemi wa vijana na hata watoto katika viwango vyote vya elimu kuanzia shule za chekechea, msingi, sekondari na hata vyuo vikuu

**Toleo**: Chapisho la Shujaaz ambalo hutolewa kila Jumamosi ya kwanza ya mwezi.

**Chapta** : Kila toleo la Shujaaz huwa na Numbari yake tambulizi kwanzia toleo la kwanza ambalo lilitambulishwa kama chapta 1, toleo la pili chapta 2 kwendelea.

**Kibonzo**: Mchoro au michoro ya picha kwenye paneli moja ambayo hukusudia kusimulia hadithi kwa kuchekesha na aghalabu huambatanishwa na maandishi.

**Vikatuni**: Kundi la michoro ya picha kwenye paneli zaidi ya moja ambayo inasimulia hadithi na maandishi kama maelezo ya michoro ya picha hizo.

**Paneli:** Sehemu ambayo picha ya michoro ya vibonzo au kibonzo hupatikana.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandishi ambapo utathmini wa tafiti za wasomi mbalimbali waliyoshughulikia mambo yanayohisiana na utafiti huu umefanywa. Mapitio haya kimahususi ni maandishi yanayohusu *Shujaaz* kama toleo la kila mwezi la kampuni ya *Well Told Story* na *Shujaaz* kama kazi ya fasihi. Katika sehemu hizo mbili mapengo yaliyopo kuhusiana na utafiti huu yalionyeshwa. Mawazo ya wasomi mbalimbali ambayo yanashahibiana, yanayotofautiana na yaliyosaidia kuendeleza kazi hii kuhusu *Shujaaz* kama kazi ya fasihi. Sehemu ya pili ya sura hii ni ile ya msingi wa nadharia. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ile ya Metausasa.

## 2.2 Yaliyoandikwa kuhusu *Shujaaz*

Kulingana na Boiye (2018) *Shujaaz* ni sehemu ya jukwaa la aina tofauti za upashaji habari ikiwa na lengo la kuinua na kuimarisha hali ya maisha ya vijana katika Afrika Mashariki. Kupitia mahojiano kuhusu *Shujaaz* na msanii wa vibonzo Daniel Muli katika *African Digital Art* (2018) *Shujaaz* ni kijitabu cha kurasa 32 cha masimulizi ya hadithi ambacho kinatumia Kiswahili sanifu na lugha ya *Sheng*. *Shujaaz* ina wahusika wakuu wanne Boyie na Maria Kim (picha zao zilichorwa na Eric Muthoga), Malkia (akichorwa na Naddya Oluocha-Olunya) na Charlie Pele (picha zake zilizochorwa na Daniel Muli akisaidiwa na Movin Were na Joe Barasa). Kitabu hiki kina picha zilizochukuliwa kwa kamera za watu halisi zikihusishwa pamoja na zile za kuchorwa. Muli alieleza kuwa mnamo mwaka wa 2009, Rob Burnet Mkurugenzi wa kampuni ya *Well told Story Group*, alianzisha *Shujaaz* kama sehemu ya jukwaa mseto la machapisho ya kijitabu cha *Shujaaz,* idhaa ya redio ya *Shujaaz Fm*, na mtandao wa jumbe fupi (*SMS media*) kama njia za kuwasilisha jumbe za kielimu na mafunzo kwa hadhira. *Shujaaz* huwasilishwa kwa lugha ya Kiswahili iliyochanganywa pamoja na *Sheng*. Kile ambacho mahojiano haya hayakujihusisha nayo ni wajibu wa *Shujaaz* katika fasihi andishi ya Kiswahili. Mahojiano haya pia yanafahamisha kuhusu sifa bainifu za *Shujaaz*, mbinu za kisanaa na lugha zilizotumiwa katika kitabu cha *Shujaaz* na namna lugha ya ishara ya picha na michoro na ya *Sheng* ilivyotumiwa katika. Maelezo haya ya Boiye na Muli yanatoa maelezo mafupi kuhusu namna ambavyo *Shujaaz* ilianza, wasanii wake na baadhi ya sifa za *Shujaaz*. Kile ambacho hawakufanya na ambacho utafiti huu umejaribu kufanya ni kueleza kikamilifu nini kilifanya *Shujaaz* kuanzishwa. Pia, lengo na madhumuni yake ni nini kulingana na waanzilishi wake,

kulikuwa na changamoto zipi ilipoanzishwa na walikabiliana nazo vipi, *Shujaaz* imefikia yapi katika mafanikio yake na ni mabadiliko yapi yametokea katika *Shujaaz*tangu kuzinduliwa kwake.

Kwa mujibu wa McConnell (2009), neno *Shujaaz* ni neno la *Sheng* lenye maana ya Kiswahili ya Shujaa. *Shujaaz* huwa ni kijitabu kinachopewa wasomaji wake bure kinachotolewa mara moja kwa mwezi, husimuliwa katika vipindi vya redio vya kila siku, maonyesho ya televisheni, mitandao ya umma, jumbe fupi za simu, na mtandao. Kulingana na DIAL & Echo Mobile (2018), inakisiwa kuwa *Shujaaz* inashabikiwa na asilimia 40 ya Wakenya wa umri wa kati ya miaka 15-24. Kutokana na utafiti huru uliofanywa 2018 *Shujaaz* imejishindia tuzo tofauti za *International Emmy Award*- 2012 na 2014, kupendekezwa kushindania tuzo la *International Emmy Award* 2013 kwa kuhusishwa na hadithi iliyoitwa *Jongo Love*, ambapo pamoja na *Jongo love* zikashinda tuzo la *One World Media Award* mwaka wa 2012 na 2013 mtawalia. Maelezo haya ya McConnell (2009) yanadokeza ufanisi ambao Jukwaa zima la *Shujaaz* limeyapata. Pengo lililopa hapa ambalo McConnel hakulizingatia ni kutambulisha sifa bainifu za *Shujaaz*, kubainisha uwezekano wa *Shujaaz* kuhakikiwa kama fasihi ya Kiswahili na kutoa tathmini ya upekee uliopo katika *Shujaaz* kama kazi ya fasihi.

Kulingana na jarida la *New Agriculturist* (2011), kijitabu cha *Shujaaz* husawiri maisha ya wahusika wakuu wanne. *Shujaaz* huhimiza na kuwawezesha vijana kuwa mashujaa katika jamii zao. Inakisiwa kuwa kila nakala ya *Shujaaz* husomwa na watu ishirini wengi wakiwa kati ya miaka 11- 18 ambapo mbinu mpya za kilimo huwasilishwa kwa vijana. Mashirika ya *Partner Organization FIPS-Africa* na DFID *Research* yalishirikiana na *Shujaaz* kurahisisha na kusambaza jumbe za mbinu za kilimo kupitia kitabu hiki cha hadithi na vibonzo nchini. Kwa mfano, hadithi ya kuwapaka vifaranga rangi ya zambarau ili wasichukuliwe na mwewe, ukuzaji wa sukuma wiki na mbinu ya kulowesha mbegu kabla ya kuzipanda. Pia wanaeleza kuwa *Shujaaz* hulenga kuoanisha burudani na masomo au mafunzo. Kuna machapisho matatu maalum yaliyochapishwa kuhusiana na kura ya maoni ya mabadilisho ya katiba mwaka wa 2010 kwa ushirikiano na Tume Huru ya Mipaka ya Uchaguzi Nchini (IEBC). Kulingana na jarida hili la *New Agriculturist* (2011) *Shujaaz* imekuwa kichocheo cha kukuza na kuimarisha mawazo kuhusu biashara na namna ya kupata mikopo ya kuanzisha biashara. *Shujaaz* pia hupiga vita, ukabila na kuhimiza uzalendo. Maelezo haya yanatoa mfano wa majukumu yaliyotambuliwa kutekelezwa na *Shujaaz* na baadhi ya maudhui yanayopatikana katika *Shujaaz*. Haya ni

mambo muhimu kwa utafiti huu kwani yanatoa fursa kwa utafiti huu kuzingatia majukumu na maudhui mengineyo ambayo hayakushughulikiwa. Kulingana na Dayo (2014) *Shujaaz* ni kijitabu cha katuni ambacho nia yake ni kusuluhusha na kuelekeza jamii. Anasema kuwa kijitabu kimoja cha *Shujaaz* chaweza kusomwa na wengi kutokana na mvuto wa picha, vituko vilivyopo na hasa lugha waipendayo wasomi wake ya *Sheng*. Dayo (2014) asema kuwa nakala 600,000 za kijitabu hiki husambazwa bure na huwafikia wasomaji milioni 10. Hali hii inayofanikiswa kupitia mbinu ya kuwafikia wasomaji katika idhaa ya DJ Boiye ya *Shujaaz FM*. *Shujaaz FM* hupeperushwa na idhaa ishirini na nne tofauti nchini Kenya kila siku. Dayo anadai kuwa *Shujaaz* ina nafasi muhimu ya kielimu kwa vijana walio kati ya miaka 16 hadi 26 ambao wako au wameshatoka shuleni na vyuoni. Kwa waliotoka shuleni na vyuoni *Shujaaz* huwapa nafasi ya kuendelea kujielimisha kwa kuweka darasa katika kijitabu hiki uk. 90-cha *Shujaaz.* Aliyoeleza Dayo (2014) ni muhimu kwa utafiti huu kwani yanatambulisha baadhi ya sifa na takwimu muhimu kuhusu *Shujaaz*. Haya ni mambo ambayo yameshirikishwa katika utafiti huu. Mbali na hayo sifa zaidi kuhusiana na muundo na mbinu mbalimbali za uwasilishaji na majukumu yanayotekelezwa na sehemu mbalimbali za *Shujaaz* ni mambo ambayo utafiti umeshughulikia kwa kutumia vigezo vya uhakiki vya fasihi.

Kwa mujibu wa Hutchinson na wenzake (2019) *Shujaaz* hutafuta kuimarisha maisha ya vijana nchini Kenya kwa kuchochea na kuimarisha mbinu mwafaka za kuimarisha afya yao na kuhimiza mbinu mwafaka za kujiinua kiuchumi. Hutchinson na wenzake walichunguza athari ya *Shujaaz* miongoni kwa vijana. Uchunguzi ambao waliufanya kwa kipindi cha miaka miwili wakihusisha vijana mia saba wa umri kati ya miaka 15 na 24. Walitafuta kujua namna kijitabu cha *Shujaaz* na idhaa ya redio ya *Shujaaz Fm* pamoja na mitandao ya digitali ya *Shujaaz* katika mitandao ya umma na utumizi wa jumbe fupi za simu zilivyoathiri mtazamo, maadili na tabia ya vijana katika maswala ya upangaji uzazi na uzalishaji mali. Utafiti wao pia ulidhihirisha kuwa baada ya kupokezwa mbinu za kuimarisha uzalishaji mali mapato ya waliopata mbinu hizi yaliongezeka kwa shilingi 2,096 kila mwezi. Hutchinson na wenzake (2019) wanaeleza kuwa kijitabu cha *Shujaaz* kina dhima kinazotekelezwa katika jamii mojawapo ikiwa takwimu za kufanikiwa kwa *Shujaaz* katika kubadilisha tabia miongoni mwa vijana. Maelezo haya ni muhimu kwani yamekuwa sehemu ya maudhui na fani katika *Shujaaz* ambayo imechunguzwa na utafiti huu.

## 2.3Tafiti kuhusu kijitabu cha *Shujaaz* kama Fasihi

Katika sehemu hii Ngugi (2018) alitafiti kuhusu matumizi na uamilifu wa *Sheng* katika muktadha wa taaluma ya fasihi, hasa ikichukuliwa kuwa fasihi huelimisha na kuburudisha. Anaeleza kuwa *Shujaaz* ni chapisho linalolenga kuwaelimisha na hata kuwaburudisha vijana katika jamii kwa kupitia msimbo wa *Sheng* na mitindo changamano ya uwasilishaji wa ujumbe huo. Utafiti huu wa Ngugi (2018) umeelezea matumizi ya lugha ya *Sheng* katika *Shujaaz* kwa kuangalia ilivyofanikisha mazungumzo mbalimbali kama ilivyotumiwa na wahusika tofauti kitabuni. Utafiti huu ulichota baadhi ya aliyoshunghulikia kuhusiana na *Sheng* katika kutafiti sehemu ya fani na matumizi ya lugha katika *Shujaaz*

Ngugi (2018) anaeleza kuwa, katika *Shujaaz* kitanzu cha *'Mchongoano'* na mafumbo hubainika kama njia ya kujiburudisha miongoni mwa vijana. Kile ambacho hakufanya ni kueleza mchongoano na upekee wake kama unavyotumika katika kazi hii ya *Shujaaz*, jambo ambalo utafiti huu umejaribu kueleza hasa ukiegemea suala la fani ya muundo na mtindo. Pia hakushughulikia '*Ujinga ni?'* ambayo ni fani nyingine iliyotumiwa kitabuni. Kila ambacho hakijazingatiwa hapa ni kuwa Ngugi ametaja tu uwepo wa fani ya *mchongowanoo* na ile ya *Ujinga ni?* Japo hajatoa mifano, hajaeleza sifa na upekee wa fani hizi katika *Shujaaz.*

Ngugi (2018) anaelezea kipengele kingine cha kiubunifu katika muundo cha kutoa nafasi kwa wasomaji kuuliza maswali mbalimbali katika *Shujaaz* kuhusu namna ya kukabiliana na hali mbalimbali za maisha. Kwa mfano, maswali ya mapenzi, (CHAPTA 49), au wanapewa nafasi ya kusimulia jambo fulani lililowapata wao au mtu fulani wanayemjua. Wasomaji wanapewa nafasi ya kutoa maoni na kuchangia katika kusimulia hadithi ile walioisoma na ambayo imewaguza kwa njia moja au nyingine kwa vile inavyadhihirisha hali halisi ya maisha yao. Kuhusiana na maelezo haya ya upekee wa kuhusisha hadhira, utafiti huu ulipiga hatua na kutafuta kujua kutoka kwa waandishi wanaowahusisha wasomaji katika sehemu zao husika changamoto wanazokumbana nazo kwa kuhusisha hadhira. Uhusishaji huu hufanikishaje kazi ya *Shujaaz* na ni mambo yapi ambayo hadhira hushiriki kuliko mengine na kwa nini. Swali la kimsingi la kutafitiwa hapa likiwa 'mbona kushirikisha hadhira?'. Haya ni maswali ambayo yamejibiwa na utafiti huu.

Uchunguzi wake Dimbu (2021) alipotafiti kuhusu uchanganuzi makinifu wa diskosia katika vikatuni vya *Shujaaz* alilenga kueleza namna muwala ulivyokuzwa katika vikatuni vya *Shujaaz*.

Vilevile amefafanua kuhusu mikakati ya mazoea ya kijamii na kutathmini jinsi mahusiano ya uwezo yalivyowasilishwa katika vikatuni vya *Shujaaz*. Utafiti wake ulifaa sana utafiti huu hasa katika kupata hoja zinazohusiana uhakiki wa fani na maudhui ya *Shujaaz* kama kazi ya fasihi.

Vartanova (2008) amezungumzia kuhusu mitandao ya kijamii *ikiwemo Facebook, Twitter, Whatsapp, Istagram, You tube* na namna ambavyo zinafanikisha mawasiliano baina ya Shujaaz na Vijana. Kwani kupitia kwake watunzi wa Shujaaz waliweza kupata maoni, ushauri na majibu yaliyoulizwa. Mitandao hii ikiwapa vijana nafasi ya kujieleza na kutoa maoni ya hatua ambazo wangezichukua endapo wangezipata katika hali ya wahusika katika hadithi hususan. Maelezo yake yatafaa sana kwani utafiti huu ulijikita katika matumizi ya yumbe fupi yaani *SMS* ambapo mtunzi amepeana numbari mahsusi (20308) ambayo hadhira yake ingetarajiwa kutoa maoni bila malipo yoyote.

## 2.3 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Metausasa. Nadharia ya Metausasa au baada ya usasaleo ni wazo uliyozinduliwa mnamo 1975 na Zavarzadeh anashikilia kuwa nadharia hii iliibuka kutoka uwanja wa kutathmini uzuri wa kitu. Mnamo 2010, dhana hii ilirejelewa tena na wasomi Timotheus Vermeulen na Robin van den Akker. Kulingana na Ciprian na wenzake (2015) wanaendeleza dhana hii kuwa metausasa ni jaribio la kuunganisha, kusawazisha na kuleta suluhisho la hali kinzani kati ya usasa na usasaleo. Caprian anaeleza kuwa, kiimsingi nadharia hii ni juhudi ya kuleta maridhiano na suluhu kwa matatizo au migororo iliyopo. Ni hatua ambapo kilicho muhimu sio kupinga bali ni juhudi za kutafuta suluhu kwa mambo yaliyopo katika jamii. Inahimiza na kukuza mawazo ya matumaini na uwezekano wa mambo. Inakuchochea mawazo ya 'Kesho itakuwaje ikiwa…', 'tunaweza kufanya nini ili…'. Yaani, ni mawazo razini ya kujenga, kuleta pamoja, kutafakari, mawazo ya kimantiki, ya kutafuta kutenda, kuwaza kabla ya mambo kutokea.

Nadharia hii ilifaa utafiti huu kwani inatoa mwongozo katika kufasili yaliyofanikisha kuafikia madhumuni ya utafiti huu. Kulingana na Abramson (2015) nadharia ya metausasa ina mihimili yake ambayo ni: Upatanisho, mabadilishano ya mawazo, kweli kinzani, usambamba, kuporomoka kwa masafa, wingi wa ubinafsishaji, ushirikiano, utata na utukiaji sawia na mwingiliano taaluma. Katika utafiti huu mihimili iliyotuongoza ni ile ya:

i. **Upatanisho**: Mhimili huu huhimiza kufanya kazi kwa pamoja kwa pande kizani kwa nia ya kuleta uelewa na ufahamu wa kile kinachozungumziwa ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa na kubalifu kwa nia ya kuleta suluhisho la pamoja na matumaini. Katika utafiti huu mhimili huu ulikuwa muhimu katika kufafanua sehemu ya fani kwa kuonyesha upatanisho wa sanaa tofauti; uchoraji, picha, na lugha simulizi na andishi na matumizi ya teknolojia ya simu katika kujenga kazi ya *Shujaaz*.

ii. **Mabadilishano ya mawazo**: Mhimili huu huhimiza dhana tofauti kushirikiana kuimarisha hali ya Maisha katika juhudi za kuboresha yaliyo ya maisha. Mhimili huu ulifanikisha uhakiki wa sehemu ya fani katika kuonyesha namna ambavyo uhusishaji wa sanaa tofauti za picha, michoro, fasihi andishi na simulizi pamoja na matumizi ya teknolojia ya simu umefaulu kuzaa kazi moja ya fasihi ambayo ni *Shujaaz*.

iii. **Kuporomoka kwa masafa**: Mhimili huu unaeleza uwezekana wa kuondolewa kwa kikwazo cha watu kutoweza kushirikiana kutokana na ubali au masafa yaliopo baina yao kumawazo, kiumri, kimaeneo, kimsimamo, kishughuli zo za kimaisha kijamii, kisiasa na kiuchumi. Nia hapa ikiwa kuleta watu pamoja na kufanikiwa uwepo wa ushirikiana na umoja japo kuna utofauti kati yao. Mhimili huu ulifaa utafiti huu katika sehemu ya kutathmini upekee wa kazi ya *Shujaaz* fasihi. Upekee wa kuunganisha hadhira na mtunzi wa *Shujaaz* kupitia jumbe fupi za simu, juhuzi za mtunzi kuonyesha inavyoweza kuleta malidhiano baina ya makundi yaliyo na mgogoro kisiasa na kijamii na juhudi ya mtunzi kuonyesha namna sanaa tofauti (uchoraji, picha, maandishi, teknolojia) zinaweza kuunganishwa na kuwasilisha ujumbe katika utungo moja wa kifasihi

iv. **Ushirikiano na mwingiliano taaluma**: Mhimili huu unaunga mkono juhudi zote za kubomoa, kupanga upya na kufaragua uwepo wa istilahi kama 'tanzu', 'vyama', 'idara', 'taaluma', 'taasisi' na nyinginezo zenye kuwekea mipaka tofauti na kutenganisha. Mhimili huu uliongoza katika kuhakiki fani na maudhui katika *Shujaaz* hasa katika kuchunguza namna kazi nzima ilivyopangwa kwa kutumia michoro, picha, uwepo wa sanaa za fasihi simulizi na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano ya simu katika kazi hii ya *Shujaaz*. Nyenzo hizi zikifanikisha kuipa kazi hii upekee ambao utafiti huu ulinuia kuufatitia na kuutathmini kama nyenzo za kifasihi.

Kwa mwongozo wa mihimili hii ya nadharia ya metausasa uliongoza utafiti hii kwa kuzingatia

vigezo vya kubainishia sifa ya kazi ya fasihi (uhusika, hadhira, muundo, msuko, ulahisia mazingaombwe/ fantasia, migogoro, maudhui na uadilishaji, ramsa, lugha, mtindo, motifu ya safari na mwonoulimwengu) ilikutimiza mahitaji ya dhumuni la kwanza la utafiti huu. Vilevile mihimili hii ilitoa mwongozo katika kutumia vigezo vya uhakiki vya kazi ya fasihi ambavyo maudhui (dhamira, ujumbe/maadili, mitazamo, migogoro, misimamo, falsafa na itikadi) na fani (muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika na mandhari) kukidhi mahitaji ya dhumuni la pili la utafiti huu. Kisha kuongoza vigezo vya kutathminia upekee wa kazi ya fasihi (muundo, mtindo, lugha, wahusika na mandhari.) kukidhi mahitaji ya dhumuni la tatu la utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, maswala kuhusiana na mbinu za utafiti zilizofanikisha utafiti huu yalishughulikiwa. Katika sehemu hii, vipengele vya muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, sampuli lengwa, njia ya kukusanya data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo umejadiliwa.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kiathamano mkabala wa kufasili yaliyomo. Kulingana na Kombo na Tromp (2006), muundo wa utafiti hutoa maelezo ya kuchunguza sifa zinazobainika katika jambo fulani linalochunguzwa. Kupitia muundo huu, utafiti huu ulikusanya data ya kimsingi kutoka matoleo yaliyoteuliwa kimaksudi ya *Shujaaz* na ukufasili data hiyo iliyohusiana na mada ya utafiti. Kisha data zililizopatikana zilichambuliwa kulingana na malengo ya utafiti huu.

## 3.3 Sampuli Lengwa

Sampuli katika utafiti huu iliteuliwa kimaksudi. Kwa mujibu wa Oso na Onen (2009) kuna mbinu mbalimbali za kuteua sampuli kutegemea aina ya utafiti. Mojawapo ya hizi mbinu ni mbinu ya kimaksudi pale ambapo mtafiti huamua nini ajumuishe katika sampuli kutegemea mahitaji ya madhumuni ya utafiti huu. Mbinu hii ilitumiwa kuteua sampuli ambayo ilizalisha data toshelevu katika kukidhi malengo ya utafiti. Kufikia Januari 2021 kuna machapicho 130. Kwa hivyo, uteuzi wa kimaksudi ulilenga usomaji wa machapisho 13 ya *Shujaaz* ambayo yanawakilisha asilimia 10 ya machapisho hayo. Uteuzi huu ulifaa kwani uliwezesha kupata mengi ya kuwakilisha matoleo hayo mengine. Mbinu hii vilevile iliwezesha uteuzi wa matoleo ambayo yaliyohusiana na mada ya utafiti na pia yalifanikisha malengo ya utafiti huu. Ufaafu wa mbinu hii pia ni kuokoa wakati na pesa. Matoleo yaliyoteuliwa yakiwa ni: CHAPTA 12, 27, 33, 57, 68, 73, 88, 93, 98, 102, 109 na matoleo maalum 01/30 na 03/03.

## 3.4 Mbinu ya Ukusanyaji wa Data

Mugenda (1999) ameainisha jinsi nne kuu za kukusanya data: hojaji, mahojiano, uhakiki wa maandishi, kuchunguza kwa kushuhudia. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kusoma machapisho yaliyokuwa yameteuliwa kimaksudi. Kisha, yaliyo muhimu kwa utafiti huu yalidondolewa kutoka machapisho yaliyosomwa na kufasiliwa. Data ya kimsingi ilitolewa moja kwa moja kwenye kila toleo lililoteuliwa kulingana na mahitaji ya malengo ya utafiti huu. Kwa

mfano, kama ni sifa za *Shujaaz*, hoja zilitolewa kwa kutoka kila toleo lililoteuliwa kwani kuna sifa zilizopo katika toleo moja lakini hazipo katika toleo lingine. Data ya sekondari ilitolewa katika kazi zilizo andikwa kuhusiana na *Shujaaz*. Kwa mfano kazi ya Ngugi (2017) ambayo inamaelezo kuhusu maudhui na matumizi ya lugha ya Sheng katika *Shujaaz* hoja ambazo ni muhimu kwa utafiti huu.

Kwa kuzingatia mahitaji ya madhumuni ya utafiti huu, nadharia ya metausasa kupitia mihimili yake iliongoza kukusanya data mwafaka. Ili kukidhi mahitaji ya dhumuni la kwanza maelezo ya kubainisha sifa bainifu za *Shujaaz* kama fasihi ya Kiswahili mihimili yote mnne itatumiwa pamoja na vigezo vya sifa za kazi ya fasihi kukusanya data inayodhihirisha sifa hizi katika matoleo ya *Shujaaz*. Vigezo hivi ya sifa vikiwa ni: uhusika, hadhira, muundo, msuko, ulahisia mazingaombwe/ fantasia, migogoro, maudhui na uadilishaji, ramsa, lugha, mtindo, motifu ya safari na mwonoulimwengu. Maelezo ya kutambulisha na kuainisha sifa bainifu za Shujaaz na mifano kutoka kwenye matoleo ya Shujaaz yaliyoteuliwa yalitolewa.

Kuhusiana lengo la pili la utafiti huu, kwa mwongozo wa nadharia ya utafiti huu pamoja na vigezo vya uhakiki wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi vikiwa maudhui (dhamira, ujumbe/ maadili, mitazamo, migogoro, misimamo, falsafa na itikadi) na fani (muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika na mandhari) Maelezo ya uhakiki wa *Shujaaz* kama fasihi kwa kuzingatia vigezo vya uhakiki yalitolewa yakiambataniswa na mifano mwafaka.

Kisha maelezo na mifano mwafaka ilitolewa kuhusiana na kubainisha na kutathmini upekee ya *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili yalitolewa kwa kuzingatia vigezo vya muundo, mtindo, lugha, wahusika na mandhari ili kukidhi madhumuni ya tatu ya utafiti huu. Kwa mfano mtindo aliyoutumia mtunzi wa Shujaaz wa kuchanganya maandishi, michoro/vibonzo, picha za watu halisi na lugha ya Sheng kwa upatanisho katika kazi moja ni upekee wa kimtindo.

Ni muhimu kutaja kuwa utafiti huu umetumia mbinu ya kuhakiki maandishi, picha na michoro iliyopo katika kila toleo lililoteuliwa kukusanyia data.

### 3.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa katika utafiti huu ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa kufasili data. Kulingana na Kombo na Tromp (2011) uchanganuzi na fasili ya yaliyomo unafaa ambapo utafiti unahusu data iliyopo katika maandishi. Kusoma matoleo yaliyoteuliwa pamoja na

makala tofauti yaliyotafitia *Shujaaz* kulifanywa ili kuchanganua dhana tofauti zilizotokana na data ya kimsingi na kisekondari iliyokusanywa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti huu.

Muundo wa kifasili ulikumika ili kuweza kupata maana iliyokusudiwa na mwandishi katika uwasilishaji wake kwa kuzingatia vigezo vya kubainisha sifa za kazi ya fasihi, vigezo vya uhakiki wa kazi za fasihi na vigezo kutathmini upekee wa kazi ya fasihi. Umuhimu wa mbinu hii ya kufasili ni kuwezesha upataji wa maelezo kuhusu ujumbe nuiwa kama ulivyowasilishwa na mtunzi kupitia maandishi, michoro, picha na mtindo wa lugha aliyotumia mtunzi wa *Shujaaz*.Baada ya kukamilisha kupanga kila kilichohitajika data ilitolewa kwa mtindo wa kinadhari katika sura. Kila sura ikishughulikia madhumuhi mahususi ya utafiti huu.

**3.6 Uwasilishaji wa Data**

Utafiti huu ni wa kithamano na data iliyokusanywa, kufasiliwa  na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo na kupangwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti yalipangwa na kuwasilishwa katika sura tofauti ifuatavyo: sura ya nne ikiwa na matokeo ya uchanganuzi wa data kuhusiana na sifa bainifu za *Shujaaz* kama fasihi ya Kiswahili, sura ya tano ikihusu matokea ya uchunguzi wa uhakiki wa *Shujaaz* kama fasihi ya Kiswahili na sura ya sita ikihusu upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi.

# SURA YA NNE

## SIFA BAINIFU ZA *SHUJAAZ* KAMA FASIHI YA KISWAHILI

### 4.1 Utangulizi.

Sura hii inachunguza *Shujaaz* ni nini, ina sifa zipi bainifu na kuzieleza. Ili kufanya hivi matoleo teuliwa yalisomwa na kwa mwongozo wa nadharia ya utafiti na kwa kuzingatia vigezo vya kubainisha sifa za kazi ya fasihi maelezo yatatolewa. Hasaa mhimili ya upatanisho, kuporomoka kwa masafa  na ule wa ushirikiano na mwigiliano wa taaluma. Mifano anuai ilitolewa moja kwa moja kwenye matoleo  yaliyochaguliwa kimaksudi ili kukidhi mahitaji ya dhumuni la kwanza na ufasili kutolewa.

### 4.2 Sifa za fasihi

Kulingana na Wamitila (2008) na Njogu akiwa na Chimerah (2008) kazi ya fasihi huwa na sifa zifuatazo:

a) Fasihi ni utanzu wa sanaa. Kuna aina tatu za sanaa: sanaa za ghibu (ni aina ya sanaa ambayo uzuri wake hujitokeza kwa kusikiliza. Mfano, muziki, mashairi), sanaa za maonyesho (ni sanaa ambayo uzuri wake hujitokeza katika kuuona. Mfano ni uchoraji, ususi na ufinyanzi) na sanaa za vitendo (Sanaa ambayo uzuri wake hujitokeza kwa kuona na kusikiliza mfano ukiwa maigizo na tamthilia).

b) Kazi ya fasihi husawiri vipengele vya maisha, mahusiano, na hisia za watu katika jamii husika.

c) Fasihi ni ufundi unaotumia lugha ili kuleta mguso au hisia fulani za watu katika muktadha fulani.


d) Fasihi huweza kutolewa maelezo ya fani na maudhui.

### 4.3 Sifa za Shujaaz

*Shujaaz* ni aina ya kazi ya sanaa inayotumia lugha, michoro, picha, arafa kupitisha ujumbe husika kwa jamii iliyoikusudia. Wahusika wake huwasiliana kwa lugha ya Kiswahili, lakini Kiswahili kilichochanganyika na Kiingereza na pia kwa lugha ya Sheng. Mazungumzo mengi yanaendeshwa kwa kugha ya Sheng ambayo ni lugha ya vijana. Wahusika wengi ni vijana na pengine ndiyo sababu ya mtunzi kutumia lugha ya Sheng ambayo vijana wengi hujitambulisha kwayo. Vile vile Sheng hurahisisha mawasiliano baina ya vijana kwani huwavutia na hufurahia

kuitumia. Sheng haina urasmi na inawapa vijana uhuru wakutumia maneno bila kujali usanifu wa namna wanavyotumia lugha. Kwa njia hii kazi hii inafanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira lengwa. Matoleo yote yametumia mseto huu wa lugha. Hali hii inaleta upatanisho wa matumizi ya lugha tofauti katika kazi moja na kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Dhana hii ya upatanisho wa lugha tofauti katika moja na kuporomoshwa kwa masafa ya lugha ua mtaani na lugha rasmi kunachangia kuwepo kwa  mojawapo wa sifa bainifu ya *Shujaaz* kama fasihi kwani tanzu nyinginezo za fasihi hutumia Kiswahili pekee tena Kiswahili sanifu.

*Shujaaz* kama fasihi inatumia sanaa ya michoro kuwasilisha ujumbe pia. Michoro iliyopo ni michoro ya wahusika katika mazingira na makazi yao wakiendelea na shughuli na mahusiano yao ya maisha katika jamii. Michoro iliyopo ikionyesha mawasiliano baina ya wahusika kwani kuna kujibizana ambapo maneno ya wahusika yamewekwa kwenye vibofu vya maneno. Mfano ufutao kutoka CHAPTA 12 uk 6, wadhihirisha haya.





**Kielelezo cha 1: chapta 12 ukurasa 6**

Hisia na vitendo au maigizo ya mawasiliano yao na vitendo huwasilishwa kwa michoro.

Matumizi ya michoro kama mtindo wa mtunzi wa kuwasilisha ujumbe wake inaipa hii kazi sifa ya kazi za katuni/vibonzo ambazo hutumia michoro ya watu kama wahusika. Kwa mfano, katika ukurasa huu wa 6 wa chapta 12, Boiye anaonekana katika kituochake cha redio ya mtaani akizungumza na mashabiki wake akiwahimiza kuwa wametoka mbali kisha genge la vijana wanaojiita 'mateste wa Group ya vijanaa' wanafika kwake kudai ada ya ilinzi. Yaelekea kuwa Boiye nashangaa kutamba kiongozi wa kile kikundo hujipatia pesa kwa kudai pesa za ulinzi kutota kwa wakazi wa mtaa huo kwa kudai pesa za ulinzi kinyuma cha sheria na anaposema hana pesa wanashikwa mashati na kutishiwa.

Vilevile mtunzi wa *Shujaaz* ametumia sanaa ya picha hasaa picha za watu halisi ambao wamo katika jamii katika shughuli zao katika mandhari halisi wakiwa katika mazungumzo na wahusika wa kuchorwa. Utungo kama huu wa kutumia picha halisi za wahusika na mandhari yao hutumiwa



**Kielelezo cha 2: CHAPTA 57 ukurasa wa 8.**

katika vitabu vya fotonovella (vitabu vya picha za watu halisi kama wahusika). Tofauti na

fotonovella ambapo picha za wahusika wote huwa halisi katika *Shujaaz* mtunzi amechanganya picha halisi na zile za wahusika wa kuchorwa. Hii ni sifa bainifu ya matoleo ya *Shujaaz* kama kazi ya kifasihi. Mfano unapatikana katika CHAPTA 57 uk 8

Kutokana na mifano iliyopo hapa juu sifa zifuatazo zinajidhihirisha:

a) kuwa *Shujaaz* vilevile hushirikisha sanaa ya vitendo kama ilivyo katika maigizo na tamthilia. Msomaji anaweza kusoma yanayosemwa na wahusika wanapojibizana na kuwasiliana na pia anaweza kuona vitendo vyao.
b) Kuna mazingira ya uhalisia wala sio ya kubuni au kidhahania
c) Kuna wahusika hai waliopigwa picha na kuonekana wakizungumza na mhusika wa kuchorwa. Hali inayoleta dhana ya upatanisho wa hali halisi na sanaa ya uchoroji
d) Mazingira yaliyotumiwa yanaweza kuakisi hali halisi ya jamii hiyo kusudiwa
e) Mbinu ya usemezano/ udayolojia imetumika kufikisha dhima ya mojawapo ya *Shujaaz.*
f) Ukichunguza kwa umakini utagundua kuwa kila sehemuya picha au paneli imebeba ujumbe fulani. Kwa mfano paneli ya kwanza imebeba ujumbe wa uwajibikaji, ya pili dhima/jukumu la *Shujaaz* la kuwa jukwaa la kuwapa wanajamii nafasi ya kujieleza na kumegea wengine tajriba zao za maisha na ya tatu ikihamasisha vijana wawajibike na kuzinduana kuhusu ni lipi wanaloweza kulitenda kuboresha maisha yao kiuchumi na inaonyesha kuwa ni muhimu vijana ambao wako kazi baada ya kupata ushawishi na nasaha kwa vijana mwenzao wanavyofaa kujituma na kurajesha fadhila kwa jamii.
g) Mbinu za mawasilianao kwa kutumia mitandao ya kijamii imetolewa pale chini ya ukurasa huu. Hii ni nafasi ambayo hadhira inapewa kuuliza maswali na kupata ushauri kutoka kwa mtunzi wa kazi ya *Shujaaz*. Hii ni sifa mpya ya kifani katika fasihi lililopo katika *Shujaaz*.

### 4.4 Sifa ya usawiri vipengele vya maisha, mahusiano, na hisia za watu katika jamii.


Kulingana na wamitila (2008) fasihi huakisi yanayotukia katika jamii na Shujaaz kama ilivyo tanzu nyingine za fasihi nyingine huakisi yanayoendelea katika jamii na kuyawasilisha kiubunifu kupitia matoleo yake. Kila toleo likiwa na yale ambayo huwa linaakisi katika jamii. Kwa mfano katika CHAPTA 88, sehemu ya kwanza uk 2-7, inahusu tamasha za uigizaji katika shule anamosomea mhusika Malkia katika eneo la pwani. Uwepo wa minazi ni ishara kuwa mandhari ni ya pwani. Na ni tamasha za shule kwani wahusika wamevaa sare za shule na kuna madarasa

na chumba cha maakuli. Sehemu hii inaakisi maisha shuleni wakati wa tamasha za uigizaji na baadhi ya changamoto ambazo shule hupitia katika hatua ya kufanikisha tamasha hizo. Mtunzi analenga kuhimiza kuwa shuleni ni pahala muhimu pa vijana kukuzia talanta zao za uwigizaji na wanafaa

kuungwa mkono na kusaidiwa kwa kila hali. Sehemu hii vile vile imeangazia changamoto la mahusiano ya kimapenzi baina ya wanafunzi shuleni kama uhusiano uliopo baina ya Venessa na Juno. Mtunzi anatoa mfano wa jinsi wazazi wanavyopasa kushughulikia swala hili ili kuepusha mgogoro kati yao na watoto wao walioshuleni lakini wanajihusisha kimapenzi kama ilivyo katika

ukurasa wa 7. Anapendekeza utoajiwa ushauri kulikokukemea. Mtunzi katika ukurasa wa 7 anatoa nafasi kwa hadhira kutoa ushauri na maoni kupitia alafa fupi kupitia numbari 20308 kuhusiana na

swala hili la mahusiano ya kimapenzi kwa vijana shuleni. Kunaahadi ya zawadi ya Shilingi elfu moja kwa yeyote atakaye tuma alafa. Hizi ni sifa bainifu za shujaaz kuwa hadhira inatarajiwa kushiriki katika kushauri na kuelekeza katika masuala ya mahusiano kati ya vijana katika jamii.



**Kielelezo cha 3: Chapta 88 ukurasa wa 7**

Sehemu ya pili ya Maria Kim uk 9-14, inahusu changamoto za mahusiano baina ya vijana kama ilivyo baina ya Sifa na mpenziwe hasa kuhusiana na swala la kwenda katika kituo cha afya ili wapatiwe ushauri na kupiwa hali yao ya kiafya kabla hawajaingiliana kingono. Sifa akisimulia kuhusu kifo cha dadake ilichotokana na kuavya mimba. Mpenziwe Sifa hataki kutumia kinga ya kuzuia ujauzito na anaombwa kufika kituo cha Future Fab kwa ushauri. Katika sehemu hii tunaona namna vijana wanasaidiana kujijali na kujichunga kwa mahusiano kwa nia ya kuboresha maisha yao ya sasa na kesho. Slim akishauri mpenziwe Safi naye Maria Kim akimshauri Safi.

Katika sehemu ya tatu ya D.J Boiye uk 15-16, Boiye, June na Mose wanatoe maelezo au maoni kuhusu sifa za mke bora (wife material) na za mume bora (Husband material) lengo likiwa kuwahamasisha vijana wananuia kujiunga na taasisi ya ndoa wajue yakuzingatia. Boiye pia ndiye mhusika mkuu katika sehemu zinazofuata kuanzia uk 17- 23 inayohusu kazi mbovu ya vijana wanoeneza visa vya wizi wa mabavu na kuvunja moyo vijana wenzao wachapa kazi kwa kuwapora na kuwaibia. Mtunzi anapigia debe ofisi ya ombudsman kwa kutoa anwani ya barua pepe ambapo malalamishi kuhusi wa maovu katika jamii. Hapa mtunzi amsawiri changamoto za vijana katika pilkapilka za kujitaftia riziki.




**Kielelezo cha 4: Chapta 88 ukurasa ya 26**

Katika sehemu inayofuata uk 24-25 D.J Boiye anazungumza na mpigapicha mashuhuri Ronald Tonui ambaye anatoa tawasifu yake kuhusiana na kuanzisha biashara yake, changamoto alizopitia, kufaulu kwake na ushauri wake kwa vijana watafutao lakufanya maishani. Anahimiza umuhimu wa kujituma na kuwajibika iwapo mtu anataka kufaulu maishani.

Sehemu ya mwisho uk 26-31 ni sehemu ya Maria Kim ambapo anazungumzia kuhusu Profyam. Profyam ni lakabu ya kupewa kijana yeyote mjanja mwenye mipango kabambe ya kijijenga kimaisha. Pia na anafedha kiasi za kukuza na kuendeleza mipango yake kabambe. Maria anahimiza vijana kusaidiana na mawazo ya kuinuana kimaisha na kuhusiana kimapenzi. Mbali na maswala ya kujiimarisha kifedha Profyam ipo katika matandao wa kijamii wa *Facebook* ambapo kuna ukurasa unaojiita *LOVE AND HUSTLE* ambapo washiriki waliopo hujiita Profyam.

Kutokana na maelezo kuhusiana na CHAPTA 88 ni dhahiri kuwa mtunzi wa Shujaaz anajaribu kusawiri maisha ya vijana shuleni na mtaani na jinsi inafaa vijana wenyewe kuimarika katika kuyaboresha maisha na talanta zao. Sifa hii ya kiaskisi jamii inajitokeza waziwazi. Sifa bainifu hapa ni kuwa mtunzi amejikita katika kusawiri maisha ya vijana kwa kutumia wahusika vijana, kuangazia changamoto za maisha yao na hata kutumia lugha ya vijana ya sheng. Hali hii inaweza kufasilisiwa kuwa msimamo wa mtunzi kuhusu nafasi ya vijana katika jamii. Kuwa vijana wana nafasi kubwa katika kuiendeleza jamii.

### 4.5 Sifa ya Ujengaji/ Utambulishaji wa Fani na Maudhui katika *Shujaaz.*

Kwa mujibu wa Bakize (2014), Ngugi (2012), Senkoro (2006) na Wamitila (2008), kazi ya fasihi hukamilishwa kwa vipengele muhimu navyo ni fani na maudhui. Shujaaz nayo kana kazi ya fasihi ina sifa ya kujengeka katika vipengele vya fani na maudhui. *Shujaaz* kama fasihi ina sifa ya kujengeka katika vipengele vya fani na maudhui.

**a) Fani**

Kwa mujibu wa wataalamu na wahakiki wa fasihi; Mbatiah (2001), Wamitila (2003), Njogu na Chimerah (1999), fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Fani ni mbinu zote zinazotumika kuwasilisha maudhui katika kazi za kifasihi. Vipengele vya fani ambavyo ni: matumizi ya lugha, wahusika, mandhari, mtindo, muundo, muktadha na usuli. Vipengele hivi huitwa fani kwa sababu vyote huchangia pamoja katika kuwasilisha ujumbe (maudhui) kutoka

mwandishi hadi msomaji. Vipengele vinavyojitokeza katika Shujaaz ni kama ifuatavyo:

1. **Wahusika:**

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), wanaeleza kuwa, wahusika ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Mazingira haya yaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Wahusika hujadiliwa kwa namna wanavyoingiliana na dhamira na hili hujitokeza kutokana na maneno, tabia na matendo yao, yaani kulingana na hulka yao.

Hawa ni watu au viumbe vingine wanaotenda matendo mbalimbali katika kazi ya fasihi. Wahusika hawa hueleweka kutokana na matendo wanayoyatenda, namna wanavyo nena, wanavyosawiriwa na mtunzi au wahusika wenzao na pia kutokana na majina yao na hasa majina ya kimajazi huwezesha kuwajua na kuwaelewa vizuri. Wamitila (2008) anaeleza kuwa mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanadamu. Hii ndio maana neno 'mhusika' linatumika bali si 'mtu' au `kiumbe'. Wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mwandishi kubeba na kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi.

Katika *Shujaaz* wahusika waliotumiwa ni wale wa kuchorwa na wahusika picha halisi za watu hai. Hata hivyo, kuna wahusika aina mbali mbali wanaotumiwa katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa Ndungo na Mwai, (1991), Msokile (1993) na Wamitila (2002) wameainisha aina zifuatazo:

**(i) Wahusika Wakuu:** Mhusika mkuu hasa ni yule anayehusishwa katika kazi nzima tangu mwanzo hadi mwisho. Ukuu wa mhusika unatambulikana kuambatana na dhima aliyopewa na msanii. Hata mara nyingine mhusika mkuu hutumiwa na msanii kama kinywa chake. Yeye ndiye husema na kutenda msanii anayoyapendelea yaelewekekatika jamii. Wahusika wakuu wana umuhimu mkubwa katika kazi ya fasihi. Katika Shujaaz wahusika wakuu ni D.J BOIYE, MARIA KIM, CHARLIE PELE NA MALKIA. Wahusika hawa hutawala matukio katika sehemu zao katika kila toleo la *Shujaaz.*

**(ii) Wahusika Wadogo (Wasaidizi):** Hawa ni wahusika wanaomzingira mhusika mkuu na wanaomsukuma aamue au asiamue jambo kinyume chake.Wahusika hawa

hujitokeza hapa na pale katika kazi ya fasihi. Wahusika wadogo husaidia kuijenga dhamira fulani inayojadiliwa katika kazi ya fasihi. Hawa huchorwa sambamba na mhusika mkuu ili kusaidia hadhira kumwelewa mhusika mkuu zaidi. Wao husaidia kuyajenga maudhui fulani katika kazi ya fasihi. Lakini mradi tu wao wametumiwa kusaidia kuyajenga maudhui yale wao wangali wasaidizi tu. Mfano wa wahusika wasaidizi katika *Shujaaz* wahusika wasaidizi ni kama vile, FILO, SANGOMA, DOKI,CHUXX, J.K, RONSKI na NYAYA katika Chapta 33

**(iii) Wahusika Wajenzi:** Hili ni kundi linalotumiwa kujenga aina hizi zingine mbili za wahusika. Wao hasa hutumika kimsingi kuwakilisha jamii nzima ya kazi ile ya fasihi. Hawa ni wahusika ambao kwa kiasi kikubwa hutumika kwa lengo la kujenga au kukamilisha Maudhui ya kazi ya mwandishi. Pia hutumika kushirikiana na wahusika wakuu na wahusika wasaidizi. Wahusika wa aina hii huwa ndio wengi katika kazi ya fasihi katika kudhihirisha matukio au dhamira mbalimbali katika jamii. Kwa mfano wahusika ESTHER, MICH na DAN katika sehemu ya MALKIA (ukurasa wa 2-7 Chapta 68) wanakuza maudhui ya mapenzi na suala ka matumizi ya kinga za kuingiliana kimapenzi ilikuepuka kupata watoto kabra ya wakati ufaao. Katika Chapta 68 pia ukurasa wa 10-15 kuna mhusika picha kwa jina Joseph Barasa ambaye anaendeleza maudhui ya biashara kilimo.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999) wameainisha aina kuu nne za wahusika:

a) **Mhusika Mkwezwa:**Ni mhusika mwenye sifa za kiutendaji. Ni hodari na shujaa. Katika baadhi ya matoleo ya shujaaz kuna wahusika ambao ni mashujaa na wamepewa sehemu katika matoleo hayo ambao seheu hizi zinaitwa SHUJAA. Kwa mfano katika Chapta 57 ukurasa wa 3-8 kuna Shujaa DALTON WYCLIFFE ODHIAMBO ambaye ni mhusika picha wa kutoka sehemu ya Kibera Nairobi ambaye amesawiriwa kama shujaa wa kuhifadhi usafi wa mazingira. Katika Chapta 68 uk8-9 kuna sehemu ya Shujaa wa Mtaa kwa jina PAUL KUHUHA aka PROTISA ambaye ni Mhusika picha aliye shujaa katika biashara ya upigaji picha na uchukuaji wa vidio.

b) **Mhusika wa Kisaikolojia:** Huyu ni mhusika anayekumbana na matatizo mengi ya kijamii na anaibusha hisia za huruma kwa wasomaji. Mfano mzuri ni katika Chapta 27 uk 18-23 sehemu ya MARIA KIM ambapo kuna mhusika

picha FAITH NYAKUNDI ambaye aliambulia uja uzito na kujifungua mtoto akiwa mwanafunzi  na maisha magumu aliyoyapitia lakini hakukata tamaa maishani hadi alipofanikiwa maishani licha ya yale magumu aliyoyapitia katika gheto ya Mukuru Nairobi kwa sababu ya umasikini.

c) **Mhusika wa Kimapinduzi:** Huyu ni mhusika anayeelewa historia, siasa, mazingira na hali ya kiuchumi ya jamii yake. Yuko radhi kujitoa muhanga kubadilisha maisha ya wanyonge. Ana itikadi kali na msimamo thabiti. Katika Shujaaz wahusika wote wakuu; DJ BOYIE,MARIA KIM, CHARLIE PELE na MALKIA, wanajitokeza kama wahusika wa kimapinduzi kwani katika kila sehemu wanapotumika katika kila toleo kuna tatizo mahsusi ambalo linaathiri jamii liwe wa kiuchumi, kisiasa au kijamii ambalo wanalenga kulitafutia suluhisho.


d) **Mhusika Jumui:**.Ni mhusika wengi katika mmoja. Hupatikana zaidi katika fasihi ya kidhanaishi. Mhusika huyo mmoja anakuwa na sifa za wahusika wengi. Anatumiwa kuonesha fujo za maisha. Hivyo anaitwa muhusika  jumui. Mfano muhimu ni "mimi" na "sisi". Katika Shujaaz hatuna aina hii ya wahusika.

Ujengaji wa wahusika kifani katika *Shujaaz* ni ujumuishaji wa wahusika wa aina mbili. Kuna wahusika wanaotajwa kitabuni (*Shujaaz*) na kuna wahusika ambao ni hadhira walioko nje ya kitabu. Sifa bainifu inayodhihirika kuhusiana na wahusika wa Shujaaz ni kuwa karibu wote ni vijana hasaa wa shule za upili (walioko shuleni) na wale waliomaliza shule ya upili (walioko mijini na mashambani wakitafuta au kafanya kazi zao au za kuajiriwa).

Hata hivyo *Shujaaz* ina sifa bainiafu ya kuhusisha hadhira kama sehemu ya wahusika wake. Katika Shujaaz hadhira ni sehemu muhimu sana ya wahusika na hadhira imehusishwa kama jambo la mwisho katika kila sehemu ya kila toleo. Hadhira inahimizwa kushiriki kwa kutuma maoni yao kupitia jumbe fupi za simu bila malipo na kwa kutunzwa kwa zawadi ya shilingi elfu moja kwa wanatuma maoni yao. Hadhira kuu ya kazi ya *Shujaaz* ni vijana.

Kazi yoyote inayolenga kuwavutia hadhira ya vijana. *Shujaaz* imetimiza haya kwa kuwa na mambo kama: Picha za watu halisi na mashuhuri kama vile Dr. Ofweneke, Govi, Victoria Kimani na wengine, Michoro ya katuni au vibonzo ya wahukia wote wakuu na wadogo wao, lugha yenye mvuto wanayojitambulisha nayo ya Sheng, mada zinazohusu maisha ya vijana kama vile mapenzi, umaarufu, usanii, michezo, elimu, mitindo ya mavazi, anasa na starehe, sherehe, kutajirika haraka, rangi za kivutia, masuala ya tekholojia kati ya mengine.

*Shujaaz* ina sifa ya kushirikisha hadhira kwa kuwapa nafasi ya kutoa maoni au mchango wao kuhusu mada husika mwishoni mwa kila sehemu. Sifa hii inakuza dhama ya uporomoshaji wa masafa hivi kwamba jambo ambalo linahusiaha taaluma mbili tofauti yaani fasihi na teknolojia zinafanya kazi kwa pamoja. Kwa mfano katika CHAPTA 88, uk 7, 14 na 31. Wasomaji wana nafasi yakuchangia na hata kujishindia zawadi ya shilingi elfu moja kwa kutuma maoni kwa kutumia ujumbe mfupi wa simu usiolipishwa chochote kupitia numbari 20308. Mtunzi wa Shujaaz anaibua sifa nyingine bainifu ya Shujaaz ambapo mtunzi hashirikishi tu hadhira yake moja kwa moja bali anatoa himizo la kushiriki kwa hadhira kwa kuwapa wanao shiriki nafasi ya kushiriki bila kughalamika na




juu yake anawapa zawadi.

**Kielelezo cha 5 Chapta 88 ukarasa wa 14.**




**Kielelezo cha 6 Chapta 88 ukurasa wa 14**




**Kielelzo cha 7 Chapta 88 ukurasa wa 31**

2. **Mandhari**

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mandhari hurejelea wakati na mazingira ya kijiografia ambayo yanakuwa msingi muhimu katika uandishi wa kazi za kifasihi. Mandhari huweza kuwa nguzo muhimu ya uhusika; pale ambapo matendo ya wahusika yanafungamana au hata kumotishwa na mazingira wanamojikuta. Mandhari huweza kufungamana kwa kiasi kikubwa na maudhui na dhamira zinazopatikana katika kazi inazohusika. Katika baadhi ya kazi za kifasihi mhusika anaweza kuchimuzwa au kuwekwa wazi au bayana kwa njia ambayo inadhihirika sana na mandhari, kwa upande wake, kufifizwa au kutokuwa wazi. Uhusiano unaotokea baina ya mhusika na mandhari unaweza ukawa wa kimpatano au ukawa wa kikinzani au ukazua mgogoro, kati ya mhusika na mandhari yenyewe. Wamitila (2008) anaeleza kuwa mandhari yoyote yale huwa msingi mkubwa wa matarajio yetu kuwahusu wahusika ,tabia zao, lugha zao, misukumo yao, aina zao n.k. Mtaalamu huu anaainisha mandhari katika aina mbalimbali kama vile; Mandhari ya kijiografia, mandhari ya kihistoria, mandhari ya kidhanifu/kinjozi, mandhari ya kiishara, mandhari ya kidokezi, na mandhari ya kiajinabi.

Kwa mjibu wa mlaga (2017), mandhari ni kipengele kingine cha kimuundo ambacho hurejelea mahali au makazi maalumu yaliyojengwa na mtunzi, na mnamo matukio au matendo mbalimbali ya wahusika wa kazi ya fasihi. Mandhari inaweza kuwa halisi au inaweza kuwa ni ya kubuni. Mandhari ni lazima iendane na maudhui yaliyokusudiwa. Kwa namna nyingine mandhari inaweza kutazamwa kama dunia au ulimwengu wa wahusika wa fasihi.

Katika *Shujaaz* mandhari tofauti yametumika. Kuna mandhari ya sehemu za makazi ya mjini kama anamkaa DJ BOIYE, kuna mandhari shule za mjini kama wanazosomea MARIA KIM na MALKIA, kuna mandhari ya mashambani yakiwakilishwa na anoishi CHARLIE PELE, kuna mandhari ya makazi ya sehemu za mabanda kama anakoishi MARIA KIM, kuna mandhari ya pwani. Wakati ulitumika katika *Shujaaz* ni wakati wa sasa kwani masuala ya teknolojia na yanayoendela katika jamii hivi sasa yanajitokeza katika kila toleo. Jumuiya aliyotumia mtunzi ni jumuiya ya vijana. Vijana wa shule,


vijana wa mashambani, pwani ya Kenya na hata sehemu za mjini Nairobi.

Sifa bainifu kuhusiana na mandhari ni kuwa kila toleo lina sehemu tofauti zinazohusisha mandhari tofauti. Kwa mfano, katika CHAPTA 93, sehemu ya kwanza inahusu Maria Kim na mandhari ni hotelini wanamofanya kazi Chuxx na wenzake. Sehemu ya pili inahusu CELEB, ambapo mtunzi anatupa tawasifu ya msanii wa mziki msichana Phy Ngetich Sehemu ya tatu inahusu Malkia sehemu ya pwani kuhusiana na suala la kutoa maoni kuhusu bajeti inahusu maslahi ya vijana.Sehemu ya nne inahusu Maria Kim tena akiwa katika shamba la kukuza uyoga kama kilimo biashara. Sehemu ya tano ilihusu Charlie Pele akiwa mashambani ambapo ushirikiano wanakijiji unadhihirika katika kuhusisha viongozi wa kisiasa (MCA) katika maisha yao.




Sehemu ya mwisho inahusu DJ Boiye na mandhari ni maeneo ya ofisi ya Mheshimiwa Mwakilishi Wadi (kuna kibao cha MCA's office) kama inavyodhihirika katika ukurasa

wa 30 wa chapta hii ya  93Mandhari hapa yakiwa ni ya kubuni, matukio yanatokea nje ya ofisi za MCA ambapo yaonekana akizungumza na kundi la vijana. Mitindo ya nywele ya baadhi vijana inadhihirisha usasa. Wanazungumzia kuhusu mradi wa 'Talent Center' ambao MCA amewaahidi utajengwa. MCA pia anawaahidi kuwa yuko tayari kuwahudumia kila wakati na wanaweza kufika kwake wakati wowote. Maudhui yanazoendelezwa hapa ni ya u.ongozi wa kisiasa. Ahadi za maendeleo ni sifa mojawapo ya wanansiasa .Hali hii ya mandhari tofauti tofauti katika toleo moja ni sifa bainifu inajitokeza katika matoleo yote. Baadhi ya mandhari ni ya kubuni lakini mengine ni halisi.   Mandhari yaliopo katika  Kielelezo cha 2: CHAPTA 57 ukurasa wa 8  ni mfano wa mandhari halisi.  Kwani picha iliopo inahusu sehemu halisi ya Kibera kule Nairobi.




**Kielelezo cha 9 Chapta 57 ukurasa wa 8**

Mhusika picha ni mhusika halisi. Wanayoyazungumzia kuhisu tatizo la taka  hapo Kibera yanaonekana kutokana na rundo la takataka zilizopo. Makazi niyamababnda kama yanavyo dhihirika katika picha.

3. **Mtindo**

Mtindo ni namna ya upekee ambayo mwandishi anaitumia kuwasilisha kazi yake tofauti na waandishi wengine. Mtindo wa mwandishi fulani unaweza kutambulika kwa kuchunguza mambo yafuatayo; uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, uteuzi wa mandhari, miundo ya sentensi, urefu au ufupi wa aya, majina anyowapa wahusika wake nk. Mtunzi wa *Shujaaz* anatumia mtindo wa kuchanganya mambo tofauti katika kazi moja; amechanganya tanzu za fasihi simulizi na zile za fasihi andishi pale anapotumia 'mchongoano' na 'ujinga ni' kama ilivyo katika uk. 32 wa Chapta 93, amechanganya matumizi ya sanaa ya picha za kuchorwa (katuni) na ile ya picha za watu halisi(fotonovela) mfano katika CHAPTA, 57, 58, 68, 78, 88, 93, 98, 102 na 109 amechanganya mtindo wa katuni na wa uandishi wa tawasifu. Amehusisha maoni ya wahusika na yale ya wasomaji wanaotuma maoni kupitia numbari ya jumbe fupi za simu 20308 mwishoni mwa kila sehemu. Amechanganya matumizi ya marangi tofauti tofauti za kuvutia pia kama mtindo wa uwasilishaji wa ujumbe katika picha zake anaa nyingine iliyotumika katika matoleo yote. Hii ndiyo sifa bainifu ya kimtindo ya *Shujaaz*. Yaani Shujaaz inakuza dhana ya upatanisho na ushirikiana wa kitaaluma, sanaa tofauti na kwa kuhusisha tanzu tofauti za fasihi andishi na simulizi katika kazi moja.

4. **Muundo**

Wamitila (2008) anaeleza kuwa muundo ni umbo na mpatano, mshikamano na uhusi visehemu tofauti vya kazi inayohusika. Anaeleza kuwa muundo huundwa na elementi kadhaa: mtiririko wa matukio (visa), sura au matukio, wahusika, na mandhari. Kutokana na mtiririko wa visa na matukio katika kazi ya fasihi tunapata aina kuu mbili za muundo ambazo ni: Muundo wa moja kwa moja (msago) na muundo rejeshi (kioo)..


Katika *Shujaaz* muundo unaotumiwa ni wa moja kwa moja huku kukiwa na sehemu kadha fupi; sehemu tano au sita ambazo huwa fupi na zinazohusu wahusika tofauti. na kurasa zake kwa ujumla huwa kurasa 32 au 24. Katika *Shujaaz* msuko huwa ni wa moja kwa moja na tena matukio huwa mafupi. Kwa mfano katika CHAPTA 93, sehemu ya MARIA KIM, uk wa 2-7, ni tukio la kurasa tano tu. Ikizingatiwa kuwa hii

si riwaya ambapo maneno huandikwa kwa lugha ya nathari au tamthilia, idadi ya maneno yaliyo katika vibofu vya maneno ni chache. Hivi kwamba wanenaji husema bila kueleza waliyonayo moja kwa moja kwa njia sahili.


Matukio si mengi katika kila sehemu kwa mfano katika sehemu hii ya MARIA KIM, tukio linatukia katika maeneo ya kazi(hotelini) na wafanyikazi wa hoteli wanajadiliana kuhusu matumizi ya mipira ya kuoana kimwili/ kujamiana. Sehemu hii ni mfano unaobainisha muundo wa kueleza matukio moja kwa moja. Kwani wasichana waliopo wakiongozwa na DOREEN inabainika hubeba mipira hii kwenye mikoba yao kila waendapo jambo ambali mhusika CHUXX anadai kuwa halifai na kuwa utumizi wa mipira hii unahatari ya kusababisha ugumba na ugonjwa wa saratani kwa watumizi wake. Kutokana na CHUXX kumuudhi DOREEN kwa kumuuliza mbona anabeba ‘CD’ kila wakati eti kama yeye alikuwa choo cha umma “Public Toilet’, CHUXX anafutua kazi siku hiyo hiyo aliyoajiriwa kwa kuonekana kutokuwa mwadilifu. Tukio linaishia kwa MARIA KIM kuelezea DOREEN umuhimu wa yeye DOREEN na mpenzi wake MOSE, kutembelea kituo cha huduma ya ushauri na maelekezo kwa vijana cha FUTURE FAB, ili MOSE wache kuogopa kutumia mipira ya kuonana kimwili. Katika msuko huu, wahusika huwa hawaelezwi kwa kina, wala kwa mapana, na badala yake, vitendo halisi vya wahusika, yakiwepo maneno wanayoyasema wao ndio yanayojenga kisa chenyewe.

Sifa bainifu ya *Shujaaz* kimuundo ni kuwa haina urefu maalum kwani kuna matoleo yenye kurasa 32 na mengine 24, haina idadi sawa za sehemu za ndani, kila toleo lina sehemu tofauti ambazo hazihusiani kimatukio na kiujumbe, hakuna mpangilio maalum wa yaliyomo hivi kwamba hakuna sehemu maalum ya kutangulia au ya kumalizia.

Katika matoleo maalum; ‘SPECIAL EDITION 03/03’ ukurasa ya 8-9 muundo uliotumika hapa ni wa kimaelezo ambapo kuna maswali na majibu kuhusiana na pendekezo la katiba.




**Kielelezo cha 10 Special Edition03/03 uk 8 na 9**




**Kielelezo cha 11 Chapta 27 ukurasa wa 18**


Katika matoleo yote muundo wa kidayalojia umetumika ambapo wahusika wanazunguza kwa kupishana zamu kama ilivyo katika tamthilia ila hapa maneno yamefungiwa katika vibofu. Maneno yaliyofungiwa katika vipofu yote huwa yameandikwa kwa herufi kubwa . Kauli za wahusika zikiwa fupi na za kupisha zamu.

5. **Muktadha**

Muktadha ni dhana inayorejelea mazingira yanayoendana na tendo au jambo linalofanyika. Ambapo kila jambo linalosemwa linadhibitiwa na mambo mengineyo kama wakati, wahusika wengine na mandhari. Muktadha huhusisha kurejelea matukio yaliyotokea kabla yale hayajasemwa, hasa yale yaliyosababisha maneno yaliyodondolewa kusemwa au matukio yanyayotokea kutokea namna yanavyotokea.

Matukio katika *Shujaaz* ni mafupi mafupi kila sehemu ikiwa na muktadha wake tofauti bila ya sehemu zozote kuathiriana kwa vyovyote vile. Katika *Shujaaz* hakuna matukio ya sehemu tofauti ambayo yanarejeleana kila sehemu na tukio lake lina muktadha wake. Kwa mfano katika Chapta 68 sehemu ya kwanza ambayo ni ya MALKIA (uk2-7) inatukia sehemu ya pwani na unahusu kumsaidia rafiki (KUOKOLEA BESHTE) na

baadhi ya wahuska wake ni MALKIA, ESTHER, MICH na DAN. Matukio yanatokea kwenye salon, nyumbani kwa ESTHER na mtaani. Sehemu ya pili ya Chapta 68, ukurara 8-9, inahusu 'SHUJAA WA MTAA' ambapo tunatapa mhusika Paul Kuhuha aka Protisa anatupatia tawasifu yake. Hapa picha halisi zimetumika zikionyesha mandhari halisi. Maudhui yakihusu uwajibikaji katika kujikimu kimaisha kupitia bishara ya upigaji picha . Sehemu ya tatu ukurasa 10-15, inahusu 'HUSTLA' ambapo husika CHARLIE PELE anamhoji mhusika picha halisi Joseph Barasa katika mandhari halisi shambani mwake Joseph kule Narok. Matukio hapa yakihusu kilimo biashara. Sehemu ya nne ni sehemu ya 'CELEB' ambayo inahusu msanii halisi mashuhuri wa uimbaji VICTORIA KIMANI akizungumza na mhusika DJ BOYIE. Kuna picha halisi ya Victoria na pia michoro wa mhusika BOYIE na VICTORIA. Matukio yanahusu maelezo kuhusu maisha ya VICTORIA. Sehemu ya tano ni yake MARIA KIM na inahusu 'DRAMA YA MABESTE WANGU' . Yaani vituko vya marafikie MARIA. Baadhi ya wahuska hapa wakiwa ni MARIA, JOHN, KA-DUVET na PATRICIA. Matukio yakuhusu maswala ya changamoto za mapenzi. Matukio yanatokea nyumabi kwa MARIA, hotelini na katika chumba cha burudani.




**Kielelezo cha 12 CHAPTA 27, uk 31**

6. **Matumizi ya Lugha**

Matumizi ya lugha yanahusu mambo mawili makuu, nayo ni, Mbinu za sanaa/mbinu za lugha na Mbinu za mwandishi/mbinu za kimtindo. Mbinu za saana/mbinu za lugha zikiwa ni fani za lugha ambazo tayari huwepo katika lugha na msanii huzitumia kama vile matumizi ya tamathali za usemi ama mbinu za mwandishi ni mbinu za kibunifu anazotumia mtunzi kupamba mawasilisho yake.Mtunzi wa *Shujaaz* ametumia lugha kwa namna sahili mno hivi kwamba mbali na kuwepo kwa 'Mchongowano' na 'Ujinga ni' ambazo ni mbinu za mwandishi matumizi ya tamathali za usemi yameadimika kwani lugha iliyotumiwa pia ni sahili.

Sifa bainifu hapa ikiwa usahili wa lugha katika *Shujaaz* kiasi cha kutotumika kwa tamathali za usemi ambazo kwa kawaida hupatikana kwa wingi katika tungo nyinginezo za fasihi. Mtunzi ametumia Sheng kwa wingi kiasi cha kuumpa msomaji kamusi ya Sheng' 'SHENG DICTIONARY' kama ilivyo katika CHAPTA 27, uk 31 na CHAPTA 93, uk 32. Uwepo wa kamusi ya sheng katika matoleo ya *Shujaaz* ni sifa zake bainifu ya mbinu za Sanaa. 'SHENG DICTIONARY' inajitokeza katika baadhi ya matoleo ya hapo awali yaliyokuwa na sehemu za kamusi ya Sheng kama ilivyo katika CHAPTA 27 na 33. Katika matoleo mengi kuna sehemu ya 'Mchonguano' na 'Ujinga ni?' Kwa mfano katika CHAPTA 33 uk 29, CHAPTA93 uk 32,

7. **Usuli**

Usuli unahusu maisha ya mwandishi na namna tajriba yake ya hapo awali huaathiri kazi husika. Usuli ni chanzo, msingi au chimbuko la kazi za kifasihi. Kunao usuli unaomhusu mwandishi na ule unaohusu ulimwengu wa hadithi. Usuli wa mwandishi huwa ni jumla ya mambo yaliyompata (yaliyomwathiri) mwandishi katika maisha yake utotoni mwake hadi wakati wa kuandika kazi za kifasihi. Hii ni kusema kuwa mambo yaliyomwathiri mwandishi (mazuri au mabaya) pia huathiri namna anavyoandika. Usuli katika ulimwengu wa hadithi unapochunguza wahusika wa kifasihi kuhusu maingiliano yao, mawazo yao, na sifa nyinginezo tunaona kuwa vyote hivyo huathiriwa na mazingira (mandhari) yao kama wahusika.

*Shujaaz* imejengeka katika usuli wa ulimwengu wa hadithi na wahusika wake huathiriana katika maigiliano yao na mazingira yao kama wahusika. Dhana ya upatanisho na mbadilishano wa mawazo mingoni mwa wahusika kunachangia sana katika kujengeka kwa usuli katika *Shujaaz*. Mhusika mmoja katika toleo moja aweza kujitokeza mara mbili katika sehemu tofauti akiwa na sifa tofauti na akiathiriana na wahusika katika hali tofauti. Kwa mfano katika CHAPTA 98, Mhusika Maria Kim anatokea mara tatu katika sehemu tatu tofauti; sehemu ya kwanza ni kuanzia uk 10-15 ambapo Maria ni mwanafunzi katika Jongo High School, matukio na tabia zake na wenzake ni za wanafunzi. Mazingira yale ya shule yana lazimu matukio kuwa ya shule. Tukio likihusu changamoto za mapenzi na kuandikiana barua za mapenzi baina ya wanafunzi shuleni na hatari zake. Katika sehemu ya pili uk 23-25, Maria Kim yupo katika kile wakipendacho vijana kuingia katika mtandao wa kijamii wa 'facebook' anapoangalia yaliopo katika sehemu ya 'Love and Hustle' ambapo vijana mbalimbali wametuma jumbe kujihusu. Anatoa changamoto za ni nani aliye mfano bora wa kuigwa na vijana kutokana na kuadilika na kufaulu kwake. Katika sehemu ya tatu uk 26-31, Maria Kim yupo mtaani na tukio linahusu mhusika Chuxx na warembo wake ambapo Chuxx anajihusisha na warembo wengi kutokana na kuwa na pesa ambapo watano kati yao wanapata ujauzito jambo linalomtia Chuxx matatani. Maria Kim hapa anajitokeza kama mshauri na mwelekezi kwa Tabby mmoja wa wapenzi wa Chuxx na anamwekeleza kwenye kituo kinachotoa huduza za bure za uzazi cha T-Safe.

Katika mfano huu usuli wa matukio unaathiriwa na mazingira na mahusioano baina ya wahusika na hali hii ipo katika matukio yote ya *Shujaaz* kama sifa yake bainifu. Kwamba Mhusika aweza kujitokeza katika sehemu tofauti katika toleo lile lile moja lakini adhihirishe sifa tofauti.

**b) Maudhui**

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) Maudhui ni maswala mbalimbali yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya kifasihi. Maudhui pia, ni yaliyomo au jumla ya maswala yanayoibuka katika kazi za kifasihi (riwaya, tamthilia, hadithi fupi au ushairi). Vipengele vinavyohusiana na maudhui ni: dhamira, ujumbe, falsafa, maadili na migogoro. Kupitia vipengele hivi

pamoja na uwepo wa dhana ya upatanisho na ushirikiano na mwingiliano wa sanaa na taauma mbalimbali sifa bainifu za *Shujaaz* zinadhihirika ifuatavyo:

1. **Dhamira**

Wamitila (2002), dhamira kuu ni kiini cha kazi ya fasihi, ni wazo kuu, ni jambo linalomsukuma msanii kuandika kazi yake ili aweze kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Dhamira ndogondogo, ni mawazo madogomadogo ambayo hujenga dhamira kuu. Dhamira ni wazo kuu au lengo kuu ambalo lilimsababisha mwandishi kuandika kazi yake ya kifasihi. Kulingana Mwenda (2004), dhamira ni neno linalochukuana na ile azma, lile lengo au kusudi la mtunzi katika kuitunga kazi yake. Hii ni kwa sababu, aghalabu kila mtunzi huwa amesukumwa na jambo fulani (liwe zito au liwe lepesi) katika utunzi wake. Kama tulivyotangulia kutaja, hakuna mtunzi anayeweza kutunga katika au kutokana na ombwe. Mwandishi, hata anapoandika tungo za kubuni, huwa amesukumwa na jambo au mambo fulani aliyowahi kushuhudia katika fikra zake au katika hali halisi maishani; hata hizi fikra hujengwa na mambo fulani ya tajiriba halisi katika maisha halisi.

Watayarishaji wa *Shujaaz* bila shaka wana dhamira zao zilizowasukuma hadi kuandika matoleo yote waliyoyatoa na wanayozidi kutoa. Katika sehemu hii ni muhimu kubainisha sifa bainifu za dhamira zinazojitokeza katika *Shujaaz.* Kwa mfano baadhi ya dhamira katika CHAPTA 27 ni:

i) Mwandishi ana dhamiria kuhamasisha vijana dhidi ya uovu na madhara ya kuuza kura zao wakati wa uchaguzi

ii) Mwandishi ana dhamiria kuonya vijana dhidi ya kuwachagua viongozi wasiowajibika kutimiza ahadi walizozitoa wakati wa kampeni.

iii) Katika uk 16-17 mwandishi alidhamiria kuonyesha maoni ya wasomaji kuhusu maswala ambayo yanawasilishwa na *Shujaaz.*

iv) Mwandishi vile vile anadhamiria kuonyesha vijana hasaa wasichana kuwa wanauwezo wa kuibadilisha jamii kwa kupinga na kupiga vita ufisadi hata kama wametoka katika jamii masikini hasa za maeneo ya mabandani au ‘Ghetto’.

v) Mwandishi pia alidhamiria kuonyesh changamoto zinazowapata wasichana wanapopata mimba na kujifungua wangali shuleni. Analenga kuwaonyesha

kuwa bado wanaweza kufanikiwa maishani wakirudi shule baada ya kujifungua na kutimiza ndoto zao

vi) Mwandishi anadhamiria kuhimiza wasomaji wake umuhimu wa kununua mbegu ambazo zimepitishwa na idara husika ikiwa wangetaka kupata mazao mengi na bora kuliko kununua mbegu ambazo hazijaidhinishwa.

vii) Mwandishi pia alidhamiria kukuza lugha ya ‘Sheng’ kupitia ‘MCHONGOWANO’, ‘UJINGA NI …’ na pia kupitia ‘SHENG DICTIONARY’

Dhamira katika toleo la SPECIAL EDITION zikiwa ni:

i) Mwandishi anaonya vijana dhidi ya kujiunga ma makundi ya kijambazi kwani mwisho wake ni kutiwa mbaroni na kufungwa.

ii) Mwandishi anahamasisha umuhimu wa kukuza ufahamu wa vijana kuhusu uchaguzi na namna ya kukubali matokeo wowote ule mfano ukiwa uchaguzi wa viranja mashuleni. Mtunzi anapendekeza kuwa uchaguzi wa vingozi wa wanafunzi shuleni ufanike kupitia kuchaguliwa na wanafunzi wenzao kwa kuwapigia kura.

iii) Mwandishi vilevile anawahimiza vijana kusoma katiba ya nchi ili waelewe haki zao na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa

iv) Mwandishi pia anawaonya vijana dhidi ya kuchochewa na viongozi wabaya wachukie na wapigane kwa misingi ya kikabila kwani havijengi nchi bali si kuijenga.

Dhamira katika toleo la CHAPTA 109 ni:

i) Kuwahumiza vijana kujipanga na kuanzisha biashara yaani ‘HUSTLE FITI’ kuliko kutarajia tu kuandikwa kazi za ofisi.

ii) Mwandishi anadhamiria kuwafahamisha vijana hasa wanafunzi katika shule za upili kuhusu madhara ya kujihusisha kimapenzi wangali shuleni kwani kufanya hivi kutaathiri masomo yao na kusababisha kuanguka katika mitihani.

iii) Mwandishi anawaonya wanafunzi dhidi ya kutegemea mitihani bandia wanapojiandaa kwa mtihani kwani huenda wanayodhania ni mtihani wa kweli unaweza kuwa kinyume na hapo wakaanguka mitihani yao.

iv) Mwadishi anawahimiza vijana kuhusu kujichunga na kujitunza wanapojiingiza katika mahusiano ya kimapenzi kwa kutembelea kituo cha T-SAFE.

v) Mwandishi analenga vilevile kuwaonya vijana wavulana ambao wana mazoea ya kuwapachika wasichana mimba na kuwaruka kuwa ni muhimu wachukue jukumu la kuwalea Watoto wao Pamoja wa kuwakidhia mahitaji yao na mama wa watoto hao.

vi) Kupitia mahojiano ya Dr. Ofweneke (mwigizaji mashuhuri wa vichekesho nchini Kenya) mwandishi anawahimiza vijana wasilalie talanta zao kwani zinaweza kuwasaidia kujiinua maishani na kuwa watu mashuhuri

Kutokana na mifano hii sifa bainifu za dhamira katika matoleo haya ya *Shujaaz* ni:

i. Mwandishi anawalenga vijana wa shuleni na waliomaliza shule.
ii. Mwandishi analenga changamoto zinazokumba vijana katika maisha; mapenzi, malezi, mimba za mapema, umaskini, n.k
iii. Mwandishi analenga kuonyesha nafasi ya vijana katika jamii katika Nyanja zote; kijamii, kiuchumi na kisiasa

**2. Ujumbe**

Ujumbe Mlaga (2017) Ujumbe ni funzo au fundisho linalopatikana katika kazi ya fasihi. Ujumbe pia hugawanyika katika aina mbili ambazo ni; ujumbe mkuu na jumbe zinazoendana na dhamira ndogo. Ujumbe mkuu hutokana na dhamira kuu na pia jumbe nyingine hutokana na dhamira zile ndogondogo. Kwa hiyo, ujumbe ni funzo na maadili yaliyokusudiwa na mtunzi yawafikie wahusika aliowalenga kufikisha kazi yake ya fasihi. Ujumbe ni taarifa aipatayo msomaji asomapo kazi za kifasihi.

Kwa mfano katika *Shujaaz* kila toleo linawasilisha jumbe tofauti katika kila sehemu iliyopo kila sehemu ikiwa na ujumbe wake. Katika CHAPTA 58: sehemu ya kwanza ya DJ Boiye uk 2-9 ujumbe unahusu changamoto zinazokumba vijana katika juhudi za kukuza talanta zao na kuzitumia kujiinua kiuchumi na kimaisha. Katika sehemu ya pili ya CELEB yake DJ boiye, uk8-9, kuhusu Bi. Liz Marami ambaye ni nahodha wa kwanza mwanamke nchini Kenya. Ujumbe hapa ni kuwa vijana wakike wahamasike kuwa wanaweza fanya kazi yoyote watakayo mradi wawe na azma kwani hakuna kazi

zilizotengewa wanaume pekee. Kisha kuna sehemu ya Malkia, uk 10-15, kuhusu mahusiano ya vijana kimapenzi na chamgamoto za matumizi ya mipira ya kuonana kimwili na namna vijana wengi hawana ufahamu kamili wa ufaafu wa mipira hiyo na kwa hivyo kuwa na mtazamo hasi wa wavulana kuchukulia kuwa msichana akiwa na mipira hii yeye ni kiruka njia. Sehemu inayofuata uk 16-17, inahusu JITUME UPENYE, ambayo kuna tawasifu ya kijana 'Holy Boy' ambaye ni mpiga picha mashuhuri kule Meru. Ujumbe hapa nikuwa ilikufaulu katika kila jambo lazima vijana wajitume. Mwisho kuna sehemu ya Maria Kim, uk 18-23, inahusu changamoto za wapenzi hasa ikiwa mmoja katika mahusiano hayo hataki kutumia kinga wakati wa ngono. Ujumbe hapa ukiwa vijana wanafaa kujadiliana na kukubaliana kuhusu swala salama la kuonana kimwili ili uhusiano wao uweze kudumu.

Sifa bainifu katika jumbe katika *Shujaaz* nikuwa Jumbe zote zinahusu vijana na chamgamoto zao za kimaisha. Fasihi nyingine zingehusu jamii nzima kwa jumla lakini *Shujaaz* imeejikita kwa kundu la vijana katika jamii.

3. **Falsafa**

Wamitila (2008) anaeleza falsafa kama dhana inayotumiwa kuelezea mwelekeo wa kimawazo ambao unadhihirika katika kazi ya kifasihi. Mwelekeo huu unajengwa kwenye dhana ya urudiaji. Mtaalamu huu anaeleza kwamba kulingana na utohozi wa neno hili kutoka Kiarabu na Kilatini, Falsafa huweza kuelezwa kama busara iliyo fikiwa baada ya mtu au watu kutafakari kwa kina kuhusu jambo lolote la kiulimwengu ni busara itokanayo na harakati za kimawazo.

Kwa mujibu wa mifano iliyotolea katika sehemu ya fani, sifa bainifu kuhusiana na falsafa katika *Shujaaz* ni kuwa, vijana wana nafasi muhimu sana katika maendeleo ya jamii katika sekta za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Haya yanatokana na vile ambavyo wahusika karibu wote aliowatumia mtunzi ni vijana katika matoleo yote. Falsafa yake ni kwamba vijana wanahitaji kupewa nafasi ya kujieleza, kusidiwa kuweza kujitatulia changamoto za kisiasa, kiuchumi na kijamii zinazo wakumba. Haya yatawezekana kwa kupewa ushauri na maelekezo, kukubaliwa wajieleze, kushirikishwa katika kila jambo katika jamii, kupewa nafasi za uongozi, na kujumuishwa katika harakati zote za jamii za kisiasa,

kiuchumi na kijamii. Mtunzi wa *Shujaaz* anashikilia kuwa japo vijana wananapitia changamoto nyingi katika maisha yao wao wenyewe wananweza kusaidiana kujiopoa katika changamoto hizi. Anaonelea kuwa pasipo na elimu ya stadi ya maisha hasa kuhusiana na maswala ya ngono vijana wengi watajipata matatani ya ndoa za mapema, uja uzito kabla ya ndoa, uavyaji mimba na hatari zake na masaibu mengine ya kuwaathiri kiafya na kiuchumi.

**4. Migororo**

Wamitila (2014), Suala kuu linaloshughulikiwa au linalounda migogoro inayaotawala matukio linahusu vijana. Matoleo yote ya *Shujaaz* yanahusu changamoto wanazopitia vijana maishani mwao. Migogoro wa mtu na nafsi yake, mtu na jamii, mtu na mazingira yake, mtu na asili yake, mtu na jaala yake, mtu na hali ya kiuchumi, mtu na siasa za jamii yake, mtu na utamaduni wa jamii yake, mtu na mpenziwe n.k. Katika CHAPTA 40, uk 5-8, DJ BOIYE na rafikiye wanadhihirisha changamoto ambazo vijana wanapambana nazo katika juhudi za kujijenga kiuchumi. Uk 12-17, ukionyesha mgogoro baina ya wanajamii na mazingira kutokana na suala la ukosefu wa maji ya kutosha kwa matumizi ya nyumbani na shambani.

Kwa kuangalia mifano iliyotolewa kutoka matoleo ya *Shujaaz* katika sehemu za maudhui zilizo hapa juu inasibu kuwa pakubwa sifa bainifu kuhusu migogoro iliyopo katika *Shujaaz* ni migororo ya kimapenzi, kiuchumi na kisiasa kati ya vijana wapenzi. Hata migogoro iliyopo ya mt una nafsi yake inahusu maswala ya mahusiano ya kimapenzi, changamoto zake na athari za matokeo yake.

**5. Uadilishaji**

Fasihi ya watoto na vijana huwa na maudhui au dhamira ambazo zinakusudia kufundisha au kuwaadilisha vijana. Dhamira katika kazi za fasihi ya vijana huelekezwa katika kuwanufaisha ama kuwajenga vijana kulingana na malengo ama maadili ya jamii zao. Kwa hivyo, dhamira zinazochukuana na mahitaji ya vijana katika jamii ndizo hukuzwa katika kazi hizo. Kazi za vijana, kama ilivyo katika *Shujaaz,* hutawaliwa na changamoto na matumaini ya vijana katika kujisaka na kujitambua, mapenzi na changamoto zake, mahitaji ya pesa na changamoto za kujiinua kiuchumi, uongozi na

nafasi ya vijana katika siasa za jamii yao, matarajia ya jamii kulingana na ada za kitamaduni na athari za ukengeushi, changamoto za teknolojia n.k. Katika CHAPTA 102, uk 2-7 suala la uaminifu

linashughulikiwa ambapo vijana wanahimizwa kuwa waaminifu wanaposhilikiana na wenzao kujikuza kiuchumi. Wasiwatapeli au kuwaibia wenzao.

Katika sehemu ya MALKIA, uk 12-17, mwandishi anadhamiria kuonyesha umuhimu wa kuweka akiba kutoka chochote mtu apatacho kwani akiba hiyo itafaa baadaye. Kupitia mhuskia MALKIA, vijana wanaadilishwa kuwa lazima waweze kutafuta njia za kujitegema kwa mahitaji yao kwa kuweka akiba ya pesa wanazopewa za matumizi. Suala la kimsingi linajadiliwa katika *Shujaaz* ni kuwataka vijana wawajibike katika nyanja mbalimbali za maisha yao. Kupitia mbinu ya uigizaji, wahusika mbalimbali wanasawiriwa kwa kuonyesha jinsi walivyowajibika au la, katika matendo yao.

### 4.6 Hitimisho

*Shujaaz* kama kazi ya fasihi imedhihirisha sifa kadha bainifu zikiwemo; kwamba ni fasihi inayotumia lugha mseto ya Kiswahili kilichochanganywa na kiingereza na Sheng, sifa ya wahusika wake wote wakuu kuwa vijana na wasaidizi pia, sifa ya kuchangnya Sanaa tofauti na tanzu tofauti za fasihi katika kazi moja kati ya sifa nyinginezo. Yaelekea pia hadhira yake pia ni vijana kwa hivyo kimsingi ni haki kutoa kauli kuwa *Shujaaz* ni fasihi ya vijana. Kutokana na vigezo hivi vya sifa za fasihi ni bayana kuwa *Shujaaz* imeafiki sifa hizo na bila shaka ni kazi ya fasihi inayowakilisha sifa mpya ya fasihi kama inavyopendekezwa na nadharia iliyoongoza utafiti huu.

# SURA YA TANO

# UHAKIKI WA *SHUJAAZ* KWA KUTUMIA VIGEZO VYA UHAKIKI WA FASIHI YA KISWAHILI

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inajishughulisha na uhakiki wa *Shujaaz* kwa kutumia vigezo vya uhakiki wa kazi ya fasihi ya Kiswahili. Ilikufanikisha haya vipengele vya maudhui na fani katika *Shujaaz* vinafafanuliwa kwa mifano kutoka matoleo 13 ya *Shujaaz* yaliyoteuliwa ambayo ni: matoleo maalum- SPECIAL EDITION 01/3 na 03/03, CHAPTA 27, 33, 40, 57, 68, 78, 88, 93, 98, 102 na 109. Uhakiki uliongozwa na nadharia ya metausasa ili kutimiza lengo la pili la utafiti huu; kuihakiki *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili kwa kutumia vigezo vya uhakiki wa kazi za fasihi.

## 5.2 Uhakiki wa *Shujaaz*

Uhakiki wa *Shujaaz* ni kazi au kitendo cha kuitafakari, kuichambua na kuifafanua kazi ya *Shujaaz* ili kuweka bayana fani na maudhui yaliomo ndani yake. Kulingana na Wamitila (2008), fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa au huacha hisia fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani. Hivyo basi fasihi ina beba mambo makuu matatu ambayo ni: Lugha ya kisana(lugha isiyo ya kawaida), kuelezea tajriba ya maisha ya jamii husika na kutumia ubunifu/ubunilizi. Mhakiki au mchambuzi wa kazi ya fasihi hushughulikia vipengele vya maudhui na fani.

## 5.3 Uchambuzi wa Maudhui katika *Shujaaz*

Maudhui ndio kipengele kikuu zaidi katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Kipengele hiki hujumuisha: dhamira, ujumbe/maadili, mitazamo, migogoro, msimamo na falsafa na itikadi. Vipengele hivi ndivyo vigezo vilivyozingatiwa katika uchambuzi au uhakiki wa *Shujaaz* ili kuweza kutathamini, kueleza kuainisha na kutoa maoni kuhusu kazi hii ya *Shujaaz*. Hata hivyo, Uchambuzi huu uliongozwa na kaida za uhakiki waa kazi za fasihi na nadharia ya utafiti huu.

i) **Dhamira.**

Mwandishi wa *Shujaaz* ana yale yaliyomsukuma kutunga kazi hii. Akawa ana nia au jambo ambalo alikusudia kuliwasilisha au kulitajia jamii ilishughulikie. Kwa mujibu wa Wamitila (2008) dhamira ya kazi ya kifasihi mbali na kuhusu ujumbe, adili au maadili fulani, huweza pia kuwa mvuto au mwitikio wa kiujumi au umbuji wa mazingira au kitu fulani. Dhamira

huhusiana na wahusika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa wahusika wanaweza kuangaliwa kama nyenzo muhimu na kuu wa kuendelezaji dhamira. Mtunzi wa *Shujaaz* ana dhamira zake ambazo zinajidhihirisha kupitia namna alivyosuka matukio na maingiliano wa wahusika wake. Katika *Shujaaz* baadhi ya dhamira kuu zilizopo ni:

- **Nafasi ya vijana katika uongozi na siasa na uchaguzi wa viongozi**

  Mwandishi wa *Shujaaz* anadhamiria kuonyesha kuwa vijana wana nafasi katika uongozi na siasa za jamii yao. Ili kudhibitisha haya ni vyema kutoa mifano bayana. Katika, SPECIAL EDITION 01/03 na 03/03 dhamira kuu ni kuonya vijana dhidi ya uongozi au viongozi wabaya kwani wanaweza kuvuruga amani katika jamii. Katika sehemu ya BOIYE, mwandishi analenga kuhamasisha wasomaji wake hasaa vijana wasome pendekezo la katiba ya nchi. Wakifanya hivi wataweza kuelewa namna inavyo waathiri, wajue haki zao, wajue kuhusu kesho yao na hivyo kuweza kufanaya uamuzi ikiwa katiba hii inafaa au haifai. Mwandishi pia anawaonya vijana kutojihusisha na vikundi visivyo halali mtaani. Anaonya kuwa, vikundi hivi vyaweza kuwa na ushawishi wa kujihusisha na maovu yanayoweza kuvuruga amani katika jamii. Jambo hili linaweza kuwanyima ujasiri wa kuwa na msimamo thabiti na wakibinafsi wa kujiongoza maishani. Pia wanaweza kushindwa kufanya maamuzi ya busara hasa katika upigaji kura. Anashutumu viongozi ambao hutumia vikundi vya vijana kwa kuwapa pesa na ahadi za uongo ili kutatiza amani na kuogofesha jamii. Kwa hivyo mwandishi anadhamiria kuwa vijana kama tegemeo la jamii wanatakiwa kuchukua nafasfi za uongozi dhidi ya vingozi waliopo wanaoendeleza chuki, utengano na ukabila katika jamii. Vijana wasimame na haki na ukweli uliopo katika mwongozo wa katiba ya nchi. Vijana wawaondoe viongozi wabaya katika nyadhifa za uongozi kwa kuizindua jamii kuhusiana na njama za viongozi hawa dhalimu. Vijana pia wawanie nafasi za uongozi kwa wakifanya hivyo watakuwa na nafasi bora ya kutatua changamoto zinazoikumba jamii kama wanavyozielewa.

  Katika sehemu ya MALKIA katika SPECIAL EDITION 01/03, mwandishi anadhamiria kuonyesha umuhimu wa kuwako uongozi bora kutoka kwa baraza la viranja shuleni ili kudumisha amani miongoni mwa wanafunzi. Viongozi wa mabaraza haya wanaonywa kuwa wakishindwa na kazi wako hatarini ya kubanduliwa.

Katika CHAPTA 33, kila sehemu ina dhamira yake tofauti. Kwa mfano, sehemu ya BOIYE, dhamiria kuwahamasisha vijana wasanii maarufu na viongozi kuwa katika mstari wa mbele kuwahimiza vijana kuchukua kura na kushiriki katika upigaji kura kwani hapo ndipo watawachagua viongozi vijana wafaao kuwaongoza. Katika CHAPTA 33, sehemu ya MARIA PIA katika uk 18-19 anawahimiza vijana kuwachagua vijana wenye nidhamu kuingia katika uongozi wa serikali gatuzi ili maslahi ya vijana yaweze kushughulikiwa.

Katika toleo hili hili sehemu ya CHARLIE PELE, mwandishi anaonya wale watu amabo wanachochea chuki yaani 'hate Speech' niongoni mwa wanajamii kuwa wanaweza kuchukuliwa hatua za kisheria au hata kuchukuliwa hatua na wanajamii wenyewe. Katika sehemu ya MARIA KIM ya toleo hili, mwandishi anaonya vijana dhidi ya kuwaamini viongozi sana. Sababu iliwa baadhi ya viongozi si wakweli na huwa na agenda zao za kibinafsi ambazo ni za kujinufaisha wao wenyewe au hata kuleta chuki kati ya wanajamii. Viongozi hawa huchukua nafasi hii kujinufanisha. Mwandishi anawahimiza wanajamii kwa jumla kuhibitisha madai ya viongozi hasa wakati wa kampeni za uchaguzi ili kuepukana na kupotoshwa kwa ahadi na madai ya uongo.

Katika CHAPTA 27, sehemu ya kwanza ya BOIYE inalenga kuwaonya vijana dhidi ya kuuza kura zao kwani kufanya hivyo nikuuza haki yao na kununua shida kwa kupoteza nasafi ya kuchagua viongozi wafaao kuongoza jamii wao. Vili vile katika sehemu ya MALKIA, mwandishi analenga kuwahamasisha vijana pamoja na wanajamii kuwa ni haki yao kushirirki kwa kutoa maoni kuhusu uundaji wa bajeti ya taifa. Pia wana jukumu la kufuatilia kujua namna pesa za umma zinavyotumika ilikuweza kudhibiti matumizi mabaya ya pesa za umma ili kuepusha kuporomoka kwa uchumi kunakosababishia wananchi hali ngumu ya maisha kiuchumi

Katika CHAPTA 93, uk 14- 15, mwandishi anawafahamisha vijana umuhimu wakuchangia katika mapendekezo ya bajeti katika vikao vya maeneo gatuzi ili maslahi yao yaweze kuwekewa mifuko ya matumizi. Mwandishi anawapatia

mpangilio wa hatua za uundaji wa bajeti nchini Kenya kutoka kwa wizara ya fedha nchini na ni lini kutakuwa na vikao vya utoaji maoni kutoka kwa umma. Katika uk 24-30, mwandishi anahiziza vijana kuhusisha mwakilishai wa wadi waliyemchangua katika kutatua matatizo kama ya usalama katika jamii. Mwandishi anaorodhesha majukumu ya mwakilishi wadi yaani MCA ili vijana wayaelewe ambayo ni: kudumisha uhusiano mzuri kati ya wanajamii katika wadi yake, kupeleka maoni ya wananchi katika bunge la eneo gatuzi, kuhudhuria vikao vya bunge gatuzi na kuhakikisha wananchi wanapata huduma kama inavyotakikana.



**Kielelzo cha 13 kutoka CHAPTA 93 uk 14**




**Kielelezo cha 14 kutoka CHAPTA 88 uk 18**

Katika CHAPTA 88, uk 17-22, vijana wanafahamishwa kuwa wana nafasi ya kukomesha ukosefu wa usalama na maovu mengine katika jamii kwa kuripoti visa kama hivi katika idara ya OMBUDSMAN kama ilivyo katika uk 18 ulionukuliwa hapa juu.

- **Mahusiano ya mapenzi kati ya vijana**

  Mwandishi anadhamiria kuonyesha changamoto zinazo wakumba vijana katika mahusiano yao ya kimapenzi na namna wanavyo kabiliana na changamoto hizo. Katika CHAPTA 57, uk10-15, sehemu ya MARIA KIM, mwandishi analenga kudhihirisha changamoto za vijana mtaani kimahusiano na katika raha zoa. Anaonya vijana daima kuwa waangalifu kwa kujikinga dhidi ya hatari za kungiliana kimapenzi bila kinga na kutahadhari wanapoenda maeneo ya burudani kwani ajali zaweza kutokea na yafaa waweze kuwa salama.

Katika CHAPTA 57, uk26-31, sehemu ya MALKIA, mwandishi anawaonya vijana wanao jihusisha na mapenzi kabla ya ndoa wachukue tahadhari ya kujikinga na wasikize ushauri wanao pewa na marafiki dhidi ya kufanya hivi. Wasichana waepuke kudanganywa kwa urahisi na wananume maarufu na matajiri kwani waweza kuambukuzwa magonjwa au hata kushika mimba nje ya kabla ya ndoa.


Katika CHAPTA 68, uk 2-7 mwandishi anaonya vijana dhidi ya kujihusisha na wapenzi zaidi ya mmoja kwani kufanya hivi kuna hatari yake kiusalama na kiafya. Vile vile katika uk 18 – 23 mwandishi anadhihirisha vituko vya mapenzi kati ya vijana kwa kuangazia aina tofauti za mahusiano kati ya wasichana na marafiki wao wa kiume na jinsi kila mhusika aliopo uhusiano wake ni tofauti na wa mwingine. Mwandishi anataka kuonya vijana kuwa hakuna mahusiano baina ya watu tofauti huwa yanafanani. Mahusinao ya ESTHER na wavulana wawili MICHI na DAN yanampatia changamoto ESTHER. Katika uk 5 ESTHER anakumbushwa yaliyompata SARAH alikuwa na 'Maboy wengi' yaani urafiki na wavulana wengi hadi akapata mimba. Kwa hivyo vijana wanafaa kujifunza kutokana na yaliyowapata wengi ili kujiepusha kufanya makosa yaliyofanywa na wenzao.

Katika CHAPTA 78, uk 10-15, mwandishi analenga kuwaelimisha wavulana kuwa wajue kuwathamini wasichana wanaotumia mbinu za kujikinga kama vile kubeba mipira ya kuonana kimwili wakati wa ngono. Kwani wasichana hawa huwa wanajali maslahi yao na ya wapenzi wao hasaa ikiwa hawajaoana kwani wataepuka kupata magonjwa au kuangukia uja uzito. Katika uk 18-23, mwandishi analenga kuonyesha namna mgogoro juu ya matumizi ya mbinu za kujikinga('CD') yaani matumizi ya mipira yakujamiana miongoni mwa vijana. Mwandishi anaonyesha namna matumizi ya mipira hii yanavyoweza kuathiri mahusiano baina vijana wapendanao kutokana na uvumi unaohusishwa na matumizi ya mipira hii. Kuna wanachukulia kuwa wanaotumia mipira hii huwa si waaminifu na jambo hili kuweza kuweka uhusiano baina yao hatarini ya kuvunjika.

Katika CHAPTA 88, uk 2-7, mwandishi analenga kuonyesha changamoto za kimapenzi ambazo vijana wanapitia wakiwa katika shule za upili. Mwandishi

anaonyesha umuhimu wa wazazi hasa wazazi wakike na mashangazi katika kuwashauri na kuwaelekeza wasichana. Kwa kuchukua jukumu hili wataweza kuwasaidia wasichana kuepikana na hatari za kujihusisha kimapenzi wangali wachanga. Katika uk 9- 14, mwandishi anadhamiria kuonyesha athari ya kungiliana kimapenzi/kujamiana bila kinga kwani huweza kuleta ujauzito usiotakikana na kupelekea msichana kuamua kuava mimba jambo ambalo lisipofanywa na wataalam wa kiafya waliofaulu laweza kusababisha kifo cha msichana husika. Katika uk.16 mwandishi anatoa orodha ya sifa za mke na mume mwema ambazo vijana/ wazulufu wanatakiwa kuzitilia maanani wanapotafuta wachumba.


Aidha, matumizi ya simu kama chombo cha mawasiliano kama ilivyo katika uk 26-31, kuna nafasi yake katika kujenga mahusiano baina ya vijana. Mwandishi anadhihirisha jinsi teknolojia ya simu inavyonogeza mapenzi baina ya vijana.




**Kielelezo cha 15 kutoka CHAPTA 88 katika uk 29**

Katika CHAPTA 93, uk 2-7 mwandishi anawashauri vijana kutafuta ushauri kutoka vituo vya afya kuhusu masuala yanayohusiana na mbinu tofauti za kujikinga wanapo jamiana ili kuzuia mimba zisizotakikana na kujikinga dhidi ya magonjwa ya zinaa na UKIMWI. Vilevile wataweza kupata ushauri na ufahamu dhidi ya kasumba nyingi zinazoenezwa kuwa kutumia mbinu kama ya mipira ya kuonana kimwili inaweza kusababisha ugumba kwa wanaume na saratani miongoni mwa wanoitumia mipira hiyo.

Katika CHAPTA 98 uk. 8 – 9, mwandishi analenga kuonyesha tena namna kasumba za uongo kuhusiana na matumizi ya mipira ya kuona kimwili zilivyochangamoto kwa vijana wapendanao. Hali huwa mbaya hasa ikiwa mmoja katika mahusiana haya amekolezwa kasumba potovu kuhusiana na athari za mipira hii na hataki kuitumia ilhali mwenzake anasisitiza lazima watumie mipira wakati wa kuonana kimwili. Hali hii inaweza kupelekea kuvunjika kwa mapenzi yao na wanahitaji kupata ushauri ufaao katika vituo vinavyo toa hudima za maswala ya uzazi kama FUTURE FAB.



**Kielelezo cha 16 Kutoka Chapta 93 uk 7**

Jambo hili linakuwa changamoto katika mahusiana haya na mwandishi anashauri vijana kama hawa watafute ushauri kabla ya uhusiano wao kuvunjika. Katika uk 10 – 15, mwandishi anaonya vijana kutoingilia maisha ya wapenzi wengine kama kusoma barua zao za mapenzi kwani suala hili linahatari yake ila waheshimu mahusiano ya wengine. Katika uk 26-31, mwandishi anaonya vijana wavulana ambao wakipata pesa kazi yao ni kuponda raha huku wakifanya mapenzi kiholelaholela na wasichana. Wavulana hawa huishia kuwapachika mimba wasichana kadha huku wakiwa hawa yuko tajari kuchukua majukumu ya kuwatunza na kulea watoto hao.

Katika CHAPTA102, uk 10-11, mwandishi anatoa fursa ya maswali na majibu kuhusiana na changamoto za kimapenzi wanazo piatia vijana katika mahusiano yao. Anawahiziza wasinyamaze wanapokubiliana na matatizo yanayowafanya kukosana bali watafute ushauri wa namna ya kusuluhisha matatizo baina yao. Katika uk 26-31, mwandishi analenga kuonyesha namna vijana wanaojihusisha katika mapenzi mapema wanavyoweza kuzua migogoro baina yao na tamaduni za jamii zao. Utamaduni ni sehemu muhimu katika maisha ya mwanajamii yeyote na ni muhimu kila mtu kupitia ada zote za maisha ya jamii husika.

Katika CHAPTA 109, uk 10-12, mwandishi anatahadharisha vijana hasaa wasichana kuwa lazima wawe macho wanapo hudhuria miviga kama vile maombolezi vijijini hasa maombolezi yanayohushisha densi kama vile 'Disco matanga'. Hatari iliyopo hapa ni kuwa wao kushawishika ni rahisi. Vilevile wakati mwingi kungiliana kimapenzi bila kinga kwaweza kutokea na hapo wasiwasi wa kupata mimba na magonjwa kuanza. Uk 13-18, mwandishi vile vile anaonya vijana dhidi ya athari ya wavulana kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja huku wakiwa hawapo tayari kuchukua jukumu la kulea watoto watokanao na tabia yao hii mbaya.

- **Nafasi ya vijana katika kijiinua kiuchumi**

  Mwandishi wa *Shujaaz* anadhamiria kuonyesha namna vijana wanavyoweza kujikuza na kukuza jamii kwa kushiriki katika shughuli za kiuchumi kama vile biashara na kilimo.

Katika CHAPTA 33 sehemu ya katikati ya toleo hili ni sehemu ya Shujaa wa mwezi yaani 'SHUJAA OF THE MONTH' Ilio na maoni ya wasomaji wa Shujaaz ambao wanaeleza kuhusu miradi ya kujiinua kiuchumi walioanzisha na ikawabadilishia maisha yao kiuchumi. Lengo hapa likiwa kuwahamashisha vijana kuweza kutafuta na kuanzisha miradi yao ya kujijenga kiuchumi na wasitegemee kuajiriwa kazi kwani hazipatikani


Katika CHAPTA 78, uk 2–7, mwandishi anadhamiria kuonyesha vijana changamoto ambazo wafanya biashara vijana hupitia katika juhudi za kukuza biashara zao. Katika biashara mambo huwa si mteremko bali kuna panda shuka nyingi zinazao hitaji uvumulivu mkubwa na kutokata tamaa.

Katika CHAPTA 93, uk 17-22, mwandishi analenga kuwazindua vijana kuhusiana na uwepo wa aina nyingi za kilimo biashara. Anafanya hivi kupitia mhusika Bruce ambaye ni kijana anayejihusisha na biashara ya kulima uyoga. Cha muhimu ni vijana kupenda kazi, biashara au kilimo wanachokifanya. Vilevile ni muhimu kuwa wazingatifu na kuelewa soko inahitaji nini na lini. Kisha, ni muhimu kutopoteza mwelekeo kwa anasa baada ya kufaulu kifedha. Katika uk 23-28, mwandishi anatoa mfano mwingine wa kilimo biashara wa ufugaji wa kuku kama kitegea uchumu kingine ambacho kina faida kubwa hivyo vijana wasidharau ufugaji wa kuku.

Katika CHAPTA 98, UK 1-7, mwandishi anashauri vijana kuwa wananafasi muhimu sana kuchangia katika kutafuta suluhu kwa halingumu inyoweza kuikumba jamii kama vile gharama ya maisha. Vijana wanafanya hivi kwa kutoa maoni yao katika mabaraza ya kijiji. Mwandishi anaonyesha fursa ambazo vijana wanafaa kuzitumia na kuwajibika kiasi cha kutoa maoni yao kwa machifu na kata katika ofisi za serikali gatuzi.

Katika CHAPTA 68, uk 10-15, sehemu kwa jina HUSTLA, mwandishi anawahimiza vijana kurudi mashambani na kutilia kilimo maanani kwani kunatija bora kilimoni tena ya haraka. Kama anavyokiri kijana Joseph Baraza mkulima wa sehemu za Narok. Vijana wanahimizwa kushiriki kilimo biashara. Katika CHAPTA

102, uk 2-7, mwandishi anahimiza vijana kuungana pamoja na kuanzisha mradi wa kujiinua kiuchumi kama ule wa kuwazolea watu taka zao za nyumbani kwa malipo. Ila anaonya kuwa kukiwa na wasiowaaminifu katika vikundi kama hivi na kuwaibia wengine basi panaweza kuwa na hatari ya kuvunjika kwake. Uaminifu na kutokuwa na tamaa ya kuwachezea wengine shere ni mambo muhimu katika makundi ya uwekezaji.




**Kielelzo cha 17 chapta 68 kutoka uk 14**

Katika CHAPTA 102, uk 12-17, mwandishi anawashuri vijana wajizoweshe kuweka akiba ya chochote kidogo wa patacho kwa kufanya hivi kutawawezesha kununu watakacho. Vilevile ni mbinu bora ya kujiinua kiuchumi na tabia bora ya kufuata

watakapo kuajiriwa. Katika uk 25, kupitia kwa tawasifu ya kijana mwekezaji wa biashara kilimo Joseph Kimani, mwandishi anawashauri vijana kuwa hata kama wamesoma. Vijana wanaweza kujiinua kiuchumi kwa kuanzisha biashara kilimo na hata kuunda matandao wa kuwasiliana baina ya wakulima au wakulima chipukizi na hapo kupata pato lake. Kwa mfano, Kimani hapa anawasiliana na wakulima kupitia wavuti WWW.THEAGRIPRENUER.COM.

Katika CHAPTA 109, uk 2-3, kupitia kwa mhusika Nick anayeendesha biashara ya hoteli, mwandishi anawashauri vijana kuwa watakapo weka biashara zao wakumbuke kuwa lazima wafanye bidii kuimarisha biashara hizo. Pia yawafaa wadumishe uaminifu kwa wateja wao na wajue kuongea vizuri na wateja wao. Wakifanya hivi biashara zao zitafaulu.


- **Vijana na masomo.**

Mwandishi analenga kudhihirisha changamoto za vijana wanapoendelea na masomoyao hasa katika shule za upili. Sehemu ya MARIA KIM katika toleo CHAPTA 33, inalenga kuzindua vijana wanafunzi wasichana wa shule za upili kuwa hata ingawa wanaishi sehemu duni za mabadani yaani ‘GHETTO’ na pengine ni mayatima na maskini kuwa wasikubali kutazama ufisadi ukitendeka katika jamii na wanajukumu pia kusimamana kupiga vipa jambo hili.

Vile vile katika toleo hili, MARIA KIM pia anawahimiza wasichana wa shule za upili kuwa kuangukia ujauzito na kujifungua mtoto wangali katika shule ya upili si mwisho wa maisha kwani wanaweza kurudi shule baada yakujifungua na kuendelea kukimbizana na ndoto zao za maisha na hatimaye kufanikiwa. Kwani elimu ndiyo silaha tu ambayo wasichana kama hawa wanaweza kutumia kupiga vita umaskini katika jamii.

Katika CHAPTA 88, uk 32, mwandishi analenga kuwapa vijana walio masomoni mawaidha ya mbinu dhabiti za kutumia wakati wanapo jiandaa kuukabili mtimani wao. Wanaweza kufanya muhtasari wa masomo, kutumia mitihani iliyofanywa hapo awali, kufanya marudio kwa makundi na kuwa na mpango wa kibinafsi wa kufannya

marudio.




**Kielelezo cha 18 kutoka Chapta 88 uk 32**

Katika CHAPTA 109, uk 4-9, mwandishi anawahiza vijana kujiamini na kujiandaa vizuri wakati wa mitihani. Anawaonya dhidi ya kutegemea mitihani bandia ambayo watadanganywa ndiyo itakayo kuja katika mtihani halisi kwani huenda wakapoteza pesa zao bure. Matokeo duni wakati mwingine hupatikana kwa njia hii ambapo wanafunzi husomea mambo ambayo kwenye mtihani halisi hayapo. Mwandishi pia na dhihirisha athari ya waliokatika mahusiano ya kimapenzi katika shule za upili hasa

katika kujiandaa wakati wa mitihani kwani changamoto hii hupelekea wanafunzi kuwa na matokeo duni.

- **Afya bora**

  Katika CHAPTA 33, sehemu ya MARIA KIM, mwandishi anawashauri wasomaji wake kuwa na umakini wanapochagua sehemu za kupata huduma za kiafya zifaazo wanapougua ili wapate huduma bora na kwa gharama nafuu. Sehemu ya CHARLIE PELE katika toleo hili, inatoa himizo kuhusu lishe bora ili kuepukana na majanga kama kuangukia upofu. Vilevile, sehemu ya CHARLIE PELE katika toleo lili hili inalenga kuhimiza umuhimu wa kula chakula bora kilicho na madini muhimu ya kumpa mtu afya imara. Anahimiza umuhimu wa kula viazi vitamu na maziwa kwani huwa na madini mengi ya vitameni.





**Kielelezo cha 19 katika Chapta 33 uk 27**

- **Matumizi ya lugha ya vijana ya Sheng**

Mwandishi ameandika kazi yake akilenga hadhira ya vijana na njia ya pekee yakufanikisha uwasilishaji wake ni kutumia lugha wanayo ielewa na wanayo jitambulisha kwao ambayo ni sheng. Lengo lake hapa ni kuonyesha kuwa sheng ni sehemu ya maisha ya vijana na nimuhimu kuielewa ilikuweza kuwasiliana kwa urahisi na vijana.

Katika CHAPTA 33 katika sehemu ya mwisho uk 29 ambayo inalenga kutoa burudani kwa wasomaji kwa kuwashirikisha katika utani wa 'MCHONGOWANO' na 'UJINGA NI?'.


MCHONGOANO

Eti wewe ni mlafi hadi unaonja maji ya sembe.

Wewe ni mnono mpaka ukitembea soil inasema tembea vizuri.

Boyie naskia manzi yako ameiva akikalia stool inageuka makaa

Nasikia Tv yenu ni old skul, ile advert ya harpic hufanywa na pit latrine.

Tv yenu ni ndogo mbaka ma-presentaz watangazanga waki-do Gully Creepa.

DJ Boyie we ni mtall hadi ni wewe huuzia watu wa ndege mutura

Ati kwenu kuna insecurity mpaka police station hufungwa saa kumi.

UJINGA NI

Ujinga ni kukua na Beef na mama Mboga.


Ujinga ni kukopa vitu kwa shop ulipe end month na uko Jobless.

Ujinga ni kumeza Mara moja Mara mbili

**Kielelezo cha 20 kutoka Chapta 33 uk 29**

Pia katika uk 9 katika CHAPTA 33 kuna 'SHENG DICTIONARY' inayolenga

kukuza msamiati wa wasomaji walugha ya sheng. Kwa mfano kuna maelezo ya maneno ya sheng kama vile: BWEKS ikimaanisha TWO, BINGI ikimaanisha DREADLOCKS n.k.




**Kielelezo cha 21 kutoka Chapta 33 uk 9**

Katika CHAPTA 93, uk 32 kuna mifano mingine ya maelezo ya maneno ya sheng kama vile: Bambe – high life/au life ya ubabe, ndenga/rithee/thwao – gun, kushandwa/ kuangushwa – shot, mbogi – gang, squad au crew nk.

- **Kukuza burudani.**


Mwandishi analenga kukuza burudani ya vijana kupitia vipera walivyoibua vijana vya fasihi simulizi vya 'mchongoano' na 'ujinga ni?'Katika CHAPTA 93, uk 32, kuna tamadhali za usemi za kukejeli/ kupigana vijembe yaani **Mchongoano** ambao ni semi za kuumbuana kiutani. Kwa mfano:

  - Uko meno ya yellow hadi ukifungua mdomo tumbo inakaa kama imewashwa bulb! [kuonyesha kiwango cha kuchafuka cha meno]
  - Kwenu mko wachafu hadi nzi za kwetu huita za kwenu nzi za Ghetto![kuonyesha kiwango cha kuchafuka]

- Uko na pimples mob kwa uso mpaka ukichukua photos, camera inadai ‘join the dots’![ kuonyesha wingi wa chunuzi]

**Ujinga ni?** Vilevile katika ukurasa uu huu kuna kipengele kingine cha burudani cha fasihi simulizi. Ujinga Ni? Ambacho kinahusu kuueleza vitendo ambavyo watu hutenda ambavyo huonyesha ujinga wao. Kwa mfano:

- Ujinga ni kumkatia dem kwa kanisa then unamlipia sadaka![kuonya dhidi ya utovu wa nidhamu kanisani]
- Ujinga ni kua mbele na panga after elections na hata Uhuru ama Raila hakujui![kuonya dhidi ya kushiriki vita baada ya uchaguzi]
- Ujinga ni kubeba makaa na umevaa T- shirt imeandikwa ‘lets conserve our trees’ [kuonya dhidi ya kutenda kinyume cha matarajio]
- Ujinga ni kuambia kipofu unenionea![ kuonya dhidi ya kutania walemavu]Ujinga ni kukopa landlord pesa alafu izo pesa ulipe nazo rent![kuonya dhidi ya ujanja wa kijinga]




**Kielelezo cha 22 kutoka Chapta 93 uk 32**

- **Teknolojia ya mawasiliano na vijana katika *Shujaaz.***

Mwandishi anadhamiria kuonyesha namna teknolojia ilivyo kuchua nafasi yake katika maisha ya vijana na kuwa sehemu muhimu katka mawasiliano yao. Sehemu ya mwisho inahusu maoni ya wasomaji wa *Shujaaz* lengo likiwa ni kuwaunganisha vijana kutoka sehemu mbali mbali kwa kuwapa sehemu ya kujieleza na kusaidiana kimawazo kupitia kutuma jumbe fupi kwa waandalizi wa *Shujaaz* kupitia nambari 20308 ambayo hailipishwi. Katika CHAPTA 88, uk 26-31, mwandishi anaonyesha namna teknolojia ta simu ina nafasi yake katika maisha ya vijana hasaa katika kujenga mahusiano baina yao zaidi katika masuala ya mapenzi.





**Kielelezo cha 23 kutoka Chapta 88, uk 7**

Katika CHAPTA 98, uk 13-15, mwandishi anwashauri vijana kuhusu kutumia simu ya rununu kujisajili na huduma za ushauri na shirika la T-SAFE linalotoa huduma kwa vijana kati ya miaka 15-19. Ambapo wakitembelea kituo hiki wanaweza kupata ushauri kuhusiana na mapenzi kabla ya ndoa, kupimwa ujauzito, kupimwa magonjwa ya kuonana kumwili/ kujamiana na ushauri na namna ya kuzuia kuangukia uja uzito. Katika sehemu huu nambari ya ujumbe mfupi ni tofauti ni **22699.**




**Kielelezo cha 24 kutoka Chapta 78 uk 15**

Katika uk 26-31, mwandishi anawashauri vijana kutumia simu zao kutafuta huduma za ushauri na maelekezo kutoka kwa vituo vya T-SAFE na FUTURE FAB. Nambari hii 22699 pia iko katika uk 31



**Kielelezo cha 25 kutoka CHAPTA 98 uk 22**

Katika uk17-22, mwandishi anaonyesha jinsi vijana wanaweza kutumia teknolojia ya simu kujipatia pesa kwa kushiliki michezo ya uwekezaji kama vile JANTA CHALLENGE, TOUCH DOH na JIACTIVATE.

Vilevile katika uk 23-25, mwandishi anaonyesha jinsi vijana wanaweza kujiimarisha kupitia kusoma kuhusu vijana wengine waliofaulu katika wayafanyayo; yawe masomo, biashara, usanii au uongozi. Yaani vijana wa kuigwa katika mtandao ya facebook na istagram sehemu ya Love and Hustle.

- **Kukuza talanta.**

**Kielelezo cha 26**




**kutoka Chapta 57 uk**

Mwandishi anadhamiria kuonyesha namna vijana wanavyofaa kutambua talanta zao, kuzikuza na kuzitumia kubadilisha maisha yao na ya jamii kwa jumla. Katika CHAPTA 57, uk 16-17 sehemu ya BOIYE, mwandishi analenga kuwachangamsha vijana kuwa wanaweza kujiajiri kwa kutumia talanta zao kama vile uimbaji waweze kujiinua kiuchumi. Pia anawahimiza kuunda mtandao wa kufahamishana kuhusu njia tofauti za kujiinua kiuchumi.

Katika Chapta 33, uk 30-31 ambayo ni sehemu ya MALKIA, Mwandishi analenga kuhimiza matumizi ya kawi mbadala ya ‘Bio-gas’. Sababu ikiwa ni kwamba kuanzisha mradi wa Bio-gas hakuna gharama kubwa na husaidia kuhifadhu




mazingira.

**Kielelezo cha 27 Chapta 33 uk 30**

Katika CHAPTA 57, sehemu ya CELEB, BOIYE anazungumza na msichana msanii mwimbaji maarufu kutoka Kingstone Jamaica kwa jina ALAINE ambaye picha yake halisi na yakuchorwa imetumika. Mwandishi hapa analenga kuhimiza vijana kuwa wasilalie talanta zao. Kwamba talanta zao zinaweza kuwatoa katika hali duni kiuchumi na kuwapa ajira nzuri na umaarufu pia.


Katika CHAPTA 68, uk 16 – 17, mwandishi kupitia kwa mwimbaji mashuhuri Victoria Kimani. Mwandishi anawahamasisha vijana wasikate tamaa wanapoendeleza talanta zoa kwani kufaulu si rahisi bari kunahitaji bidi, nidhamu na kutokata tamaa hadi siku mambo yatakapofunguka na fanaka kupatikana.

Katika CHAPTA 78, uk 8-9, mwandishi anawahimiza wasichana kuwa hakuna kazi yoyote wasiyoweza kufanya hata ya urubani kama alivyo faulu nahodha Liz Marami ambaye ni mwanadada wa kwanza nahodha nchini Kenya. Katika uk 16- 17 pia kuna tawasifu ya kijana Holy Boy wakutoka Meru ambaye kupitia kwake mwandishi anawahimiza vijana kuwa mahitaji yao na shida za maisha huenda ndizo zitawafanya kutambua talanta zao na hapo mambo yatabadilika na wakaweza kufaulu maishani.

Katika CHAPTA 88, uk 2-7 mwandishi anaonyesha nafasi ya shule na wazazi katika kukuza talanta za wanafunzi wangali chipukizi. Kwamba mchango na ushirikiano wa walimu na wazazi ni muhimu kufanikisha talanta kama uigizaji miongoni mwa wanafunzi. Katika uk24-25, mwandishi kupitia kwa kijana mpiga picha mashuhuri Ronald Tunoi, anataka vijana waelewe kuwa kila talanta inachangamoto zake na yafaa kuwa na uadilifu na mpango mwema ili kuifanikisha.

Katika CHAPTA 93, uk 8-9 mwandishi kupitia kwa tawasifu ya mwimbaji mashuhuri Phy Ngetich kutoka Sotik Kenya, analenga kuwashauri vijana kuwa wana haki ya kuwa na maisha mema na kupata kila kitu wanacho hitaji maishani. Lakini, ili kufanikiwa lazima wawe na bidii ili wakuze upekee wao katika wayafanyayo na kuwa gwiji watajika.

Katika CHAPTA 98, uk 16, mwandishi kupitia tawasifu ya msanii shupavu GOVI au Lemuel King Malik, anawashauri vijana kuwa kujenga jina ili kuwa maarufu huchukuwa muda na wasiharakishe kwa kuwa na tamaa ya pesa cha muhimu nikuwa wazingativu na kulenga kupata wanachokitaka. Vilevile anawakumbusha kuwa kufanikiwa ni majaaliwa ya Mungu na lazima waweke Mungu mbele ili wafanikiwe.





**Kielelezo cha 28 kutoka Chapta 98 uk 16**

Katika CHAPTA 102, UK8-9, mwandishi kupitia tawasifu ya mwigizaji mashuhuri CHEBET, anawashauri vijana wanaotaka kufaulu katika uwanja wa uigizaji kuwa lazima wajitume kwenda mahojiano ya wanaotaka kuwa waigizaji. Vilevile, inabidi wajiunge na vikundi vya uigizaji au wajaribu bahati yao katika majukwaa ya mitandao ya kijamii ambapo watu wanaohitaji waigizaji wanaweza kuwatambua na kuwapa nafasi za kujiendeleza.

Katika CHAPTA 109, uk 21-22, katika tawasifu ya kijana msanii wa vichekesho DR. OFWENEKE, mwandishi anawashauri vijana kuwa ilikufaulu katika kukuza talanta zao lazima wajikubali walivyo na wasijaribu kuiga watu wengine. Wakifanya hivyo bila shaka watafaulu.

- **Kukuza Ushujaa**




**Kielelezo cha 29 kutoka Chapta 68 uk 8**

Mwandishi anadhamiria kuhimiza vijana kuwa na moyo wa kuwajibika kujitolea kwa
hali na mali kuihudumia, kuiboresha na kuibadilisha jamii huku wakijijenga kiuchumi. Wawe na moyo wa kujitoa mhanga kuingia kutoa ushauri kwa vijana wenzao waweze kuwajibika bila ya kuwategemea wazazi wao kwa kila kitu. Paul Kuhuha katika Chapta 68 uk 8-9 ni 'Shujaa wa Mtaa' ambaye bidii yake binasfi licha ya changamoto nyingi utotoni mwake ameweza kujiimarisha kiuchumi kupitia biashara ya upigaji picha na vedio. Yeye ni shujaa wa kuigwa na vijana wengine.

Katika CHAPTA 12 kuanzia ukurasa wa 18 kuna naoni ya wasomaji yanayotolewa kuhusu SHUJAA ABRAHAM wa kutoka Eldoret. Abrraham anasifiwa na wasomoaji kwa namna anavyo endesha biashara yake ya kilimo biashara ya ukuzaji na uuzaji wa mboga. Katika ukurasa wa 19 kuna SHUJAA CHRISTOPHER wakutoka Dagoreti Nairobi ambaye anashiriki katika kampeni ya kutetea uwepo wa amani katika mtaa wake ambapo amani ilikuwa imekosekana kutokana na uhasana wa ubaguzi wa kikabila.

Katika CHAPTA 57, sehemu ya kwanza ya SHUJAA na BOIYE, uk3 mwandishi analenga kuhamasisha vijana na wanajamii kwa jumla kujitokeza na kuhudumia jamii bila ya kitarajia malipo. Kuwa ni muhimu kuungana na kuboresha jamii kwa kuchanga raslimali kidogo kila mtu au hata kujitolea kwa hali kuhakikisha jamii iko bora kama alivyofanya Dalton Wycliffe Odhiambo mkaaji wa Kibera. Dalton walianzisha huduma ya bure ya kuhifadhi usafi wa mazingira akiwa na wenzake bila ya kulipisha chochote na kufaulu kuweka mazingira ya hapo Kibera kuwa safi.

Katika toleo hili hili la CHAPTA 57, sehemu ya SHUJAA na CHARLIE PELE, mwandishi anahimiza uwajibikaji katika maeneo ya kazi kama alivyofanya Irene Mwihaki kutoka Sotik walipokuwa na shida ya maji alipokuwa akifanyia kazi yake ya saloon. Aliwajibika na kwenda kwa idara ya maji ya serikali gatuzi ya Sotik na wakasaidika pamoja na wapangaji wenzake. Faida na biashara yake ikaimarika.

Kufikia hapa ni dhahiri kuwa dhamira zilizoshughulikiwa katika Shujaaz zinaafikiana na maoni ya Ntarangwi (2004) kuhusu dhamira anaposemma kuwa dhamira ni azma, lile lengo au kusudi la mtunzi katika kuitunga kazi yake. Hii ni kwa sababu, aghalabu kila mtunzi huwa amesukumwa na jambo fulani (liwe zito au jepesi) katika utunzi wake. Kama ilivyotangulia kutajwa, hakuna mtunzi anayeweza kutunga katika au kutokana na ombwe, ni jambo linalomsukuma msanii kuandiks kazi yake ili aweze kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Maelezo ya Pamela (2018) yanahitimisha sehemu hii ya dhamira anaposema kuwa *Shujaaz* ni chapisho linalolenga kuelemisha na hata kuburudisha vijana katika jamii kupitia msimbo wa *Sheng* na mitindo changamano wa uwasilishaji wa ujumbe huo. Kwa hivyo *Shujaaz* ni kazi iliyotungiwa vijana kwa hivyo dhamira zake ni dhamira zinazohusu vijana zaidi kuliko wanajamii wengine.

- **Ujumbe/Maadili**


  Kulingana na Mlaga (Khj), Ujumbe ni funzo au fundisho linalopatikana katika kazi ya fasihi. Ujumbe pia hugawanyika katika aina mbili ambazo ni; ujumbe mkuu na jumbe

  zinazoendana na dhamira ndogo. Ujumbe mkuu hutokana na dhamira kuu na pia jumbe nyingine hutokana na dhamira zile ndogondogo. Kwa hiyo, ujumbe ni funzo na maadili yaliyokusudiwa na mtunzi yawafikie hadhira aliowalenga kufikisha kazi yake ya fasihi. Ujumbe pia katika kazi ya fasihi ni mafunzo mbali mbali yapatikanayo baada ya kuisoma kazi ya fasihi. Ni mafunzo/maadili mbalimbali ambayo msomaji/msikilizaji huyapata baada ya kutumia/kupitia kazi fulani ya fasihi. Wamitila (2002) Mafunzo katika kazi ya fasihi hupatikana kupitia dhamira zilizojitokeza katika kazi husika.

Katika *Shujaaz* matoleo yote yanalenga kuadilisha vijana katika maswala ya aidha ya kisiasa, kijamii na kiuchumi Kwa mfano katika CHAPTA 109 mafunzo yafuatayo yanadhihirika:

a) Katika dondoo liliopo hapa chini, inabainika kuna funzo la uwajibikaji na

umuhimu wa kujazatiti kujikimu kiuchumi kupitia biashara. Jambo hili linaingiliana moja kwa moja na hali ilivyo katika jamii hivi sasa. Ukosefu wa kazi za kuajiriwa umekithiri jamii hasa vijana na njia inayopendenkezwa




hapa ni kwa vijana wajiajiri wao wenyewe.  Wanapendekezewa wafanye hivi kwa kuanzisha biashara za kuwawezesha kuyakimu mahitaji yao na kujikuza kiuchumi. Mwandishi wa *Shujaaz* anayawasilisha haya katika matoleo yote yaliyo na sehemu ya HUSTLE FITI kama ilivyo katika uk 2-3.

**Kielelezo cha 30 kutoka Chapta 109, uk 3**


b) Kuna mafunzo kwa wanafunzi kuhusiana na maswala ya masomo na mahusiano baina ya wanafunzi wa shule za upili. Mwandishi wanawashauri wanafunzi wawe waaminifu na wazingatifu masomoni hasa wakati wa mitihani.  Katika Chapta 109, uk 6 wanafunzi wanaletewa mtihani bandia na mwenzao akidai kuwa ulikuwa 'leakage' pengine uitwe mtihani wa kuvuja lakini mtihani halisi ulipoletwa wananfunzi wanashikwa na bumbuwazi ka kuwa walidonganywa

Tatizo hili likiwa sugu hupepekea wanafunzi wengi kufeli katika mitihani. Inapoibuka kuwa mtihali walidhani ni wa kweli ni gushi huenda kukawa na vurugu baina ya wanafunzi na aliyewauzia au wapa mtihani huo gushi.


Mwandishi anawahimiza wanafunzi kujiamini na kukujiandaa vilivyo kabra ya mtihani wowote ule ili waweze kufaulu. Haya yanapatika na katika uk 6 -7 katika CHAPTA 109




**Kielelezo cha 31 kutoka Chapta 109 uk 6**



**Kielelezo cha 32 kutoka Chapta 109 uk7**




**Kielelezo cha 33 kutokaChapta109 uk 8**

b) Mwandishi anaonyesha umuhimu wa wanafunzi kuzingatia masomo na kuepukana na mahusiano ya kimapenzi wangali wananfunzi. Anahimiza kuwa wawezi kuachana na mahusiano hayao hadi wamalize masomo yao. Kwa mfano katika sehemu ya MARIA KIM akiwa Jongo High School. (uk4).



Vijana napatiwa mafunzo kuhusiana na hatari za ngono za bila kinga kama ilivyo katika sehemu ya #Sista Sauti (uk 10-12) na MALKIA #BforBae (uk 9-20)




**Kielelezo cha 35 kutoka Chapta 109 uk 20**




**Kielelezo cha 36 kutoka Chapta109 uk 18**

c) Vijana wavulana wanaadilishwa kuhusiana na kuwajibika katika mahusiano ya mapenzi kabla ya ndoa kama ilivyo katika sehemu ya MALKIA (uk 13-18). Katika dondoo hili, mvulana kwa jina Cheezy Fresh anajipata amewatia mimba wasichana watatu. Wote wameamua kuletea watoto baada ya kujifungua na kumuachia hao watoto alee. Mwandishi hapa anaadilisha wavulana kufahamu kuwa kuna hatari ya kupata Watoto wakati ambao hawajapanga kupato iwapo wameshaingiliana kimapenzi na kila mscichana wapatanao naye bila hata kutumia kinga. Matokeo ya tabia hii ya kiholela yakiwa ni watoto lazima waajibike katika kulea watoto hawa wanaopata kiholelaholela.




**Kielelezo cha 37 kutoka Chapta 109 uk 16**

d) Vijana wanafunzwa wasijidharau bali wajiamini na kukuza talanta zao kwani talanta hizi zaweza kuyafanikisha maisha yao na kuwafanya wawe maarufu. Kwa mfano katika sehemu ya mahojiano ya DJ BOIYE na Celeb. Dr. Ofweneke (uk 21-22). Mwandishi ametumia msanii huyu wa vichekesho kama mfano kwa vijana kuwa talanta aliyonayo kijana asiidharau kamwe. Kinachohitajika ni kujiamini na kujituma. Kwani akiitumia inaweza kuyabadili maisha yake na ya

aila yake. Jambo la kimsingi hapa ni kijiamini na kuwa na nidhamu katika kuitumia talanta husika ili kupata ufanisi.




**Kielelezo cha 38 kutoka Chapta 109 uk 22**

**ii)** Migogoro.


Kwa mujibu wa Mlaga (2017), migogoro ni mivutano au kutoelewana kwa pande mbili tofauti. Hiki ni kipengele muhimu sana katika kuendelea kwa kazi ya fasihi. Ili kazi izidi kuenda mbele hutegemeana ufundi wa kujenga migogoro baina ya wahusika, katika kiwango cha mtu binafsi, kati ya mtu na mtu, mtu na jamii, jamii na jamii au hata taifa na taifa. Namna migogoro inavyosuluhishwa huwa msingi muhimu wa ujenzi wa taharuki, na hata kuelekea kufika katika kilele cha kazi ya fasihi. Katika mchakato wa kusuluhisha migogoro iliyomo katika kazi maalumu ya kifasihi, maswali yanaweza kujibiwa kwa ukamilifu au baadhi ya maswali yasipate majibu mpaka mwisho wa kazi husika.

Migogoro ni mivutano na misuguano mbali mbali ambayo huibuliwa na mwandishi katika kazi ya fasihi. Mgogoro kati ya wahusika ama vikundi vya wahusika, familia zao matabaka yao n.k. Migogoro hii mara nyingi hujikita katika mahusiano ya kijamii na ndipo tunapata migogoro ya: kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kinafsia (kifikra).

Kwa kuzingatia matoleo ya *Shujaaz* yaliyoteuliwa kuna miogogoro ifuatayo inayojibainisha:

a) Kuna migogoro wa kisiasa baina ya vijana na viongozi kuhusiana na suala la uongozi mbaya wa kuwapotosha vijana kisiasa. Kwa mfano Toleo la SPECIAL EDITION 01/03 sehemu ya BOIYE uk2-4 kuna swala la viongozi kutumia hongo kuwarai vijana kwenda kunyume cha nia zao. Vijana wanashawishiwa kwa pesa chache kuzusha vururgu wakati wa kutafuta kura ili kuhangaisha wapinzani wa wanaowapatia hera hizo. Jambo ambalo laweza kuvuruga amani ya jamii na taifa nzima.


Katika CHAPTA 33 uk18-19, mwandishi anahimiza vijana kutambua kuwa wakati umefika wazinduke na wawachague vijana wenzao wawakilishe katika nyadhifa za uongozi kwa kijana mwenzao anaelewa vyema shida na mahitaji yao. Mwandishi anatoa mwongozo wa jinsi vijana wanavyoweza kujiingiza katika ulingo wa kuwania nyadhifa za uongozi kwa kujiunga na chama wakipendacho cha kisiasa. Wanatakiwa kujihusisha na shughuli zote za chama hicho. Iwapo hawana hawana chama wanaweza kusimama kama wagombea vitu wa kibinafsi au wa kujisimamia. Kisha wahakikishe wametimize masharti yote ya tume ya uchaguzi..



Kielelezo cha 39 kutoka 33 uk19






Kielelezo cha 40 kutoka Chapta 33 uk18



**Kielelezo chs 41 kutoka Chapta 33 uk 19**

b) Kuna migogoro wa kijamii baina ya vijana wenyewe kuhusu mahusianao ya kimapenzi, mimba za mapema, ukosefu wa kazi, uhalifu, ukabila na masuala ya kimasomo n.k. Kwa mfano CHAPTA 88 inashughulikia mambo kadha yanayohusu changamoto za vijana: ukosefu wa kazi uhalifu, anasa, mapenzi na afya na lishe bora. Katika uk 17- 22, mwandishi anadhihirisha namna ukosefu wa kazi umesababisha mgogoro baina ya vijana watafuta kazi na magege ya wanyanganyi. Mfano ukiwa namna genge la Scarface lilivyomfanyia Manlike ambapo wanamwibia baada ya kumpa kazi wa kuweka vibandiko vya picha za mwanasiasa mtaani.






**Kielelezo cha 43 kutoka Chapta 88 Uk 20**

Katika SPECIAL EDITION 01/03 mwandishi ameangazia suala la elimu na changamoto wanazopita wakati wa kampeni za uchaguzi wa kitaifa au hata shuleni wakati wa kuchagua viranja wa kuwaongoza wanafunzi shuleni. Katika uk 11, mwandishi anatoa mfanao wa namna watu huchochea chuki za kikabila baina ya makabila jambo ambalo huenda likasababisha vita vya kikabila kama anavyo hofia mhusika Charlie Pele katika ukurasa wa 12. Mhusika huyu ananeleza namna jamii ziliteseka hapo awali kutokana na vita vya baada ya uchaguzi ambapo familia

nyingi ziliwapoteza wapendwa wao, mifugo ikaibiwa, nyumba zikachomwa na kubomolewa n.k. Mwandishi wanahimiza vijana kuwa katika mstari wa mbele katika kutafuta suluhu la tatizo hili kabla ya janga kutokea. Mwandishi anatahadharisha dhidi ya kushiriki kitendo cha uchochezi wa uhasama baina ya makabila tofauti kwamba anayehusika na kitendo hiki ana weza kufungwa gerezani kwa kipindi cha miaka 5 ama apigwe faini ya hadi shilingi milioni moja ama zote mbili.




**Kielelezo cha 44 kutoka SPECIAL EDITION 01/03 uk 11 na 12**

c) Kuna mgogoro wa kiuchumi baina ya vijana wakipambana na hali ngumu za kichumi. Mwandishi anaonyesha namna vijana wanazozitumia kujikomboa kutoka lindi la umaskini. Vilevile kupitia wahusika tofauti katika sehemu za HUSTLE FITI katika CHAPTA 109, uk 2-3, HUSTLA katika CHAPTA 68, uk 10-15, SHUJAA katika CHAPTA 57, uk19-24, sehemu za CELEB katika CHAPTA 88, uk 24-25, sehemu ya Boiye Top Hustla katika CHAPTA 78, uk 2-3, na sehemu zingine kama ya MARIA KIM katika CHAPTA 102, uk 2-7. anapendekezea vijana mbinu tofauti au kazi tofauti ambazo vijana wanaweza tumia kujikwamua kutoka umaskini. Kwa mfano uliopo katika sehemu ya MARIA KIM katika

CHAPTA 102, uk 2-7 mwandishi anaonyesha namna vijana wanaweza ungana pamoja na kuanzisha kazi ya kuzolea watu taka kwa malipo kwa kutumia rukwama. Lakini changamoto inayowakumba ni swala la kutoaminika kwa baadhi ya washiriki ambao wanatamaa na ujanja. Mfano ni kitendo cha mhusika Chuxx ambaye alienda na kuchukua malipo kutoka kwa wateja wao bila ruhusa ya wenzake. Nia yake ikiwa ni kuwalaghai.




**Kielelezo cha 45 kutokaChapta 102 uk 2**

Kimsingi sifa inayojitokeza hapa ni kuwa *Shujaaz* ni kazi inayolenga sana vijana na migogoro wanayopitia maishani na namna ya kujinasua kutoka changamoto hivi na kuweza kuimarisha maisha yao nay a jamii kwa jumla.

**iii) Falfasa**

Huu ni mwelekeo wa imani ya mwandishi wa *Shujaaz*. Falsafa yake inajitokeza katika yale anayoyashughulikia zaidi kwa nia ya kusisitiza ujumbe mahususi. Falsafa ya mwandishi wa *Shujaaz* ni umuhimu wa ujana. Kulingana na mwandishi vijana wanajukumu la kuwajibika katika masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ili ileta maendeleo katika jamii.

Katika sekta ya kijamii kwa mfano, swala la mahusiano ya kimapenzi miongoni mwa vijana amelishughulikia katika matoleo karibu yote huku akisisitiza umuhimu wa vijana kutumia mbinu za kujikinga dhidi ya magonjwa ya kuonana kimwili na vile vile changamoto za kupata mimba za mapema kutokana na kushiriki ngono bila kinga. Mahusiano yao ya kimapenzi ndilo jambo kuu ambalo huporomosha maisha ya vijana. Linapashwa kuchukuliwa kwa uadilifu na vijana. Kijamii mwandishi anashikilia kwamba vijana wanajukumu la kukuza na kutetea umoja wa wanajamii kwa kupiga vita ukabila na ubaguzi wowote uwe wa kujinsia au kikabila.

Vilevile mwandishi na imani kuwa mabadiliko ya kisiasa yataletwa na vijana hasa watakapo jiinginza katika ulingo wa siasa na kuungwa mkono na vijana wenzao au wakiungana na kuchagua viongozi wanaojali maswahi yao kama vina na wote umma kwa jumla. Walenge kuwaondoa viongozi wafisadi wanoibomoa jamii kwa sera zaombovu na uongozi wao mbaya. Ni kazi ya vijana kupinga uongozi mbaya na kuhamasisha umma dhidi ya uongozi kama huo. Mfano mzuri unapatikana katika toleo la SPECIAL EDITION 03/03.

Katika maswala la uchumi, mwandishi ana imani kuwa vijana wakiacha kutegemea kuajiriwa na wajiajiri kwa kutumia talanta zao, kuanzisha biashara ndogo ndogo, au kuungana wakaanzisha mradi wakujipatia pato na kuikuza kiuchumi. Yaani, kujiamini na kujituma kwa nia ya kujitegemea.

Sifa bainifu kuhusiana falsafa ya mwandishi katika *Shujaaz* ni kwamba matoleo yote yanahusu umuhimu wa ujana katika jamii. Kwamba vijana ndiyo tu wataimarisha jamii wakifaulu kuimarisha maisha yao katika jamii; kisiasa, kijamii na kiuchumi.

**iv) Msimamo**

Kwa mujibu wa Senkoro (1987), Mimamo wa mwandishi ni dhana inayorejelea mwelekeo wa mwandishi katika kukabiliana na hali au tatizo iliyopo katika jamii yake. Kuna aina mbili za misimamo: msimamo wa kimapinduzi na msimamo wa kibwanyenye. Msimamo wa kimapinduzi unahusiana na kutaka kuyaondosha matatizo yaliyopo katika jamii ya mwandishi au msanii. Je, anaonyesha mwelekeo wa kutaka kuondosha matatizo yote kwa njia yeyoye ile? Akionyesha msimamo huu wa kutaka

kuondosha matatizo ya jamii yake huwa ana msimamo wa kimapinduzi. Msimamo wa kibwanyenye ni msimamo ambapo mwandishi au msanii huonyesha mwelekeo wa kuhalalisha tu matatizo yaliyopo katika jamii yake akijitahidi kubuni sababu za uongo juu ya kuwepo kwa matatizo hayo. Msanii au mwandishi akiwa na mwelekeo huu huwa ana msimamo wa kibwanyenye.

Mwandishi wa *Shujaaz* anamsimamo wa kimapinduzi. Anashikilia na kutetea mageuzi ya uongozi katika jamii bila kujali kuwa jambo hili linakubalika au la. Misimamo ya mwandishi wa *Shujaaz* ni wa kimapinduzi hasa pale anapoamua kutumia wahusika vijana wakiwa wa kuchorwa au viumbe hai waliopigwa picha. Dhana ya upatanisho, ushirikianao wa taaluma mbalimbali na uporomoshaji wa masafasa unabadili namna kazi nyingi za fasihi zinavyotungwa kifani na kimaudhui. Maudhui yake yanayowasilishwa hasa na wahusika vijana yanalenga kusisitiza umuhimu wa vijana katika kuibadilisha jamii kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mwandishi wa *Shujaaz* anawaona vijana ndiyo tegemeo la kuleta maisha bora katika jamii. Matoleo yote ya *Shujaaz* yanadhihirisha haya kwani hakuna toleo ambalo wahusika wake wakuu ni wazee au watu wa makamo. Wahusika wake wote wakuu ni vijana ishara kwamba wakati wa vijana umefika wabadili mawazo yao kutazama mambo yakiharibika katika jamii bila ya wao kuchukua hatua kubadilisha mambo. Wahusika wakuu; wawili wakiume (DJ. BOIYE na CHARLIE PELE) na wasichana wawili (MARIA KIM na MALKIA) ndiyo wanatumiwa wa mwandishi kuendeleza msimamo huu. Maudhui yote katika *Shujaaz* yanazunguka vijana na yanawasilishwa kupitia vijana. Kwa kufanya hivi anasisitiza usawa wa kijinsia katika nafasi ya vijana katika jamii.

Sifa bainifu inayojitokeza kuhusiana na msimamo wa mtunzi wa *Shujaaz* ni kuwa wakati wa vijana kuhamasishwa na wao kuhamasishana kwa nia ya kuwaelekeza na wao kuelekezana umefika iwapo jamii inatarajia kupiga hatua mwafaka kisiasa, kiuchumi na kijamii. La sivyo, jamii itasambaratika kijamii, kiuchumi na kisiasa. Sifa nyingine ni kuwa *Shujaaz* imezamia katika kushughukikia maisha ya vijana nyumbani, shuleni na mitaani katika matoleo yake yote kuliko inavyoshughulikia maisha ya wahusika wengine wazee na wazazi katika jamii na shughuli zao.

### v) Mtazamo

Mwandishi wa *Shujaaz* na vile anavyoyaangalia mambo katika usimulizi wake kama anavyoeleza Wamitila (2008), kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi huwa ana namna anavyoangalia mambo yanayosimuliwa katika kazi hiyo ya fasihi. Mtazamo huhusishwa na maudhui au dhamira kwa kuangalia kiwango au sawia ya lugha kwa kuwa hii ndiyo sawia inayoweza kuonesha mkabala anaouchukulia msimulizi au mwandishi kuyahusu masuala yanayoendelezwa katika kazi husika. Mtazamo ni hisia au uelewa wa mwandishi juu ya jambo fulani.

Kwa mujibu wa Mlaga (2017), mtazano ni dhana inayorejelea juu ya misingi ambayo mwandishi au msanii huitumia katika uchambuzi au uelewa wa matatizo au juu ya utoaji wa suluhu ya matatizo yaliyopo katika jamii. Kuna aina mbili za mitazamo: mtazamo wa kiyakinifu na mtazamo wa kidhanifu. Mtazamo wa kiyakinifu ukiwa ni msingi ambapo uchambuzi, uelewaji wa matatizo, na hata wakati mwingine utatuzi wa mwandishi au msanii huegemezwa katika ushahidi au njia za kisayansi. Katika aina hii ya mtazamo mwandishi au msanii anatumia mawazo ya kisayansi kuliko mawazo ya kidini katika mchakato wa utafutaji wa suluhisho ya matatizo yaliyopo katika jamii husika. Mtazamo wa kidhanifu ni msingi ambapo uchambuzi, uelewaji wa matatizo, na hata wakati mwingine utatuzi wa mwandishi au msanii huegemezwa zaidi katika mambo ya kiimani zaidi kuliko njia za sayansi. Katika aina hii ya mtazamo mwandishi au msanii anatumia mawazo ya kiimani au kidini kuliko mawazo ya kisayansi katika mchakato wa utafutaji wa suluhisho ya matatizo yaliyopo katika jamii husika. Kipengele cha mtazamo wa msanii huonyesha ukweli kwamba sayansi na dini bado zipo kwa pamoja hata sasa hivi. Na ndiyo sababu kuna watu ambao wanaamini katika sayansi na dini kwa wakati mmoja na kuna wengine wanaoamini katika sayansi tu. Kwa mfano mwandishi anaweza kutazama jambo fulani kwa mtazamo wa kidini, au anaweza kutazama jambo fulani kwa mtazamo wa kisiasa au kisayansi.

Mwandishi wa *Shujaaz* ana mtazamo wa kiyakinifu. Kila toleo la *Shujaaz* limesheheni maudhui yenye dhamira tofauti ambazo lengo lake ni kutafuta

suluhisho la matatizo yanayoikumba jamii. Matoleo ya CHAPTA 109, 102 na 57, yana maudhui ya uchumi na biashara. Yaliyomo yanadhihirisha mtazamo wa mwandishi kuhusiana na uchumi. Kwani, anaiangalia jamii yake na kutambua mahitaji ya kiuchumi yaliyopo na kujaribu kupendekeza namna vijana wanavyoweza kuchangia katika kusulushiza matatizo ya kiuchumi. Anapendekeza kwa mifano halisi namna vijana wanavyoweza kufanya hivi na hata kuweza kuimarisha hali iliyopo ya kiuchumi. CHAPTA 33, uk 10-15, maudhui yaliyopo yanahusu matatizo ya afya bora na lishe bora. Mwandishi akielezea kwa mifano namna ya kutatua matatizo ya lishe na afya ya jamii. Anapendekeza hatua mahsusi na muhimu za kutafuta huduma za kiafya katika vituo vya afya vya umma badala la kijitibu kwa kununua madawa katika duka za dawa bila maagizo ya daktari.

**vi) Itikadi**


Kwa mujibu wa Jesse (2017), itikadi ni jumla ya mfumo wa mawazo, fikra na imani, inayoongoza na kumwelekeza mtunzi katika kuwasilisha ulimwengu wake kwa maswala mbalimbali yanayohusu mifumo kisiasa, kiuchumi na kijamii katika jamii yake. Itikadi hutazamwa kama mawazo au mwongozo wa kimawazo unaoudhibiti mkabala wa mwandishi kuhusiana na masuala mbalimbali. Hapa itikadi inafungwa kwa mtunzi au mwandishi wa kazi ya kifasihi. Itikadi ni jumla ya mawazo ambayo hudhibiti au hujaribu kudhibiti jinsi watu wa jamii fulani inayohusika wanavyoukabili, kuufasiri na kuuelewa ulimwengu wao.

Katika *Shujaaz*, itikadi inayojitokeza ni kuwa vijana ndiyo nguzo kuu katika kuindeleza na kuiongoza jamii katika majukumu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika *Shujaaz*, itikadi inayotawala utunzi wa mwandishi ni kuwa vijana wana nafasi kupitia hali ya maisha yao kisiasa, kiuchumi na kijamii kuweza kuelekeza na kuongoza namna ambavyo mifumo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia inavyoweza kuathiri jamii. Kuporomoka kwa msingi ya kitamaduni katika jamii kumepelekea changamoto ambazo vijana wanapitia katika shughuli zao za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Vijana hawapitii hali hizi kwa kujitakia mbali ni kutokana na mifumo ya kijamii ambayo imekengeuka na kukosa udhabiti wa ni vipi haswa vijana wanavyofaa kuhusiana.

Kwa mfano katika CHAPTA 68, mwandishi ameshughulikia maudhui ya mapenzi na anasa za vijana na changamoto zake kwa vijana katika sehemu ya MALKIA na ya MARIA KIM. Ukiangalia sehemu hizi vijana katika jamii hii ya mwandishi wanaishi wanavyoishi kwani hayo ndiyo mazingira na mwelekeo ambao jamii imewapa. Wanauhuru wa kuingiliana bila vidhibiti vyovyote vilivyowekwa na jamii, wanashiriki wayatakayo kwani hakuna kidhibiti kilichowekwa na jamii. Wanabaki kujitafutia na kufuata mkondo wowote waupendao nahapa ndipo mwandishi anaonelea kuwa kilichobaki ni vijana kushauriana na kuelekezana kwa misingi ya kimaadili kama wanavyoelewa wao wenyewe




**Kielelezo cha 46 kutoka Chapta 68 uk 5**




**Kielelezo cha 47 kutoka Chapta 68 uk 19**

**5.4 Fani katika *Shujaaz***

Fani ni ufundi wa kisanaa utumiao msanii katika kutoa ujumbe wake kwa hadhira iliyokusudiwa. Fani katika fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii inayohusika. Kwa mujibu wa Senkoro (2011) na Mbatia (2001), fani ni ufundi wa msanii katika kuumba umbo la kazi ya fasihi kutokana na ubunifu wake. Fani ni ufundi ambao msanii anautumia katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Katika fani kumegawanyika vipengele mbalimbali kama vile wahusika, mitindo, muundo, mandhari na matumizi ya lugha. Vipengele hivi vinaingiliana na kutegemeana. Fani huwa na jukumu la kuupa utungo wa kifasihi umbo mahususi ambao hujengwa kutokana na muingiliano baina ya vipengele hivi vya kifani. Kwa hivyo muundo wa ndani ndio umezingatiwa kwa kuwa unaingiliana sana na msuko, yaani mfuatano wa matukio na mahusiano yake kiwakati na kiusababishi. Dhana za upatanisho, ushirikiano na mwingiliano wa taluuma, kuporomoka kwa masafa na ubadilishanaji wa mawazo ndizo zitakazo ongoza uchambauzi wa vipengele hivi vya fani.

Katika sehemu hii ya fani uhakiki umechunguza vipengele vya fani katika *Shujaaz* ambavyo ni: muundo au mtiririko (ploti) wa kazi, mtindo alioutumia mwandishi katika kazi yake, lugha

aliyoitumia na ameitumia namna gani, mandhari katika kazi hii, wahusika waliopo na jinsi mwandishi alivyowasawiri wahusika wake.

a) **Muundo**

Wamitila (2008) anaeleza kuwa muundo ni umbo na mpatano, mshikamano na huhusu visehemu tofauti vya kazi inayohusika. Senkoro (2011), Katika kazi ya fasihi muundo ni mpango na mtiririko wa kazi hiyo kwa upande wa visa na matukio. Muundo ni mgawanyo, mpangilio na mtiririko wa kazi hiyo kwa upande wa visa na matukio.

Muundo katika *Shujaaz* ni ule wa moja kwa moja. La muhimu kutaja hapa ni kuwa kila toleo huwa na sehemu kadha ambazo hazihusiani na hujisimamia kama zilivyo katika diwani ya hadithi fupi. Yaani kila sehemu katika toleo huwa na wahusika wake, matukio yake, maudhui yake tofauti na sehemu hizo nyingine. Katika *Shujaaz*, kuna matoleo yenye idadi tofauti za kurasa kutegemea yaliyomo katika toleo husika;

- Baadhi ya matoleo yana kurasa 16. Kwa mfano matoleo ya kipekee (SPECIAL EDITION. KAMA SPECIAL EDITION 03/03) ambayo yana sehemu tano ambazo ni: sura ya toleo uk 1, sehemu ya DJ BOIYE uk2-4, sehemu ya MALKIA uk5-7, sehemu inayohusu pendekezo la marekebisho ya katiba uk8-9, sehemu ya CHARLIE PELE uk10-12, sehemu ya MARIA KIM uk 13-15 na sehemu ya nyuma yenye tangazo uk 16
- Kuna matoleo kurasa 24, kwa mfano, CHAPTA 68, 78, 109 kati ya matoleo mengine. Kila toleo hapa likiwa na sehemu tofauti tofauti.
    - CHAPTA 68 ina: sura ya toleo picha ya Victoria Kimani uk 1, MALKIA uk2-7, SHUJAA WA MTAA – Paul kahuha aka Protisa, uk 8-9, HUSTLA na CHARLIE PELE na Joseph Barasa uk10-15, CELEB – DJ BOIYE na Victoria Kimani uk 16-17, MARIA KIM uk18-23 na CLASE OF CONFIDENCE – ACTRESS VERA uk 24.
    - CHAPTA 78 ina: picha ya DJ BOIYE na LIZ MARAMI uk 1, BOIYE uk2- 7, CELEB – DJ BOIYE na Liz Marami uk8-9, MALKIA uk 10-16, JITUME
    UPENYE – Holy Boy uk 16-17, MARIA KIM uk 18-23 na tangazo uk 24.
    - CHAPTA 109 ina: sura iliyo na picha ya DR. OFWENEKE uk 1,

HUSTLE FITI – BOIYE na Nick uk 2-3, MARIA KIM uk 4-9, #SistaSauti na MARIA KIM uk10-12, MALKIA uk 13-18, #BforBae na MALKIA uk19-20,

CELEB- BOIYE na Dr. Ofweneke uk 21-22 na matangazo uk 23-24.

Kutokana na Ushahidi huu ni dhahiri kuwa matoleo haya ya kurasa 24 hayana mpangilio maalum wa sehemu zilizopo. Kila toleo likiwa na seheumu zake zilizo pangwa kivyake.

- Kuna matoleo yaliyo na kurasa 32. Kwa mfano, CHAPTA 12, 27, 33, 57, 88, 93, 98, 102 kati ya matoleo mengine. Kila toleo lina sehemu tofauti ndani yake kama ifuatavyo:
    - CHAPTA 12 ina: sura iliyo na BOIYE, MARIA KIM, MALKIA NA

      CHARLIE PELE. Wote wameizungukia keki iliyoandikwa SHUJAAZ IS ONE. Keki ina msumaa mmoja uliowashwa. Yaelekea wanasherehekea umoja wao. Katika uk2, kuna tangazo la Safaricom. Uk 3-12 ni sehemu ya BOIYE kuhusu kumbukumbu yam waka mmoja uliopita kuhusu sehemu ya BOIYE. Uk 13-15, inahusu MALKIA na kumbukumbu za sehemu yake mwaka mmoja uliopita, uk 16-17 inahusu BOIYE kuhusu FAN ART, uk 18, unahusu maoni ya maoni ya shabiki wa Shujaaz kwa jina ABRAHAM na uk 19 maoni ya shabiki CHRISTOPHER. Uk 20-22 ni sehemu ya MARIA KIM kuhusu kumbukumbu ya sehemu yake yam waka uliopita. Uk 23-26 ni sehemu ya CHARLIE PELE vile vile ikiangazia kumbukumbu ya sehemu yake ya mwaka. Uk 27 na 28 inahusu maoni ya mashabiki PATRICIA na DUNCAN. Uk 29 ina husu BOIYE na MARIA KIM mada ikihusu siku ya mapenzi. Uk 29 haki 32 ni sehemu iliyo na maswali kwa wasomaji kupima ufahamu wa wasomaji kuhusu *Shujaaz.*
    - CHAPTA 27 ina: sura iliyona picha ya mwanafunzi Maria Kim na kiumbe cha ajabu uk1, yaliyomo na tangazo uk2-3, DJ BOIYE uk 4-9, MALKIA uk 10-15, SHUJAA OF THE MONTH uk 16-17, MARIA KIM uk 18-23, QUALITIES POA ZA RELATIONSHIPS uk 24, CHARLIE PELE uk25-30, MCHONGOANO, UJINGA NI? na SHENG DICTIONARY uk 31 na tangazo uk 32.
    - CHAPTA 33 ina: tangazo katika sura uk 1, yaliyomo uk 2, BOIYE uk 3-8,

CHARLIE PELE na SHENG DICTIONARY uk 9, MARIA KIM uk10-15, matangazo uk 16-17, CHUXX 4 MP uk 18-19, ART KORNA uk 20-21, matangazo uk 22, CHARLIE PELE uk 23-29, MALKIA uk 30-31 na tangazo uk32.

- CHAPTA 57: sura ina picha ya msanii ALAINE uk 1, tangazo uk 2, SHUJAA - BOIYE na Bw, Odhiambo uk 3-8, tangazo uk 9, MARIA KIM uk10-15, CELEB – BOIYE na ALAINE uk 16-17, DJ B LOOK ALIKE uk

  18, SHUJAA- CHARLIE PELE na Irene Mwikali uk19-24, tangazo uk 25, MALKIA uk 26-31 na MCHONGOANO na UJINGA NI? uk 32.
- CHAPTA 88: sura ina picha ya RONALD TUNOI uk 1, MALKIA uk 2- 7, tangazo uk 8, MARIA KIM uk9-14, Wife material ana Smoke-DJ BOIYE uk 15-16, BOIYE – KAZI MBOVU uk17-22, #JIACTIVATE uk 23,

  CELEB- BOIYE na Ronald Tonui uk 24-25, MARIA KIM 26-31 na tips za kusomea final exam uk 32.
- CHAPTA 93: picha ya Phy Ngetich uk1, MARIA KIM uk 2-7, CELEB – Phy Ngetich uk 8-9, MALKIA uk 10-15, matangazo uk 16, MARIA KIM uk17-22, CHARLIE PELE uk 23-29, BOIYE- #LIGISAFI uk 30, BOIYE – ENKAUNTA CHALLEGE uk 31 na MCHONGOANO NA UJINGA NI?

  uk 32.
- CHAPTA 98: sura ina picha ya msanii GOVI uk 1, CHARLIE PELE uk 2- 7, MALKIA uk8-9, MARIA KIM uk 10-15, tawasifu ya GOVI uk 16, BOIYE -#LIGISAFI uk 17, JANTA CHALLENGE uk 18, TOUCH DOH uk 19-21 na JIACTIVATE uk 22, MARIA KIM uk 23-25 na uk 26-31. Kisha

  matangazo uk 32.
- CHAPTA 102: uk 1 kuna picha ya msanii CHEBET, uk2-7 MARIA KIM- Chuxx ameharibu hewa, uk 8-9 tawasifu ya Chebet, uk 10-11, MALKIA - #BAEMILELE, uk 12-17 MALKIA- Closing Mula Challenge, uk 18- 24


BOIYE – Meet The Stars!, HUSTLE of the MONTH – BOIYE na Joseph Kimani uk 25, MARIA KIM – Kisu Tunayo Ama Hatuna uk26-31 na matangazo katika uk 32.

Sehemu ya kwanza huchukua katika matoleo mengi huanza uk 2-7, kama ilivyo katika CHAPTA 68, 78, 88, 93, 98 na katika matoleo mengine.  Lakini kuna matoleo ambayo ukurasa wa pili huwa na matangazo kama katika CHAPTA 57. Matoleo mengina ya ukurasa wa pili au wa tatu ukiwa kama sehemu ya yaliyomo au matangazo. Kwa mfano katika CHAPTA 27 na 33. Katika matoleo haya sehemu ya kwanza uanzia aidha uk 3- 8 au uk 4 au 5 – 8 au 10. Yaani hakuna mpangilo maalum kwamba sehemu ya kwanza lazima ianze baada ya jalada.

Kutokana na ushahidi huu ni wazi kuwa *Shujaaz* haina sura au maonyesho kama ilivyo katika riwaya na tamthilia bali huwa imegawanywa katika sehemu ambazo hutambulishwa na mhusika mkuu wa sehemu hizo na wahusika wakuu ni wanne; MARIA KIM, DJ BOIYE, MALKIA na CHARLIE PELE. Hata hivyo wahusika hawa wakuu vilevile huchukua nafasi kuu katika sehemu nyingine kama SHUJAA, CELEB, HUSTLE FITI, #BAEMILELE, #SistaSauti, JIACTIVATE,
#LIGISAFI, ART KORNA, HUSTLE of the MONTH n.k. kisha kuna sehemu za matangazo, SHENG DICTIONARY, MCHONGOANO, UJINGA NI? n.k. Shujaaz haina utaratibu maalum wa mfuatano wa sehemu hizi. Kila toleo huwa na mpangilio wake. Kila toleo laweza kuwa na sehemu 5, 6, au zaidi.

Jalada la kazi yoyote ya fasihi huwa ni sehemu muhimu ya muundo wa kazi husika kwani hutoa muhtasari wa maudhui na yanayotarajiwa ndani ya kazi husika. Kulingana na Peter M. and David
J. A. (2020) jalada la kitabu huwa na maana ya sitiara ya kuwa mzingile wa maandishi na daraja kati ya yaliyoandikwa na ulimwengu. Jalada hutimiza jukumu la kukipatia kitabu sura na pia huwa ni mwaliko wa kumuingiza msomaji katika ulimwengu wa uandishi wake uwe wa kubuni, wa kihistoria, wasifu, tawasifu na mengineyo. Jalada humkaribisha msomaji kujumuika katika yaliyomo kitabuni.

Jalada ikiwa ni sehemu ya juu ya kitabu (matini) inahusisha sehemu ya mbele na ya nyuma. Jalada la kitabu humpatia msomaji dhana ya yaliyomo kitabuni kwa kumdokezea dhamira na maudhui anayotarajia kitabuni. Vipengele vya jalada ya mbele hujumujsha: anwani ya kitabu/matini, jina la mwandishi, picha mbalimbali na rangi mbalimbali. Vipengele vya jalada ya nyuma huwa na: historia ya mwandishi, picha ya mwandishi na jina la wachapishaji. Ngugi (2017) anapoelezea kuhusu jalada la vitabu vya watoto anasema kuwa uhakiki wa kitabu cha watoto huanzia kwenye jalada. Jalada hubeba ujumbe kwa muhtasari wa hadithi iliyo ndani ya kitabu. Hivyo basi, ujumbe kwenye jalada unahitaji kuwa wenye mvuto. Katika fasihi ya watoto, vielelezo kwenye jalada huweza kuwa ndicho kigezo kinachompa mtoto motisha ya kusoma kitabu fulani. Ujalidi unahusu umbile la jalada na jinsi lilivyounganishwa na kurasa zingine. Ujalidi uliofanywa vizuri ni ule ulio imara ili kitabu kiweze kudumu kwa muda mrefu. Shujaaz haina jalada ambalo linasimamia matoleo yake yote. Jalada la *Shujaaz* hubadilika katika kila toleo. Hata anwani hubadilika katika matoleo mengine kutoka *WWW.SHUJAAZ FM* (mfano ukiwa kaitka CHAPTA 27, SPECIAL EDITION 01/3 na 03/03, 33 na 40) na *SHUJAAZ*




(mfano ukiwa katika CHAPTA 57, 68, 78, 88, 93, 98, 102 na 109)

. **Kielelezo cha 48 kutoka Special Edition 03/03 Jalada lenye anwani *www.shujaaz.fm***




**Kielelezo cha 49 Kutoka Chapta 68 Jalada lenye anwani *SHUJAAZ***




**Kielelezo cha 50 kutoka Chapta 109 Jalada**

Kila jalada lina jumbe tofauti. Kwa mfano, toleo la 109 (CHAPTA 109) kuna:

(i) Maelezo kuwa kitabu hiki si cha kuuzwa (NOT FOR SALE),

(ii) Anwani ya kitabu hiki - *SHUJAAZ.*

(iii) Kitabu ni toleo la ngapi (CHAPTA 109 au 110 n.k.),

(iv) Picha halisi ya mtu kwa jina DR. OFWENEKE na chini yake maneno- *nilianza comedy kwa church.*

(v) Kuna mchoro wa wanne ambao waononekana kupiga nduru kutokana na maneno – WAAAI! Yaliyo wazunguka na chini yake manano- *umepanga future yako aje? Cheki vituko pg12*

(vi) Kisha kuna picha ya msichana na chini yake tangazo la kuhimiza wasomaji kusikiliza Shujaaz Radio Show kila Saturday 1- 8 pm kwa Radio Maisha na Radio Jambo Sunday 8 – 9 pm.

(vii) Upande wa nyuma kuna picha ya mvulana na msichana na maneno yanayohimiza msomaji kujisajili kuwa mwanachama wa *Shujaaz*- REGESTER KUWA SHUJAAZ MEMBER DAIL *236#

(viii) Rangi zilizotumiwa upande wa mbele ni samawati nyuma ya kila yaliyomo, rangi nyekundu katika anwani huku anwani yenyewe ikiwa ya ranyi nyeupe na maeneo ya kupiga nduru, rangi ya **njano** kwenywe jina la DR. OFWENEKE na nyuma ya maneno – *Umepanga future yako aje? Cheki vituko pg12*

(ix) Upande wa nyuma kuna picha ya ukuta wa rangi ya kahawia huku neno REGISTER likiandikwa kwa rangi ya zambarau na neno KUWA rangi nyeupe na SHUJAAZ MEMBER! rangi nyekundu. Neno dail katika rangi nyeupe pamoja na * na # huku 236 yakiwa katika rangi ya samawati. Msichana amevaa brausi ya rangi ya chungwa na suruari ya samawati huku kujana akiwa amevaa sweta ya zambarau, shati nyekundu na suruali ya kijani kibichi.

Mfano wa pili ni katika toleo la CHAPTA 27 kuna:

(i) Maelezo kuhusu mchapishaji wa kitabu- *Well told story*

(ii) Maelezo kuwa kijitabu hiki haki si cha kuuzwa- *NOT FOR SALE*

(iii)Kuna anwani – www.Shujaaz.fm

(iv)Kuna anwani ndogo – KUJENGA MA- YOUTH

(v) Kuna maelezo ya hili ni toleo la ngapi- CHAPTA 27

(vi)Kuna picha ya kuchora ya msichana mwanafunzi wa shule kwani amevaa sare aliyeshika ngao na kuandamwa na maneno yafuatayo*: siri kwa madem, biz idea kali, orezo next ni nani? penzi moto moto!! na ongeza mavuno.*


(vii) Kuna mchoro wa radio na maneno TUNE IN!!

(viii) Kuna nembo ya facebook na maneno DJ Boyie chini yake, nembo ya tweeter na maneno @SHUJAAZ na nembo ya You Tube na maneno SHUJAAZ TV chini yake.

(ix)Kuna choro wa kiumbe kama binadamu ila kichwa chake ni fuvu lililodungwa kwa kalamu na maneno POVERTY kuoneka kutoka kwenye fuvu hili.

(x) Pembezoni chini upande wa kulia kuna tangazo la ushindi wa tuzo la INTERNATIONAL EMMY AWARDS.

(xi)Rangi iliyotumika upande wa mbele ni samawati kwenye anwani na kwenye sketi ya msichana, rangi nyekundu kwenyw ngao na nyuma ya nembo za anwani za mitandao ya kijamii, rangi ya kijani kibichi iliyochanagikana nay a kijani kibichi inayojitokeza kama mwangaza nyuma ya msichana na rangi ya kahawia iliyotumika nyuma ya anwani, kucholrea kiumbe ilicho na umbo la binadamu chenye fuvu lililodungwa na kalamu na katika radio. Rangi ya




machungwa imetumika kuandika CHAPTA 27.

**Kielelezo cha 51 kutoka Chapta 27 jalada**

(xii) Upande wa nyuma wa jalada kuna tangazo lililoandikwa kwa mchanganiko wa rangi ya kijani kibichi, nyekundu nay a machungwa – NI HOT. NI SEXY. NI NDIALALA….NI RADIO SHOW ITA-BLOW MIND YAKO!!! NI JONGO LOVE. FOLLOW #JONGOLOVE ON TWITTER NA FACEBOOK. STAY TUNED FOR MORE. STARRING CHUXX&GODPAPA MUSIC BY OCTOPIZZO.

(xiii) Nyuma ya haya maandishi kuna michoro ya rangi aina aina na pale juu upande wa kushoto kuna picha ya vipaza sauti. Sehemu ya chini kuna wavuti wa www.Shujaaz.fm na jina la mchapishaji – Well told Story.

Mfano wa tatu ni katika toleo la SPECIAL EDITION 03/03:




**Kielelezo cha 52 kutoka Special Edition 03/03 Jalada**

i. Kuna anwani www.Shujaaz.fm
ii. Kuna makataa ta kutouzwa – NOT FOR SALE
iii. Kuna mchoro wa vijana wanne wakiwa wameishikilia bendera ya taifa kana kwamba wanaisimamisha.
iv. Kuna nembo za mashirika ya PAMOJA na ya gtz
v. Pembezoni kupande wa kulia chini kuna maneno SPECIAL EDITION 03/03 na maandishi – wts:
vi. Rangi zilizotumika upande wa mbele ni samawati kuwakilisha mbingu, nyeupe kuwalikisha jua na kijani kibichi kuwakilisha nyasi. Kuna bendera ya nchi ya Kenya yenye marangi manne; nyeusi, nyeupe, nyekundu na kijani kibichi. Vile vile kuna rangi tofauti za mavazi ya wale vijana wanne
vii. Upande nyuma kijitabu kuna tangazo kuhusu – PEPEA! Games, kuna picha ya kuchorwa ya mkono umeshika shimu kuchukua picha ya magari. Tangazo hili nika kampuni ya Safaricom. Marangi yaliyotumika hapa ni

yale ya kampuni ya Safaricom; kijani kibichi, nyekundu na nyeupe. Simu tu ndiyo iliyo na rangi ya urujuani. Gari linalochukuliwa picha ni la rangi ya majano. Mikono ya mshika simu ni ya rangi ya kahawia.

Kutokana na mifano hii basi, ni muhimu kusema kuwa kila toleo la shujaaz ni toleo lililo na jalada lenye ujumbe tofauti kwa jumla hubainisha yafuatayo.

(i) Anwani zilizotumiwa katika jalada la kijitabu hiki zilibadilika kutoka *www.Shujaaz.fm*

(ii) na kuwa *Shujaaz.*

(iii) Kuna makataa ya kutouzwa kwa kijitabu hiki (NOT FOR SALE) kwa hivyo hupeanwa bure kupitia gazeti la *Saturday Nation* kila Jumamosi ya kwanza kila mwezi.

(iv) Kuna michoro ya watu au picha za watu halisi. Michoro ni ya katuni ya wat una vitu.

(v) Kuna maneno ambayo huenda yanahusu yaliyomo ndani mwa kitabu hiki

(vi) Kuna jina la wachapishaji ambao ni WELL TOLD STORY

(vii) Kuna matangazo tofauti katika kila toleo.

(viii) Kuna matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng

(ix) Kuna matumizi ya rangi tofauti tofauti katika kila toleo.

(x) Sehemu ya nyuma inatumiwa kutoa tangazo. Kila toleo likiwa na tangazo tofauti.

(xi) Kila toleo huwa ni CHAPTA inayofuata CHAPTA iliyotangulia.

(xii) Mbali ya matoleo ya kawaida ya CHAPTA kuna matoleo ya SPECIAL EDITION ambayo hayapo katika mfuatano wa CHAPTA

Kimsingi ni dhahiri kuwa *Shujaaz* haina mpangilio maalum kama ilivyo katika tanzu nyingine za fasihi andishi ambazo huwa na sura au sehemu ambazo zinafuata na kwa mpangilio maalum. *Shujaaz* ni kama mashairi huru ambayo ni mashairi lakini kila shairi laweza kuwa na muundo lake tofauti. *Shujaaz* inaendeleza dhana ya kuporomoka kwa masafa na kaida za utunzi na kuendeleza dhana ya uhuru wa utunzi kama nadharia ya metausasa inavyopendekeza.

b) **Wahusika:**

Njogu na Chimerah (1999), wanaeleza kuwa, wahusika ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Mazingira haya yaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Wahusika hujadiliwa kwa namna wanavyoingiliana na dhamira na hili hujitokeza kutokana na maneno, tabia na matendo yao, yaani kulingana na hulka yao. Wahusika ni watu, vitu ama viumbe waliokusudiwa kubeba dhamira mbalimbali kwa lengo la kuwakilisha tabia za watu katika kazi ya fasihi. Wamitila (2008), wahusika ni muhimu katika kuyakuza na kuyanendeleza maudhui. Matendo ya wahusika, mitazamo yao, mwonoulimwengu wao na maingiliano yao ni msingi muhimu wa maudhui yenyewe. Wahusika ndio hutumiwa kujenga matendo na matukio yanayopatikana katika kazi yoyote ya kifasihi. Jinsi wahusika wanavyosawiriwa, wasifu wa tabia, lugha wanazopewa, itikadi yao na labda hata mwonoulimwengu wao huathiriwa kwa kiasi kikubwa na dhamira na maudhui yanayohuskia.

Ntarangwi (2004), akipanua dhana hii anasema kwamba wahusika ni viumbe hai au visivyo hai ambavyo vinawakilisha watendaji halisi katika maisha ya kila siku ya jamii husika katika kuonyesha wasifu wa ndani na nje kama vile hali ya kusononeka mhusika, furaha au tabia fulani katika jamii inayotuzunguka. Hivyo wahusika huelezea hali halisi ya maisha ya jamii. Iwe mitaani, iwe sehemu za kazi, iwe shuleni na kwingineko ambako kunahusisha mikusanyiko ya watu wa tabia tofauti tofauti. Husaidia katika kuendeleza mada nzima anayoizingatia msanii kwa kufululiza vitushi na visa mbali mbali katika kazi ya msanii ili kuwafikia wasomaji au wasikilizaji wake. Mhusika hupewa maneno, dhana, na hulka ambazo ni muhimu katika kujenga hadithi, dhamira, na maudhui ya kazi ile. Wahusika wanakusudiwa kutenda matendo, tabia au matukio halisi katika mazingira halisi.

Wamitila (2002), wahusika katika kazi za fasihi ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni binaadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika huweza kutambulishwa pia na maelezo ya mhusika au msimulizi, msingi wa hisia, hali ya kimaadili, mazungumzo na matendo ya wahusika ndio kiini cha motisha au uhamasishaji wa wahusika

Mlaga (2017), anaeleza kuwa wahusika wamegawika katika makundi makuu mawili ambayo ni

wahusika wakuu na wahusika wasaidizi. Wahusika wakuu ni wale aanaobebe dhamira kuu katika kazi ya fasihi. Hawa ndiyo vipaza sauti vya mwandishi. Wahusika hawa huonekana kuanzia mwanzo wa hadithi hadi mwisho wake. Wahusika wadogo au wasaidizi ni wale ambao wanajitokeza hapa na pale katika kazi ya fasihi ili kukamilisha ulimwengu wa kazi hiyo. Wahusika hawa hutumiwa na mwandishi katika kukuza dhamira.

Kama kazi nyingine za fasihi, *Shujaaz* inawahuska wakuu, wasaidizi au wahusika wajenzi. Kwa mfano wahusika wakuu waliopo ni: CHARLIE PELE, DJ BOYIE, MARKIA na MARIA KIM.

i) **CHARLIE PELE** –

Sehemu hii huhusu mhusika CHARLIE PELE mpenda mpira wa kandanda na mandhari huwa mashambani. Matukio hutegemea mada zinazohusu maisha ya mashambani. Mhusika mkuu hapa huwa CHARLIE PELE. Katika CHAPTA 102, uk 20, tunaelezwa kuwa yeye alipoteza mama mzazi wakati wa vita vya kikabila baada ya uchaguzi, na amebaki na ndugu yake na babake mzazi, ni musika mcheshi anayependa kuchekesha watu sana bali na kuwa na ndoto za kuwa mchezaji mpira hodari katika ligi. Wahusika wake wasaidizi hubadilika katika kila toleo. Kwa mfano katika CHAPTA 98, uk 2-7, yeye na ROSIE ni wahusika wakuu wakisaidiwa na UNCLE ROSIE. Katika CHAPTA 68, uk10-15, CHARLIE ni mhusika mwelekezi katika sehemu HUSTLA, palipo na tawasifu ya kijana mkulima hodari wa kilimo biashara kule Narok upande wa bonde la ufa kijana Joseph Barasa. Joseph ndiye mhusika mkuu hapa na anajitokeza kama mhusika picha kwani picha zake halisi ndizo zimetumika wakizungumza na mhuika wa kuchorwa CHARLIE.



Katika CHAPTA 33, uk23-27, CHARLIE, ndiye mhusika mkuu akisaidiwa na mhusika JOHANA. Mhusika huyu ametumiwa katika sehemu zifuatazo kuendeleza maudhui tofauti:

- SPECIAL EDITION 01/03:uk 10-12, maudhui ya kupiga vita matamshi ya chuki baina ya makabila tofauti. Uk 16, tangazo kuhusu sakata ball.
- SEPECIAL EDITION 03/03: uk10-12, maudhui ya matamshi ya chuki ya kikabila.
- CHAPTA 27:uk 25-30, maudhui ya kilimo; matumizi ya mbegu zifaazo.
- CHAPTA 33: uk 9, aitisha msamiati wa kijumuishwa kwenye kamusi ya Sheng (SHENG DICTIONARY) na pia tangazo kuhusu njia mpya ya kujua kuhusu ufugaji wa ngombe kupitia ICOW ambayo ni huduma kupitia ujumbe mfupi wa simu. Uk 29, MCHONGOANO NA UJINGA NI?
- CHAPTA 40:uk 16 na uk23-28, maudhui ya chakula poa, afya poa. Uk 24, SHENG DICTIONARY
- CHAPTA 57: uk 19-24, maudhui ya uwajibikaji.
- CHAPTA 68: uk 10-15, maudhui ya kilimo biashara.
- CHAPTA 78: Hajahusishwa.
- CHAPTA 88: Hajahusishwa
- CHAPTA 93: uk 23-29, maudhui ya majiukumu ya wawakilishi katika mbunge la eneo gatuzi; MCA
- CHAPTA 98: uk 2-7, maudhui kuhusu kusuluhusha suala la gharama ya Maisha.
- CHAPTA 102: uk 20, tawasifu yake
- CHAPTA 109: Hajahusishwa.

Ni dhahiri kuwa CHARLIE PELE hajatumiwa kama mhusika katika matoleo yote. Hata hivyo mwandishi amemtumia kuonyesha nafasi ya vijana katika kusuluhisha matatizo yanayoikumba jamii yawe ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ametumiwa kuhumiza vijana kuwa katika mstari wa mbele kuleta amani kati ya makabila tofauti nchini kupitia michezo kama michuano ya mechi za kandanda baina ya makabila tofauti yanayoishi pamoja, kukoma kulalamikia hali ngumu ya maisha kwa kuchukua

hatua ya kutafuta suluhu kwa kuwajibika na kujiingiza katika biashara na kilimobiashara ili kuimalisha maisha yao na ya jamiikwa jumla.

ii) **MARIA KIM**

Sehemu hii mhusika mkuu ni MARIA KIM. Kulingana na maelezo katika CHAPTA 102 uk 21, tunalezwa na DJ BOIYE kuwa MARIA KIM ni mkazi wa mtaa wa JONGO na wanafunzi katika JONGO HIGH SCHOOL Akiwa shuleni ni mwanafunzi anayewasaidia wanafunzi wenzake kujielewa na kutatua shida zao kw ani amejibeba na heshima na anathamini kujituma na kufanya kazi kwa bidii. Akiwamtaani yeye ni msichana anayejielewa na kuelewa jamii yake hasa Maisha ya sehemu ya mabandani. Wahusika wake wasaidizi hubadilika takika kila toleo lakini walijitokeza sana ni ndugu yake BRYO, rafiki yake KJ, na kijana anayemtaka lakini yeye MARIA hamtaki CHUXX.

Mhusika huyu MARIA KIM ametumiwa katika sehemu zifuatazo kuendeleza maudhui tofauti:

- SPECIAL EDITION 01/03:uk 13-16, kuifahamu katiba ya nchi
- SEPECIAL EDITION 03/03: uk – 13-15, upigaji kura
- CHAPTA 27:uk 18-23, Maisha ya 'ghetto' (sehemu za mabanda mjini)
- CHAPTA 33: uk10-15, utafutaji wa huduma ya afya ifaayo, uk 16, kujua juu ya bajeti ya nchi, uk 17-18, nafasi ya vijana kushiriki na kung'ang'ania kuchaguliwa katika uchaguzi nchini
- CHAPTA 40: MARIA KIM hakuhusishwa
- CHAPTA 57: uk 10- 15, changemoto za mahusiano ya mapenzi miongoni mwa vijana,
- CHAPTA 68: uk 18-23, vituko vya maapenzi baina ya vijana mtaani,
- CHAPTA 78: uk 18-23, athari wa vijana wanaopinga utimizi wa mipira ya kionana kimwili katika mahusiano yao ya kimapenzi.
- CHAPTA 88: uk 9-14, huduma za mashauri na maelekezo kuhusu mahusiano ya kimapenzi miongoni mwa vijana. Uk 26-31, kufaulu kwa vijana

wanaojituma- PROFYAM.

- CHAPTA 93: uk 2-7, kasumba potovu kuhusu matumizi ya kinga ya mipira ya kuonana kimwili wakati wa ngono miongoni mwa vijana. Uk17-22, biashara ya ukulima ya uyoga.
- CHAPTA 98: uk 10-15, changamoto za mahusiano ya mapenzi shuleni hasa kutokana na umuhimu wa vijana kutafuta ushauri kwa wahudumu waliohitimu kama wale wa shirika la FUTURE FAB. Uk 23-24, sifa za vijana ambao ni kielelezo bora katika Maisha ya vijana wenzao. Uk 25-31 kutokana na uwajibikaji wao katika suara la kujikinga wakati wa kuingiliana kingono kwa kutumia mbinu tofauti zilizopo na umuhimu wa kupata huduma katika kliniki za FUTURE FAB na TSAFE
- CHAPTA 102: uk2-7, uaminifu katika biashara. Uk 26-31, nafasi ya utamaduni katika Maisha ya vijana - ada ya tahara kwa vijana
- CHAPTA 109: uk 4-9, maudhui ya mapenzi shuleni, uk 10-12, maudhui ya ushauri kwa wapendanao.



**Kielelezo cha 54 kutoka Chapta 102 uk 21**

Umuhimu wake ni kuwa mwandishi ametumiwa kuhimiza wanajamii kuwa wanapokuwa wagonjwa watafute huduma za afya katika vituo vya afya vya serikali au vile vilivyoidhinishwa na serikali. Ametumiwa kuonya wanajamii wajiepushe kuingia vichochoroni kutafuta huduma huko kwani huko kuna hatari ya kudhurika zaidi au hata kupoteza maisha. Amatumiwa kushauri vijana kuwa ni muhimu wakubali kutumia njia za kujikinga wanapoingiliana kimapezi ili kujiepusha na matatizo ya mimba kabla ya ndoa, magomjwa na matatizo ya kukwamisha maisha yao. Ametumiwa na mwandishi kama kielezezo cha vijana wanapenda kudumisha amani wakati wa uchaguzi na wanaowashauri vijana waepukane na kukubali kuchochewa na viongozi wabaya wasipenda amani.

iii) **DJ BOYIE**

Sehemu hii inahusu mhusika DJ Boyie. Ni kijana msanii wa mtaani. Yeye ni mhusika mkuu katika sehemu zote za BOIYE, na hujitokeza katika kila toleo. Yeye huchukua nafasi katika matukio tofauti katika Shujaaz mbali na ile sehemu ya BOIYE. Yeye yuko katika HUSTLE FITI anapo hoji vijana walifanikiwa katika kuanzisha biashara ndogo mtaani na kisha vikafaulu kwa mfano toleo la 109, uk 1-3 anapozungumza na mhusika wa picha halisi NICK ambaye anafanya biashara ya upishi. BOIYE pia anashiriki katika sehemu za SHUJAA katika toleo 57 uk 3-8, anapozungumza na mhusika mwingine wa picha halisi kwa jina Dalton Wycliffe Odhiambo. Dalton ni shujaa aliyejitolea na wenzake kuzoa takataka katika endeo la Kibera bila malipo. Ameshiriki pia katika sehemu za CELEB kufanikisha tawasifu za vijana mashuhuri kama ilivyo katika CHAPTA 68, uk16-17, 57 uk16-17, 109 uk21-23 n.k.

Wahusika wake wasaidizi hutofautiana katika kila toleo. Kwa mfano katika CHAPTA 40, uk 5-10, wahusika wasaidizi ni DEEPTI na rafikiye msanii. Katika SPECIAL EDITION 01/03 uk 2-4 wahusika wasaidizi wakiwa ni vijana wenzake katika mtaa wake.



**Kielelezo cha 55 kutoka Chapta 102 uk 24**

Mhusika huyu ametumiwa katika sehemu zifuatazo kuendeleza maudhui tofauti:

- SPECIAL EDITION 01/03: uk 2-4, maudhui ya umuhimu wa vijana kusoma katiba, uk 8-9, maudhui ya umuhimu wa kuelewa katiba ya nchi kwa vijana
- SEPECIAL EDITION 03/03: uk 2-4, jinsi ya kuepusha vita wakati wa uchaguzi, uk 8-9, majukumu ya tume ya wataalam wa katiba ya nchini
- CHAPTA 27:uk 3 tangazo kuhusu Shujaaz fm, uk4-9 changamoto ya uuzaji na ununuzi wa kura kabla ya uchanguzi. Uk 31, SHENG DICTIONARY, MCHONGOANO na UJINGA NI?
- CHAPTA 33: uk 3-9, vijana wa pwani kupanga kutopiga kura, uk 20-21, ART KORNA- ukuzaji wa kipawa cha uchoraji,
- CHAPTA 40: uk5-10, ukuzaji wa talanta miongoni mwa vijana, uk 12-17, uwajibikaji katika kubadili Maisha ya mtu binafsi na jamii kwa jumla, uk 22-
    - 23. ART KORNA, hatua za kuanda vibonzo na ukuzaji wa Sanaa ya uchoraji nchini.
- CHAPTA 57: uk 3-9, kujitolea mhanga kwa vijana kudumisha usafi wa mazingira katika makazi yetu, uk 16-17, tawasifu ya msanii wa Jamaica, Alaine. Uk 18, kutafuta watu wanaofanana kisura, uk 25, majina ya mtaani ambayo huwarejelea polisi katika sehemu tofauti nchini
- CHAPTA 68: uk 16-17, tawasifu ya msanii Victoria Kimani,
- CHAPTA 78: uk2-7, ukuzaji taalanta ya uimbaji mingoni mwa vijana. uk 8- 9, tawasifu ya Liz Marami nahodha mashua baharini.
- CHAPTA 88: uk15-16, sifa za mwanamke bora wa kuoa. Uk 17-22, huduma ya OMBUDSMAN ya kuripotiwa wafanyi kazi watepetevu kazini., uk 23, # JIACTIVATE- uzinduzi wa vijana wapige vita ufisadi, kupigania kupewa kazi, afya bora na shibe., uk 24-25, tawasifu ya mpiga picha mashuhuri kutoka Kericho, Ronald Tonui.
- CHAPTA 93: uk 30, majukumu ya viongozi katika maeneo gatuzi, uk 31, tangazo kwa wasomaji,

- CHAPTA 98:uk katika #LIGISAFI- uchapaji kazi wa viongozi. Uk 18, JANTA CHALLENGE, mbinu ya kuchunguza utenda kazi wa wakilishi wadi katika maeneo gatuzi. Uk 15-17, TOUCH DOH- mbinu mpya ya vijana kujipatia pesa. Uk 22, JIACTIVATE- mbinu mpya za kufanya vingozi kutenga wakati wa kusikiliza vijana na kutatua shida zao.
- CHAPTA 102: uk8-9, tawasifu ya Esther Chebet Mwigizaji mashuhuri kutoka Nyahururu. Uk 18, maoni kutoka kwa wasomaji na kaziwanazofanya kijiinua kiuchumi. Uk 19-24, tawasifu fupi za wahusika, CHARLIE PELE, MARIA KIM, MALKIA na DEEPTI DIVANI. Uk 23, kazi ya mwekezaji wa kilimo Joseph Kimani. Uk31, kushrerehekea waliojishindia zawadi kwa kutoa maoni yao.
- CHAPTA 109: uk2-3, maudhui ya biashara ya vijana mtaani, uk 21-22, tawasifu ya Dr. Ofweneke

Mwandishi amemtumia DJ BOIYE kuwashauri vijana katika masuala mengi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Anajitokeza kama kijana anyejielewa na kiongozi wa vijana na maudhui ya uongozi anayaendeleza vizuri. Mwandishi pia amemtumia kama nguzo ya kazi hii ya *Shujaaz* kwani ametumika zaidi ya wahusika wengine hata katika kutoa matangazo yanayohusu *Shujaaz* (CHAPTA 78 uk 24, CHAPTA 109, uk 23 na 24 n.k), kueleza kuhusu mambo muhimu katika jamii (SPECIAL EDITION 01/03 uk8-9).

iv) **MALKIA**

Huyu ndiye mhusika mkuu katika sehemu za MALKIA. Kulingana na maelezoya DJ BOIYE katika CHAPTA 102, MALKIA ni mtoto wa kipekee wa BEATRICE ambaye hakuolewa na ni mfanya biashara. Ameingila biashara yake jkiasi cha kumsahau bintiye. Ni mwanafunzi mcheshi na anayependa kuwashauri wanafunzi wenzake kujikakamua kutimiza ndoto zao maishani. Mtaani ni mscichana anayelekea kujielewa na yuko tayari kilawakati kuwasaidia wenzake mtaani wanapojikuta katika changamoto za kimapenzi. Wahusika wake wasaidizi ni wanafunzi wenzake na rafikize mataani.

Mhusika huyu ametumiwa katika sehemu zifuatazo kuendeleza maudhui tofauti:

- SPECIAL EDITION 01/03: uk 5-7, maudhui ya majukumu ya baraza la viranja shuleni,
- SEPECIAL EDITION 03/03: uk 5-7, uchaguzi wa baraza la viranja shuleni
- CHAPTA 27: uk 10-15, uchumi wan chi yetu,
- CHAPTA 33: uk 29-30, kawi mbadala ya 'BIOGAS'
- CHAPTA 40: uk 18-19 faida za BIOGAS kwa jamii. Uk 24, MCHONGOWANO na UJINGA NI?
- CHAPTA 57: uk 26-31, swala la ngono kabla ya ndoa miongoni mwa vijana,
- CHAPTA 68: uk 2-7, kusaidiana wakati wa shida miongoni mwa vijana,
- CHAPTA 78: uk 10-15, changamoto za utumiagi kinga wakati wa ngono miongoni mwa vijana.
- CHAPTA 88: uk 2-7, tamasha za michezo ya kuigiza Shuleni,
- CHAPTA 93: uk 10-15, vijana kujihusisha na uundaji wa bageti za maeneo gatuzi yao ili maslahi yao yajumuishwe.
- CHAPTA 98: uk 8-9, ushauri kwa vijana wapenzi wasiojua mbinu mbora za kujikinga wanapotaka kingiliana kingono.
- CHAPTA 102:uk 10-11, changamoto ya vijana wapenzi kukosana kutokana na mitazamo yao tofauti kuhusu kutumia mbinu za kujikinga wakati wa kufanya ngono. Uk 12-17, umuhimu na faida ya kijiwekea akiba ya chochote kidogo upatacho hata ukiwa mwanafunzi.
- CHAPTA 109: uk 13-17, maudhui ya kutowajibika katika mahusiano ya kimapenzi na uk19-20, maudhui ya mbinu za kutumia kuzuia ujauzito na magonjwa katika mapenzi

Umuhimu wa MALKIA katika *Shujaaz* ni kuwa mwandishi amemtumia kuonyesha maisha ya wasichana katika sehemu za mijini na changamoto wanazokumbana nazo kabla ya kuolewa. Ametumiwa kama kilelezo kinachohusu changamoto za vijana walio katika mahusiano ya kimapenzi. Ametumiwa na mwandishi kama kielelezo cha matatizo ya kiuchumi ya kupanda kwa gharama ya maisha ambapo anawahimiza wanajamii

kuhakikisha wameshirikishwa na vingozi katika mipango ya kuandaa makadirio ya matumizi ya pesa zilizotengewa maeneo yao ili maslahi ya vijana yaweze kuhusishwa na kupewa makadirio yake. Vilevile, ametumiwa kuhamashisha jamii kuhusu kawi mbadala ya 'BIO GAS' ambayo gharama yake ni ya chini. Gharama ya kutengeneza mtambo ni ya chini na pia ile ya kuudumisha. Faida yake ni kubwa hasa katika kutunza mazingira na afya ya watumiaji. Umuhimu wake unategemea toleo husika na maudhui ambayo ametumiwa kuwasilisha.




**Kielelezo**

*Shujaaz* vilevile inahusisha wahusika wa kuchorwa kama vibonzo au katuni. *Shujaaz* inakidhi sifa za kuitwa kitabu cha katuni au vibonzo kwani sehemu yake kubwa inawahusika

waliochorwa na mandhari ya kuchorwa pia. Hata mazungumzo kati ya wahusika yamefungiwa katika vibofu vya maneno kama ilivyo katika vitabu vya katuni. Wahukiska wote wakuu na wengi wa washika wanao ingiliana nao katika matukio wamechorwa.

Kulingana na Kimani (2006), vibonzo hujitokeza katika michoro, picha au vielelezo na huwa ni maumbo ya kuchekesha. Otuoma (2012) anasema kwamba kuna aina tatu za vibonzo; vibonzo vya michoro, vibonzo vya filamu na vibonzo vya paneli. *Shujaaz* ni aina ya vibonzo vya paneli. Na vibonzo vya paneli kulingana na Lordan (2006) na Otuoma (2012) huwa kwenye paneli moja ili kuweza kutoa hadithi fulani inayosisimua, lakini kwa mtazamo wa yanayofanyika katika jamii kila uchao. Kila mara huwa na kinachochochea wasomaji wake chini ya paneli hiyo.

Hata hivyo, mwandishi wa *Shujaaz* ametumia wahusika picha za watu halisi kama ilivyo katika fotonovela. Kulingana na www.encyclopedia.com, fotonovela ni machapisho yanayotumia picha za watu halisi kusimulia hadithi. Kaika *Shujaaz*, wahusika wengine wa picha ni vijana halisi mashuhuri katika nchi ya Kenya hasaa wasanii na mashujaa waliofanikiwa katika taaluma fulani japo wangali vijana. Kuna wahusika wa picha halisi za vijana halisi waliofanikiwa katika biashara na katika kilimo biashara. Wahusika wa picha halisi katika matoleo 13 yaliyoteuliwa ni:

- CHAPTA 27:uk 20-23, kuna picha ya mwanafunzi na dadake
- CHAPTA 33: uk 15, picha ya Henry Volunteer wa Amua Family Planning Clinic. Uk 16-17, picha za hadhira: Ibrahim Abubakar Yusuf na Mellaquer Lumabele.
- CHAPTA 40: uk 12-17, picha za Martha Chiaga mkazi wa Landi Mawe Nairobi. Uk 13, picha ya watoto wakihoji kuhusu BIOGAS.
- CHAPTA 57:uk1, picha ya Alaine na ua Bw. Odhiambo, uk 3-8, picha za Dalton Wycliffe Odhiambo mkaaji wa Kibera Nairobi, uk12, picha ya Victor Okello Oloo mkaaji wa Kibera, uk 16-17, picha za ALAINE, msanii mwanamziki kutoka Kingstone Jamaica, uk 19-24, picha za Irene Mwihaki mkaaji wa Sotik Bomet., uk 26, kuna picha ya Dennis Odhiambo

mkaaji wa Nyakach Kisumu ni Kinyozi.

- CHAPTA 68:uk 8-9, picha ya Paul Kuhuha aka Protisa fundi wa vitu vya chuma, uk 10-15, picha za mkulima wa viazi Joseph Barasa mkaaji wa Narok, uk 16, Picha ya Msanii mwanamziki Victoria Kimani, uk 24, picha ya msanii mwigizaji Vera mkaaji wa Nairobi
- CHAPTA 78:uk 1na 8, picha ya Liz Marami nahodha wa mashua. uk 16-17, picha za msanii mwimbaji Holy Boy kutoka Meru
- CHAPTA 88: uk 1 na uk24-25, picha ya mpiga picha mashuhuri Ronald Tunoi kutoka Kericho. uk 22, picha ya James Muchiri na jamaa zake pale Naivasha
- CHAPTA 93: uk 1 na uk 8-9, picha za msanii maarufu mwanamziki Phy Ngetich kutoka Sotik.
- CHAPTA 98: uk 1 na uk 16, picha ya msanii mwigizaji kijana Govi au Lemuel King Malik.
- CHAPTA 102:uk 1 na uk 8-9, picha za Esther Chebet msanii mwigizaji mashuhuri na mkaaji wa Nyahururu. uk 25, picha ya Joseph Kimani, kijana mfanya biashara ya kilimo biashara- AGRIPRENUER. Uk 31, picha za wasomaji waliotoa maoni yao na kupata zawadi, Will Mburu, Maggy Murugi, Dennis Nduru, Danson Daniel, Shaniz Wanjiru na Moses Macharia. Hawa ni wahusika hadhira na wameshirikishwa na mwandishi kuendeleza maudhui ya maendeleo ya kiuchumi kupitia biashara.
- CHAPTA 109:uk 1na 21-22, picha ya msanii Mnaigeria mchekeshaji Dr.

  Ofweneke. uk 2-7, kuna picha za kijana mpishi hodari Nick.

Mwandishi wa *Shujaaz* amefanikisha kazi yake kwa husisha dhana ya upataniasho na ushirikiano katika matumizi ya sanaa tatu tofauti; sana ya kutumia maneno, sanaa ya uchoraji na sanaa ya picha katika kazi moja. Ameafulu kuondoa mipaka ya kimatumizi ya sanaa hizi tofauti na akafaulu kuunda kazi moja ya *Shujaaz*.

Mwandishi wa *Shujaaz* vilevile hakukomea hapo bali ametumia teknolojia katika kuiboresha

kazi yake. Teknolojia katika *Shujaaz* imetumiwa kuhusisha hadhira yake kama wahusika. Mwandishi amefanya hivi kwa kuhusisha hadhira kupitia teknolojia ya simu kwa kutumia jumbe fupi zisizo malipo kupitia numbari 20308. Nafasi hii hutokea katika mwisho mwa baadhi ya sehemu inayohusisha wahusika wakuu. Kwa mfano katika CHAPTA 57 uk 9 mwisho wa sehemu ya BOIYE. BOIYE anasema ''MSEE KAA UNA SWALIMOTO KAMA EVECNA UNA–NEED ANSWERS. NITUMIE KWA 20308 UKIANZA NA WORD 'MOTO' NITASHUGHULIKIA
UJIBIWE''. Maoni ya wahadhira wamechapishwa katika baadhi ya matoleo mkama ilivyo katika CHAPTA 27, uk16-17, CHAPTA 57 uk 9, CHAPTA 102 uk 18, Vilevile kuna machapisho wa mazungumzo ya moja kwa kwa moja kati ya wahuska wakuu na hadhira yao. Dhana ya kuporomoka kwa masafa kati ya wahusika na hadhira yao na baina ya hadhira inayoshirikishwa ni jambo linalodhihirika kama inavyopenekezwa na nadharia ya metausasa.

c) **Mtindo**


Mwandishi wa *Shujaaz* ameipa kazi yake sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo huenda msanii mwingine asingeweza kuipa. Hata kama mambo anayorejelewa ni yale yamerejelewa na wasanii wengine kazi hii ina utofauti kifani na kimaudhui . Maelezo haya yanalandana na yale ya Mulokozi (1989) anayeeleza kuwa mtindo ni tabia ya utungaji ambayo hupambanua mtunzi mmoja na mwingine. Mtindo hubadilika katika namna mtunzi anavyotumia maneno yake, kama vile kutumia maneno magumu au rahisi, kuchanganya lugha, kutumia methali, jinsi anavyozipanga semi zake, kutumia sentensi fupi fupi au ndefu, takriri na namna anavyoumba tungo zake.

Mwandishi wa *Shujaaz* ameiandika kazi yake kwa mtindo unaoibua sifa maalum za utunzi wake kupitia fani na maudhui yake kwa njia inayomtofautisha na waandishi wengine. Wamitila (2008) anaeleza kuwa mtindo wa mwandishi unaweza kubainishwa kwa kuchunguza vipengele vifuatavyo:

(i) Matumizi ya lugha: Je, lugha ni rahisi au ngumu, je, kuna matumizi ya maneno ya kiufundi? *Shujaaz* inatumia lugha rahisi kueleweka. Japo kwa wingi imetumia mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kingereza pamoja na Sheng. Usimulizi wake unaeleweka kwa urahisi. Lugha iliyotumika ni lugha sahili. Mtunzi hajatumia mafumbo au msamiati uliona maana fiche. Hata msamiati mgeni wa Sheng

uliotumika mtunzi ametenga sehemu ya kamusi ya sheng kueleza maana ya msaniati huo.

Katika dondoo hili ambalo ni mfano wa hali ya matumizi ya lugha yalivyo, ni dhahiri kuwa lugha inaeleweka moja kwa moja, na ni mchanganiko wa Kiswahili na Kingereza. Vilevile kuna matumizi ya kuhamisha na kubadilisha msimbo baina ya wanenaji.




**Kielelezo cha 57 Kutoka Chapta 12 uk 5**

(ii) Matumizi ya dayolojia: Je, ni kwa kiasi gani mtunzi ametumia dayolojia, ni kwa kiasi gani dayolojia husimulia hadithi? Kwa kutumia dondoo lililotumika katika a) hapa juu kutoka uk 5 wa CHAPTA 12, ni bayana kuwa usimulizi katika Shujaaz unatokea katika hali ya dayalojia baina ya wahusika. Huku kauli za wahusika zikiwa zimewekwa katika vipofu vya sauti. Hata hivyo kuna sehemu ambazo msimulizi ametoa maelezo ya kufafanua suala husika katika usimulizi. Kwa mfano, katika uk

30 katika CHAPTA 33. Mwandishi anatoa maelezo ya ziada kuhusiana na mada inayohusika na hata kumjumuisha msomaji katika mjadala kwa kumuuliza swali kuhusiana na mada hiyo ambayo hapa inahusu matumizi ya kawi mbadala ya Biogas badala ya kutumia kuni.

Suala la kuhamamsisha na kuelimisha wasomaji kuhusu uhifadhi wa mazingira limetiliwa mkazo huku takwimu zikitolea kuwa 90% ya wakenya hutumia kawi ya kuni. Huku kila mtumiaji wa kuni akitumia tani moja ya kuni kila mwaka. Juhudi hizi za uhifadhi wa mazingira zikiunga mkono juhudi za Marehemu mshindi wa Nobel Prize Mheshimiwa Wangari Mathai kuhusu uhifadhi wa mazingira alipoanzisha kikundi cha Green Belt Movement mwaka wa 1977. Nia wake ilikuwa kupanda miche milioni 51 ili kuboresha rotuba ya mchanga, kuhimiza matumizi ya kawi mbadala, kuzuia mmomonyoko wa udongo, kuhifadhi chemchemi za maji na kuboresha mtandao wa viumbe hai. *Shujaaz* inahimiza jambo hili kwa wanajamii ili kuboresha maisha na kuhifadhi mazingira.



(iii) Namna ya usimulizi: Je, anatumia nafsi ya kwanza, ya pili, ya tatu au nafsi mbalimbali zinazopishana katika usimulizi wake n.k. Katika Shujaaz nafsi iliyotumika hutegemea hali ya mazungumzo baina ya wahusika. Mhusika anapojizungumzia huwa anatumia nafsi ya kwanza lakini wanapozungumza na wengine nafsi iliyotumika hutegemea wanachozungumzia. Lakini inategemea hali ya mazungumzo




**Kielelezo cha 59 kutoka Chapta 68 uk 6**

(iv) Ukuaji wa wahusika: Kwa vipi mtunzi anawatambulisha wahusika na kwa vipi wanabadilika katika hadithi. Katika Shujaaz wahusika wakuu ni wanne ambao ni DJ BOIYE, MARIA KIM, CHARLIE PELE na MALKIA. Kila mmoja akiwa na wahusika wasaidizi wake tofauti ambao wanajitokeza katika matukio yao tofauti. Katika kila CHAPTA wahusika hawa wakuu wanasehemu zao. Wahusika hawa hawabadiliki ila wanachukua majukumu tofauti katika kila tukio wanalohusishwa. Kwa jumla kile sehemu wanayowasilisha huwa si mwendelezo wa tukio walilowasilisha katika toleo la awali.

(v) Hisia za mwandishi: Je, hisia zake zinaonekanaje katika hadithi? Je, anaonekana ni mwenye mapenzi, mwenye matumaini, kejeli n.k. Katika Shujaaz hisia

zinzodhihirika moja kwa moja nizile za wahusika. Huenda hisia za mtunzi zinajidhihirisha kupita wahusika wake. Mada inayozungumziwa na wahusika wake huweza kuibuia hisia tofauti kutegemea kinacho zungumziwa. Ikiwa ni mapenzi na mahaba hisia hizi zinadhihirika kutokana na vitendo vya wahusika na maneno yao. Ikiwa kunajambo linaloibua hasira vivyohivyo. Mfano na mhusika CHUXX anavyodhihirisha hisia za chuki katika uk wa 15 katika SPECIAL EDITION 01/03




**Kielelezo cha 60 kutoka SPECIAL EDITION 01/03 uk15**

(vi) Namna anavyopanga sura au matukio katika hadithi: Je, sura ni fupi au ndefu? Ni nyingi kiasi gani, zimepangwaje? Na kwa nini zimepangwa hivyo? Matoleo ya Shujaaz hayana sura bali yana matukio yaliyogawanywa baina ya wahusika wake wakuu. Kila mhusika akiwa na sehemu yake ambayo ametengewa katika toleo husika japo si lazima wahusika wote wapewe sehemu katika kila toleo. Kwa mfano toleo la CHAPTA 12, lina sehemu ya tangazo uk 2, sehemu ya DJ BOIYE (uk 3-12), sehemu ya MALKIA (uk13-15), sehemu ya DJ BOIYE (uk16-17), sehemu ya maoni ya wasomaji wa Shujaaz (uk 18-19), sehemu ya MARIA KIM (uk 20-22), sehemu ya CHARLIR PELE (uk 23- 25), sehemu ya maoni ya wasomaji (uk 26-28) kisha sehemu ya maswahi kwa wasomajiuk 30-32. Urefu wa sehemu hizi unatofautina.


Sehemu zenyewe si ndefu sana kwani katika toleo hili sehemu zinachukua kurasa mbili au tatu.

Katika CHAPTA 93, kuna sehemu ya MARIA KIM (uk 2-7), sehemu ya DJ BOIYE ya CELEB – Phy Ngetich (uk 8-9), sehemu ya MALKIA (10-15), sehemu ya tangazo (uk 16), sehemu ya MARIA KIM (uk17-22), sehemu ya CHARLIE PELE (uk23-29), sehemu ya DJ BOIYE (uk 30-31) kisha sehemu ya Mchongoano, Ujinga ni na kamusi ya Sheng uk32. Katika mfano huu idadi ya sehemu na urefu wa kila sehemu ni tofauti na ilivyo katika CHAPTA 12 pengine kutegemea mada na urefu wa matukio husika.

Katika CHAPTA 68, kuna sehemu ya MALKIA (uk2-7), sehemu ya SHUJAA WA MTAA! – Paul Kuhuha aka Protisa (uk 8-9), sehemu ya CHARLIE PELE ya HUSTLA (uk10-15), sehemu ya DJ BOIYE ya CELEB – Victoria Kimani (uk 16-17) sehemu ya MARIA KIM (uk 18-23) kisha sehemu ya tangazo uk24

Kutokana na mifano hii mitatau ni dhahiri kuwa kila toleo linaidadi tofauti ya sehemu na vilevile kuna sehemu ambazo zina idadi sawa ya kurasa na kuna sehemu ambazo ni za mhusika yuleyule lakini zina urefu tofauti. Mwandishi hajajifunga katika idadi mahususi ya sehemu na urefu wa sehemu hizo wala hajajifunga pia katika idadi mahususi ya kurasa za kila toleo. Amejiweka huru.

(vii) Tamathali za usemi: Je, mwandishi ametumia kwa kiasi gani tashbiha, sitiari, tashihisi au alama za uakifishaji? Kazi ya Shujaaz imeandikwa kwa lugha sahili hivi kwambamatumizi ya tamadhali za usemi ni haba. Kazi yote iletwawaliwa na matumizi ya kuchanganya msimbo wa Kiswahili na Kingereza au Sheng.




**Kielelezo cha 61 kutokaChapta 33 uk 6.**

(viii) Mandhari: Je, mandhari yaliyotumika ni halisi au ya kubuni? Mandhari katika Shujaaz yanajitokeza katika hali mbili. Kuna mandhari ya kubuni na kuna mandhari halisi. Katika sehemu zinazohusisha mhusika wa picha na yule wa kuchorwa mandhari huwa halisi. Kwa mfano katika CHAPTA 57, sehemu ya DJ BOIYE ya



SHUJAA, uk 3-8 mhusika wa picha ni mhusika halisi kwa jina Dalton Wycliffe Odhiambo na mahali tukio linatokea ni mahali halisi ambapo ni sehemu ya Kibera kwani picha halisi za sehemu hiyo zimetumika. Hali hii ipo katika ila toleo ambapo mwandishi amehusisha mhusika halisi kwa njia ya picha yake na mahali walipo kama ilivyo katika CHAPTA 68, uk10-15.


**kielelezo cha 62 kutoka Chapta 57 uk 8**

Vilevile kuna matumizi ya mandhari ya kubuni katika Shujaaz. mandhari ambayo yanahusu sehemu zote ambapo wahusika wote ni wakuchorwa na mahali walipo panawasilishwa kwa njia ya kuchorwa. Sehemu zote zisizo na picha za wahusika halisi na mahali halisi ni za kubuni. Matoleo yote yana sehemu hizi za kubuni na ndzo nyingi. Kwa mfano sehemu ya MARIA KIM katika CHAPTA 57, uk10-15




**Kielelezo cha 63 kutoka CHAPTA 57 uk 15**

(ix) Uteuzi wa msamiati: Je, ni kwa kiasi gani msamiati uliotumika unaleta mvuto kwa msomaji? Msamiati uliotumika katika Shujaaz ni msamiati wa kuvutia na wa kufanya kazi isomeke na kueleweka kwa urahisi kutokana na kuchanganywa kwa maneno ya Kiswahili na ya kiingereza. Msamiati wa Sheng ulitumia iwapo si wa Sheng wa kawaida umeelezwa katika kamusi ya Sheng




**Kielelezo cha 64 kutoka CHAPTA 33 uk 9**

d) **Mtindo wa lugha katika *Shujaaz***

Katika *Shujaaz* lugha, michoro na picha halisi zimetumika kuwasilisha fani na maudhui ya mtunzi. Kulingana na Wamitila (2003) mtunzi wa kazi ya fasihi kama alivyo mtunzi wa *Shujaaz*, huweza kutumia lugha kama nyenzo kuu ya kazi yake kwani bila lugha huenda ikawa vigumu kuwafikia wasomaji wake. Katika uchunguzi wa matumizi ya lugha, mambo ambayo huchunguzwa ni: tamathali za usemi, uteuzi na mpangilio wa maneno, sajili za lugha kutegemea mazingira na hali tofauti-tofauti, matumizi ya nahau na misemo mbalimbali. Mwandishi wa *Shujaaz* ametumia lugha, michoro na picha kuyaibua mawazo yake na kuonyesha ukomavu wake katika kazi husika. Ametumia lugha, michoro na picha kuyaelezea mambo mbali mbali yahusuyo jamii yake kwa njia ya ubunifu na usanii. Mambo haya matatu; lugha, michoro na picha, ndiyo mzizi wa kazi hii ya *Shujaaz* na bila haya huenda kuwepo kwa *Shujaaz* hakungewezekana kuwa kama ilivyo.

**(i) Sheng katika *Shujaaz***

Katika *Shujaaz*, lugha inayotawala katika matoleo yote ni Sheng. Kimsingi *Shujaaz* inawasilisha ujumbe wake kwa kutumia lugha ya vijana ya Sheng. Kiswahili sanifu na Kiingereza sanifu zimetumika hapa na pale hatika hali ya kuhamisha na kuchanganya msimbo. Sheng ni lugha ya vijana inayoundwa kwa kuchanganya maneno ya Kiingereza na Kiswahili. Pamela (2018) anasema kuwa kutokana na mtindo wa usanii wa hali ya juu wa *Sheng*, kijitabu cha *Shujaaz* kimekuwa maarufu sana miongoni mwa vijana. Vilevile, *Shujaaz* ni chombo mwafaka cha kuwasiliana na vijana mbalimbali. Hii ni kutokana na sababu kuwa vijana wanahitaji majukwaa mbalimbali ambayo yatawapa nafasi ya kuzungumzia, kuelewa na hata kuitikia kwa hali mbalimbali katika maisha yao hasa kuhusiana na hisia, migogoro, mihemuko na matatizo wanayokumbana nayo kwa njia iliyo wazi, kweli na ya jumla bila vitisho vyovyote kutoka kwa wanajamii. Matumizi ya *Sheng* katika kijitabu cha *Shujaaz* yameshamiri mazungumzo wa wahusika wote ndani ya kijitabu hiki katika matoleo yote yake. Ni lugha nyepesi au rahisi ambayo inanuiwa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa vijana. Sentensi ni fupi fupi.

Kwa mfano, katika CHAPTA 33, uk 3 kuna maneno ya DJ BOIYE akisema:

- 'MANZE WASEE NIMESTUKA NA ZILE MESSAGE MAYUTS WAMENITUMIA' (Wenzangu nimeshtuka kutokana na jumbe fupi

za simu ambazo nimetumiwa na vijana)

- 'INAKAA NI KAMA MAYUTS WENGI HAWATA-VOTE??'

  (Inaonekana vijana hawatapiga kura??)

- 'HII RISTO HAINIBAMBI. LAZIMA NIENDE COAST NICHEKI

  NIAJE' (Hili si jambo si sawa. Lazima niende sehemu ya pwani nichunguze kinachoendelea huko)

Ukiangalia mfano huu unaona kuwa lugha ni ya vijana ya Sheng ambao inachanganya Kiswahili na maneno ya mtaani na yale ya Kiingereza. Vile vile kuna hali ya kuhamisha na kuchanganya msimbo. Kwa mfano mhusika DEEPTI katika uk 3 anasema

- YES. THIS IS MY CHANCE TO MEET DJ B. (Hii ni nafasi yangu ya kukutana na DJ B)
- HELLO - …ATI UMESEMA BASI ITAONDOKA SAA NGAPI

Hali hii ya matumizi ya Sheng na kuhamisha na kuchanganya msimbo inajitikeza katika matoleo yote ya Shujaaz.

**(ii) Lugha ya michoro, picha na rangi**

Bakize (2014), anayesema kuwa matumizi ya picha au michoro huonyesha uhalisia wa jambo linalosimuliwa na linaloendelea. Anaendelea kusema kuwa michoro na picha husaidia kueleza zaidi kile kinachozungumziwa katika kazi husika kwani huwa na mahusiano ya moja kwa moja na kile anachokieleza mwandishi au mtunzi. Hii ndiyo sababu picha zote kwenye vitabu vya fasihi ya watoto zina rangi za kuvutia ili kuchochea hamu ya watoto, pia zinaeleweka kwa urahisi na hivyo huwa rahisi kwao kupata maana. Rangi na urahisi wa kueleweka pia hufanya watoto hawa kukumbuka mawazo makuu yanayoendelezwa katika kazi husika.

Lugha ya michoro na picha hutokea palipo na matumizi ya michoro katika uwasilishaji wa ujumbe. *Shujaaz* ni mfano wa kijitabu cha vibonzo kwani hutumia wahusika wa kuchorwa. Shujaaz pia huhusisha wahusika picha kama ilivyo katika vitabu vya fotonovela. Kwa mfano, katika CHAPTA 109, uk 2-3, mwandishi ametumia mhusika DJ BOIYE ambaye ni wa kuchorwa na mhuska NICK ambaye ni mhusika picha. Upatanisho

wa Sanaa hivi mbili zinafanikiwa kuleta uhalisia na uhai wa kazi yenyewe.




CS Scanned with CamScanner

Kutokana na matumizi ya wahusika hawa wawili; mmoja wa kuchorwa na mwingine picha inakuwa rahisi kuelewa wanayoyasema kwani maneno yao yanaambatana na yanayoonekana. Vitendo vyao vinaonekana.

Kulingana na Wills (2015) vielelezo vilivyotiwa rangi kama ilivyo katika *Shujaaz* ni muhimu na huchangia kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, iwapo rangi itatumika vizuri, basi huenda ikawafanya wasomaji kuwa na utashi wa kusoma na hivyo kukua kiakili. Pili, rangi angavu zinapotumiwa vizuri huwafanya wasomaji kujinasibisha na yale wanayosoma na mambo wanayoyaona katika ulimwengu halisi. Katika *Shujaaz* kuna matumizi ya rangi tofauti tofauti za kuvutia kama ilivyo katika uliotolewa hapo juu

katika uk 2-3 katika CHAPTA 109.

(iii) **Uteuzi wa msamiati**

Kipengele hiki kinachunguza ni kwa jinsi gani msamiati uliotumika unaleta mvuto kwa msomaji. Kama ilivyo katika fasihi nyingine za watoto/vijana, mtunzi wa *Shujaaz* ametumia maneno ambayo yanalenga kuwavutia vijana hivi kwamba wanapata nafasi ya kujitambulisha kwa lugha iliyotumia. Mwandishi wa *Shujaaz* ametumia misamiati mingi yao ikiwa ni Sheng ambayo ni lugha ya vijana. Amewaandalia hadi kamusi ya Sheng (Sheng Dictionary- CHAPTA 40 uk 24, CHAPTA 27, uk31 n.k.) kwa wale wangetatizika na msamiati mgeni wa Sheng.

Kwa mfano katika CHAPTA 27, uk 31:

LEMBE – MBELE
MA-OCAMPO – KARAU/POLISI FINJE – 50 BOB
PARAA – KOFIA/ NGEPA HAWARADI – DON'T
UNDERSTAND KAMTISH – EXAM LEAKAGE
ATAKUPANGA – YOU'LL GET PAID SANTURI – SONKO
MAZUNYE – KITU POA KALULU – MSEE MJINGA

Katika CHAPTA 33, uk 9:

BWEKS – TWO (MBILI)
ARV – FAKE LIQUOR (POMBE HARAMU) ASAP – HERE
(HAPA)
BINGI – DREADLOCKS (NYWELE ZA RASTA) OTERO –
FIRST BODY (KUWA CHAPCHAP) BANGAISHA – HUSTLE
(KUTAFUTA MAPATO) CHA MBELE – OVERSEAS/
ABROAD (NGAMBO) BUNDUZ – UP COUNTRY
(MASHAMBANI) BABA – FRIEND/PAL (RAFIKI)
BYTES – MONEY (PESA)

Mwandishi huenda amechagua msamiati wake pengine kujtokana hadhira anayoilenga. Kutokata na umri wa wahusika wake huenda hadhira yake kubwa ni vijana kama walivyo wahusika wake. Vijana wengi hutumia Sheng jinsi wahusika wake wanavyoitumia na misamiati wanayoitumia. Hivyo basi wasomaji vijana wataweza kujitambulisha na kazi ya Shujaaz kwani lugha na wahusika ni kufu yao. Matoleo yote

ya *Shujaaz* yanatumia Sheng kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa ambao ni vijana. Kuanzia anwani ya ambayo ni *Shujaaz* badala ya Shujaa kila mhusika katika kila toleo anatumia Sheng. Mwandishi hapa analeta dhana ya upatanisho ya nadharia ya meta usasa kwa kupatanisha fasihi na kazi ya isimu katika kazi moja. Yaani taaluma tofauti kuletwa pamoja kutimiza lengo moja. Hapa mhakiki hujiuliza ikiwa lughailiyotumiwa na mwandishi ni rahisi au ngumu na iwapo kuna matumizi ya maneno ya kiufundi au la? Katika Shujaaz lugha iliyotumiwa ni lugha ya vijana ya Sheng.

(iv) **Tamathali za semi**

Mtunzi wa Shujaaz kama walivyowatunzi wengine wa kazi za fasihi ameipamba kazi yake kwa ufundi wa kutumia tamathali za usemi katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Katika *Shujaaz,* mtunzi ametumia tamathali za usemi ambazo zinahusisha ukiushi ambapo fungu la maneno linatumiwa na mtunzi kwa maana iliyo tofauti na maana ya kimsingi ya neno hilo. Mtunzi wa Shujaaz anafanya hivi ili kutekeleza majukumu matatu makuu ya tamathali za usemi katika fasihi kama anavyoyafafanua Wamitila (2008). Majukumu haya ni:

- Kurembesha kile kinachozungumziwa na lugha hiyo ili kiwe na mvuto wa kisanaa.
- Kufafanua kinachohusishwa na tamathali maalum.
- Kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani.

Tamathali za usemi vilevile hutumiwa pia kuipamba kazi ya sanaa ya kifasihi kwa kuongeza utamu wa lugha kwa kutumia sitiari, tashbiha, takriri, tashihisi na tafsida, methali, misemo, taswira, nahau, lugha za kigeni na kadhalika. Lugha ya kitamathali ni nyenzo muhimu katika ujengaji na uimarishaji wa hisia.

Katika Shujaaaz, baadhi ya tamathali za usemi zilizotumika ni kama vile:

- **Kuchanganya na kuhamisha msimbo**

  Massamba (2004) anaelezea kuchanganya msimbo kama mbinu ya kifasihi ya kubadili lugha kwa kutumia aina mbili tofauti za lugha kwenye matini moja wakati wa mawasiliano. Anayewasilisha ujumbe anatumia lugha mbili au hata zaidi. Kwa mfano anaweza akaingiza neno la lugha fulani katika usemi. Kwa kawaida wanafasihi hutumia mbinu hii kama mtindo wa kipekee wa kuwasilisha ujumbe. Kuna wakati pia msimulizi anaweza akakosa njia mwafaka ya kuwasilisha hoja na akaamua kuchanganya lugha. Kulingana na Wamitila (2003), kuhamisha msimbo ni mbinu ya

kifasihi ambapo msemaji anaacha lugha moja na kuhamia nyingine.

Katika mbinu hii msemaji huacha lugha moja na kuingia lugha tofauti na kuizungumza kimfululizo. Msemaji anaweza kutumia uhamisho msimbo kama mbinu ya usemi ili kueleweka zaidi au kuwasilisha hoja zake kwa njia nyepesi.

Katika *Shujaaz* kuna mifano ifuatayo:

Katika CHAPTA 57, uk 3(kuhamisha msimbo)

- Nichapie hii story yako ndio niget kushare na mafan wa shujaaz
- Niko passionate about the environment na venye niliona Kibera ikiendelea kuwa chafu na kaamua kudo somethimg about it.
- Since 2012. Uk 4

Katika CHAPTA 27, uk 23 (kuchanganya msimbo)

- Hiyo story imeni-inspire sana!
- Nime-realise kumbe hata mimi naweza achieve anything!
- Madem tunafaa tutumie masomo kupigana na poverty kwa society

- **Tashbihi:**

Msokile (1992) anafafanua kuwa aina hii ya tamathali hutumia ulinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi 'ja', 'mithili ya', 'mfano wa', 'sawa na' na 'kama'. Mtunzi hutumia ulinganishi huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini ambayo athari yake ni ya kudumu zaidi.

- Walikaa (walikuwa kama) nyani zimenyeshewa! - 03/03 uk10 (mhusika aliyetumia maneno haya alikuwa akiwarejelea watu wa kabila tofauti na lake ambao walikuwa wakipingana katika uchaguzi na wakawashinda. Walioshindwa wakawa wamefedheheka na kukosa amani mfano wa nyani aliyenyeshewa.)

- **Methali:**

Kulingana na TUKI (2004) methali ni usemi wa kisanii ambao ni wa kimapokeo na jamii huuchukulia kuwa wa kweli na hutumiwa na jamii husika kufumbia au kupigia mfano. Vilevile, methali hubeba maana pana kuliko maneno yanayotumiwa.

- Jogoo wa shamba hawiki mjini – CHAPTA 27, uk 8- Mhusika aliyetumia methali hii ni bwanake Bi. Amani ambaye anapingana na mbunge aliopo katika kampeni za uchaguzi. Mbunge aliyopo

anatumia kikundi cha wahalifu cha SCARYFACE kutisha wapinzani wake, anawapa vijana shilingi hamsini kuwarai wamuunge mkono na pia kuwanunulia pombe ya chang'aa. Vitendo hivi vinapingwa vikali na DJ

BOIYE na kuhatarisha nafasi ya mbunge huyu kuchaguliwa tena lakini Bwanake Bi. Amani ana mhakikishia kiwa hatafaulu kwani jogoo wa shamba hawiki mjini.

- Hayawi hayawi huwa - CHAPTA78, uk 14. Kwamba mambo ambayo hayakutarajiwa kufika huja yakafika na wakati ulikuwa umewadia wa Musa kumchagua mchumba wake mtarajiwa.

- **Takriri:**

Msokile (1992), takriri ni aina nyingine ya tamathali za semi ambayo yenyewe huhusika na urudiajirudiaji wa maneno, silabi au sauti zinazolingana katika kazi ya sanaa. Mwandishi huamua kwa makusudi kurudirudia maneno au vipengele hivyo kwa lengo maalumu kwa kusisitiza jambo ama kuleta mkazo wa jambo linaloelezwa. Mfano katika *Shujaaz*:

- Discount! Discount…buy CD ya manlike Kalito leo! - CHAPTA 40 uk 5
- Helicopter! Helicopter! – CHAPTA 40 uk 5
- Sob! Sob! Sob! – CHAPTA 68 uk 18
- Hivi hivi - CHAPTA 68 uk 18
- Hayawi hayawi huwa - CHAPTA78, uk 14
- Katika! Katika! Katika! Katika! Hahaha! Hahaha! – CHAPTA 78 uk 9
- Tangazo! Tangazo! – CHAPTA 93, uk 10

- **Nahau:**

Kwa Mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981), nahau ni fungu la maneno arnbayo yakipangwa pamoja huleta maana isiyo ya kawaida ya kuonekana wazi. Aghlabu nahau huundwa kwa kitenzi na nomino. Lugha ya Sheng imeudika zaidi ki nahau. Baadhi ya mifano ya nahau katika *Shujaaz* ni:

- Kupata ball – kushika mimba – CHAPTA 109 uk 13
- Kuchoma picha – kujiaibisha- CHAPTA 109 uk 17
- Nitamfunza cha mtema kuni – tamwadhibu vikali - CHAPTA 27 uk 8

- **Utohozi:**

Kwa mujibu wa Mukhwana (1988) utohozi ni namna ya kubuni majina kwa namna ambavyo maneno ya lugha chanzi yanazingatia muundo wa lugha pokezi. Utohozi ni matumizi ya istilahi kutoka katika lugha nyingine na kuzirekebisha ili ziafikiane na mfumo wa fonolojia na mofolojia ya Kiswahili. Utohozi ni utaratibu wa kuyabadili maana au maumbo ya maneno mkopo kutoka lugha changizi ili yalingane na kuafiki mfumo wa sarufi wa lugha pokezi. Inabidi maneno yanayotoholewa kutoka lugha moja hadi ya pili yafwate utaratibu wa lugha pokezi. Utohozi katika *Shujaaz* ni hasaa maneno ya Kiswahili na Kiingereza na lugha nyingine kufanywa yawe ya Sheng.

Katika CHAPTA102:

- Bizna – business uk 2
- Biggie – big uk 2
- Gamu – gum uk3
- Hustla – hustler uk 2 n.k Katika CHAPTA 88:
- Talanta – telent uk 3
- Ofisi – office uk 6
- Basi – bus uk 7
- Siste – sister uk 12
- Familia – family uk 12
- Mapero – parents
- Dokte – doctor

Katika *Shujaaz* kuna aina yake ya kutohoa maneno ya Kingereza kwa kuongezea viambishi awali kabla ya neno husika. Kwa mfano katika CHAPTA 88:

- Ma -worry – worries (huzuni nyingi) uk 12
- Aliget – She got (alipata) uk 12
- Atakusow – you will be shown (alikuonyesha) uk 12
- Kimehappen – it has happened (kilifanyika) uk 12

- Ali-die – she died (alikufa) uk 12
- Ku inspect – to inspect (alikagua) uk 20
- Mayouth – youths (vijana) uk 23
- U-take – you take (uchukue)uk 24
- Ikicome – when it comes (ikija)uk 25 Katika CHAPTA 57:
- LIORGANIZE – he organized (alipanga)uk 3
- Kuget kushare na mafan- to get to shre with fans (kupata kufahamisha mashabiki)

- katika dondoo hili kutoka CHAPTA 93 uk 3, mhusika CHUXX ametumia maneno ma- customer badala ya wateja au customers, kucome badala ya kuja au coming, maboys badala ya wavulana au boys
- Katika uk wa 6, DOREEN ametumia mameno; m-different badala ya amekuwa tofauti au is different, kum-lose badala ya kumpoteza au to




lose him, nitam-help badala ya nitamsaidia au I will help him

**Kielelezo cha 66 kutoka CHAPTA 93 uk 3**

- **Tanakali za sauti:** Wamitila (2003) anathibitisha kauli hii kwa kusema kuwa tanakali sauti hutumiwa kurejelea sauti ambayo inaigiza jinsi kitu fulani kiangukavyo, kiliavyo, kilivyo n.k.
    - Twaff! - sauti ya kugongwa -CHAPTA 27, uk 11
    - Aaaaargh! - sauti ya maumivu CHAPTA 27, uk 11
    - Skreeeeeeee! – sauti ya gari kusimama kwa gafla CHAPTA 27, uk 11
    - Kuduff!! – sauti ya mwanguko mkubwa mchangani CHAPTA 33 uk 11
    - Aaaah! – sauti ya maumivu baada ya kugongwa. CHAPTA 33 uk 23
    - Bang! -sauti ya kugongwa. CHAPTA 33 uk 23
    - Mooo! – mlio wa ng'ombe CHAPTA 33 uk 24
    - Oof! – sauti ya kukazana kusukuma. CHAPTA 33 uk 24
    - Shwiiii! -sauti ya mwendo wa kitu kilichorushwa. CHAPTA 33 uk 27
    - Ndok! – mlio wa kugungwa na kitu. CHAPTA 33 uk 27
    - Slam!!! – mlio wa mlangu uliofungwa kwa nguvu. CHAPTA 68 uk 5
    - Pungulu! Sauti ya kuanguka. CHAPTA 78 uk 12
    - Fwuup! Sauti ya kuchukua kwa nguvu na kwa kasi. CHAPTA 98 uk 11
    - Mbrrrr!!! Mlio wa pikipiki CHAPTA 109 uk 17
    - Waaaah! Kilio cha mtoto mchanga. CHAPTA 109 uk 17
- **Sitiari:**

Mbuvi (2013) anafafanua istiari kama mbinu ya kulinganisha kitu na kingine, chenye sifa sawa nacho, moja kwa moja kama vile: jambo hilo ni nanga, kumaanisha ni zito. Mtaalamu huyu anadai kuwa zipo pia sitiari ambazo hazichukui muundo huu. Hizo hutaja neno tu bila kulihusisha na kitu.

- Mwanamke ni bidii -CHAPTA 57, uk13
- Watu ni pesa – special edition 01/03 uk4
- Si nimekuwa nikisema ni kunguni hawa wametunyonya damu- 01/03- uk 11
- Watu wa kabila hio sio watu, ni Wanyama- 01/03, uk 11

- niliguza hii twiga when? CHAPTA 98 uk 29

- **Taharuki**

Mvati (2009) anafafanua mbinu hii ya taharuki kuwa ni tamathali ambayo mtunzi huonyesha kutoelezea alichotaka kusema mpaka mwishoni mwa shairi lake. Wamitila (2003) kwa upande wake anasema kuwa taharuki kuwa ni istilahi inayotumiwa na mtunzi kuonyesha hamu anayokuwa nayo msomaji yakutaka kujua yatakayotokea. Hali hii humfanya msomaji kutaka kujua mambo ambayo yatatokea baadaye. Hii ni mbinu ambayo humfikirisha msomaji

- Mwisho wa sehemu ya MARIA KIM, uk15, unaacha msomaji na hamu ya kutaka kujua ni nini kilifuata baada ya mkasa wa moto.
- Vile vile msomaji anabaki akitaka kujua hatima ya Esther baada ya wasiwasi aliokuwa nao baada ya kuingliana kimapenzi na kijana Mich. Alipata mimba au ugonjwa au kuliendaje? Uk31
- CHAPTA 78, uk 23, msomaji nanabaki akijiuliza kama Lily atakubali kuolewa na mpenzi wake

- **Jazanda:**

Kwa maoni ya Wamitila (2008), jazanda zinaweza pia kuwa za kimaelezo au za kimaelezi au za kiishara. Ishara na maelezo hayo hubeba maana inayochangia kunatisha ujumbe wa mtunzi kwa akili za msomaji kwa kumwezesha kujenga taswira ya hulka na falsafa ya mwandishi. Katika *Shujaaz* kuna matumizi ya jazanda ifuatavyo

- **Kisu** katika kauli ‘kisu tunayo hatuna?’ Kimaanisha tohara. CHAPTA 102 uk 26

- **Uzungumzi nafsia:**

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) hii ni mbinu ambapo mhusika anajiongelesha. Ni mawazo yanayompitikia mhusika yanawasilishwa moja kwa moja bila ya kuingiliwa kwa namna yoyote na mtunzi au mwandishi. Katika *Shujaaz* kuna mifano ifuatayo ya matumizi ya uzungumzi nafsia.

- **Boiye:** inaonekana kuna njia zingine za kuepuka ghasia lazima ni-share na vijana- 03/03 uk3
- **Chuxx:** wameanza machozi. Mimi nime-bounce! CHAPTA 27 uk 19

- **Babake Charlie Pele:** Woi! Woi! Nitafanyaje na hizi seeds sasa? CHAPTA 27 uk 25 na uk 26
- **Deepti:** nitatumia DJ B hizi issues za hawa vijana ye ndio anaeza waokolea na info ya maana. CHAPTA 33, uk 4.
- **Charlie Pele:** Nimechoka! Nimemaliza kupanga hizi sweet potatoes za kuuza kesho. Lakini ilikuwa kazi poa leo! Uuuuuaaaa…sasa ni kulala.
- **JK:** mimi si m-careless kama Simo. Nitanunua hii place nii-run vipoa.

  CHAPTA 57 uk 10
- **Maria Kim:** I hope JK ameni-forgive. CHAPTA 57 uk 10
- **Malkia:** Awww…ni TV Producer mpoa…aki sini win hiyo dooh! CHAPTA 57 uk 27.
- **Esther:** Aki he's the best dunia nzima! Niko sooo lucky! CHAPTA 57, uk 27
- **Chuxx**: lakini…what if ni ukweli? Nimelenga calls mob tangu doh ziishe!... niliguza hii twiga when?!

- **Mbinu rejeshi/ kisengere nyuma:**

Mbinu rejeshi ni hali ya msimulizi au mhusika kurejelea matukio ya awali ambayo huenda yanahusiana na hali yake anapoyarejelea. Mwandishi hutumia mbinu hii kuoanosha matukio ya awali na ya sasa. Mifano katika *Shujaaz* ni kama ifuatayo:

- Katika uk 12 katika SPECIAL EDITION 01/03, mhusika Charlie Pele anamkumbusha Rosie kuhusu vita vya kikabila ambavyo vilivuka baada ya uchaguzi uliopita na kusababisha vifo vya watu, nyumba zilichomwa, zingine zikabomolewa, na wanyama wakaibiwa. Haya yaote yakitokana na uchochezi wa kikabila au 'Hate Speech'. Hangependa hali kama hii ijirudie na ilikuwa lazima angefanya jambo kuzima uchochezi uliokuwa ukiendelea katika Kijiji chake.
- Chapta 12 yote imetumia mbinu rejeshi kwani kila mhusika; DJ BOIYE, MALKIA, MARIA KIM na CHARLIE PELE, wanarejelea matukio

mbalimbali ambayo waliwasilisha kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu Shujaaz ianze.

– Katika CHAPTA 88, uk11-13, mhusika SLIM anamsimulia SIFA namna dadake alivyoaga dunia baada ya kuavya mimba.

- **Chuku:**

Wamitila (2003) anaeleza kwamba chuku hurejelea hali ya msanii kukuza sifa Fulani kupita kiasi. Kukuzwa huko huwa kwa udogo au ukubwa. Nia hasa ya kuitumia chuku ni kulifanya jambo fulani litokeze kwa uwazi zaidi, kuikuza sifa fulani na kumfikirisha msomaji kwa kuuona uzito uliopo**.**

Katika CHAPTA 57, uk 32

- Tv yenyu ni noma inashika station zote mpaka police station! (mchongoano)
- Ujinga ni kubeba ladder ukiadmitiwa ati unaenda High school! (Ujinga ni?)
- Ujinga ni kuweka simu kwa maji asubuhi ndio FB inawe uso! (ujinga ni?)

**1. Matumizi ya tanzu na vipengele vingine vya fasihi**

- **Malumbano ya Mchongoano:**

Githinji (2007) anatoa kijelezi cha mchongoano kama utanzu unaohusisha majibizano ya wawili ambayo hutumiwa na vijana nchini Kenya. Katika hali hii, mmoja humtania mwingine au jamaa yake. Anaendelea kueleza kwamba huu ni mchezo wa maneno ambao ni wa kutaniana. Waaidha, ni kauli zinazotolewa kwa njia ya mzaha

isiyomuudhi mtu, isipokuwa kumshajiisha ili naye atunge mchongoano wake wa kuchekesha zaidi. Nao Morgan (2002) na Labov (1972) wanaeleza kwamba michongoano hutumika sana miongoni mwa Waafrika. Kwamba inahusu michezo ya kutusiana inayoelekezwa kwa mwingine au familia yake kama vile baba, dada au marafiki zake. Kimani (2013) naye anasema kwamba mchongoano ni utanzu unaokaribiana na vitendawili vya kiasili lakini una nguvu zaidi ya kuathiri hata vitendawili hivyo asilia. Mchongoano kama tunavyoujua hivi leo basi ni kijipera cha mazungumzo kilichoasisiwa au kuhuishwa na vijana na watoto wa leo. Ni tukio la

uzungumzaji linalonuia kukejeli, kutania au kudunisha mpokeaji.

- Katika CHAPTA 93, uk 32
  - Uko na meno ya yellow hadi ukifungua mdomo tumbo inakaa kama imewashwa bulb.
  - Kwenu mko wachafu hadi nzi za kwetu huziita za kwenu nzi za ghetto.
  - Huyu msee ni mshort hadi aki- tuck ni shirt mkono inaingia kwa socks.
  - Haiya, uko na meno big hadi zingine zimetokea nje ukienda hosi madoki hukutoa mbio wakithani unawachekelea wagonjwa. n.k.
- Katika CHAPTA 27, uk 31
  - Una kisogo bigi hadi inatokelezea nyuma ya ID.
  - Mbu za kwenu ni sugu hadi ukiwasha mosquito coil zina- kam kuota moto.
  - Kwenyu mmesota hadi mnahama na taktaka.
  - Kwenyu mmesota mpaka usiku mnatoa wall clock yenyu battery ndio zisiishe.
  - Uko na macho makubwa hadi mtaani unaitwa eye witness. n.k
- Katika CHAPTA 57, uk 32
  - Ati wewe ni fala ulido exam peke yako na ukakuwa number two.
  - Ati uko useless ata huwezi 2miwa kama bad example!
  - Ati mbuyu wako ni mkoloni mpaka akikupa gorogoro moja anakupa receipt! n.k

**Sifa za mchongoano kama ulivyotumiwa katika *Shujaaz* ni;**


- Uwasilishaji wake unahitaji pande mbili zinzoshindana kila upande ukijaribu kupiku upande mwingine kwa kutoa kauli itakayo fanfa upande pinzani ukose la kusema.

- Sifa nyingine ni ile ya matumizi ya tamathali za usemi kama vile kupiga chuku na jazanda.

  Mfani ni katika uk 32 CHAPTA 93 – kwenu mko wachafu hadi nzi za kwetu ziuita za kwenu nzi za ghetto!
- Mchongoano husheheni matusi hasa ya kusuta watu wajamaa, marafiki au kabila la mhusika mwenza.

Mfano uk 31 katika CHAPTA 33 – wewe ni mnono mpaka ukitembea siol inasema tembea vizuri.

- Mchongoano huchanganya au kuhamisha msimbo/ndimi. Kanuni za kisarufi hukiukwa kwani huwa hutokana na Sheng.
  Mfano katika uk 29 CHAPTA 33 – Ati kwenu kuna insecurity mpaka police station hufungwa saa kumi.
- Baadhi ya michongoano huanza kwa – 'Kwenyu mna/ kuna…', au 'Ati/Eti…', au jina kisha ni kwa mfano 'Kakako ni…', 'wewe ni…'. Mfano katika uk 32 CHAPTA 93- Eti uko na Ngozi tight




hadi ukufungua jicho moja mguu unainuka.

**Kielelezo cha 67 kutoka Chapta 57 uk 32**

-

Mchongoano una umuhimu wake kwani:

- Mchongoano husaidia kujenga vipawa vyao vya wanaoshiriki kufikiria na kuongea.

- Mchongoano hujasilisha wanaoshiriki kuwa wakakamavu mbele ya wenzao.
- Michongoano pia huwasaidia wanaoshirika kujumuika pamoja na kujenga uhusiano wa karibu miongoni mwao.
- Mchongoano huburudisha kutokana na ucheshi wake.
- Mchongoano husaidia watumiaji wake kuwasiliana, kufarijiana, kuelimishana na kupitisha muda huku wakitaniana


Mwandishi wa *Shujaaz* ametumia mchongoano katika kazi yake katika juhudi ya kuakisi ukamilifu wa shughuli zote za vijana ikiwemo burudani yao ya malumbano ya kutaniana.

- **Malumbano ya Ujinga ni?**

Githinji (2022), ucheshi unaokejeli ujinga ni kipera kingine cha Sanaa jadiiya ya watumiaji wa Sheng na hudhamiria kuonyesha upuzi au upumbavu wa kushikilia imani fulani au kufanya vitendo fulani. Fani hii hushirikisha imani maarufu zinazoshikiliwa na jamii, mara nyingi zikiwa usaguzi. Imani hizi kwa kawaida huwa potofu, lakini muradi tu Wakenya wengi wamezishikilia, basi zinatumika katika sanaa hii.

- Katika CHAPTA 57, uk 32
  - Ujinga ni kubebe ladder ukiadmitiwa ati unaenda high school.
  - Ujinga ni kueka picha ya daktari kwa keja ili maumivu yakizidi unamuona daktari.
  - Ujinga ni kuweka simu kwa maji asubuhi ndio FB inawe uso.

- Katika CHAPTA 27, uk 31





**Kielelezo cha 68 kutoka Chapta 27 uk 31**

Ujinga ni kubambwa na kasavuli hadi aki-smile kwa TV unamfugia jicho.

- Ujinga nikuuliza ‘face book ina pages ngapi?’
- Ujinga nikuweka miwa kwa fruit salad
- Ujinga ni kupigia mtu simu usiku kumuuliza kama amelala.

- Katika CHAPTA 93, uk 31
  - Ujinga ni kukatia dem kwa kanisa then unamlipia sadakaUjinga ni kubeba makaa na umevaa t-shirt imeandikwa ‘lets conserve our trees’
  - Ujinga ni kucheza ball mguu tupu na dame yako ni kiatu
  - Ujinga ni kuambia kipofu 'unanionea’
  - Ujinga ni kukopa landlord pesa alafu izo pesa ulipe nazo rent




**Kielelezo cha 69 kutoka CHAPTA 33 uk 29**

Sifa za malumbano ya utani:

- Huwa na sehemu ya swali na jibu: Ujinga ni (swali), kumeza Mara moja (jina la dawa) mara mbili(jibu)
- Hutumia kuchangaya msibo: ujinga nikuwa na beef na mama mboga
- Hulenge kudhihirisha ujinga au ukosefu wa hekima au ufahamu wa mrejelewa. Kiini chake ni kudhihirisha ujinga uliopo
- Nyingine huwa na maana fiche: Ujinga ni kuambia kipofu 'unanionea'
- Hutumia lugha ya Sheng: Ujinga ni kukatia dem kwa kanisa then unamlipia sadaka

Majukumu ya Malumbano ya Ujunga ni? ni kama yale ya Malumbano ya Mchongoano. Malumbano haya mawili ni mbali na kuwa yameandikwa katika Shujaaz kimsingi husemwa kwa mdomo na wahusika wanapolumbana. Ni vipengele vya utanzu wa wazungumzo ambavyo vimeibuka katika kizazi cha vijana wa kisasa.

- **Nyimbo:**


Kinoti (2008) anaeleza kuwa nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya kuvutia kwa mahadhi ya kupendeza. Anaendelea kufafanua kuwa kuna aina za nyimbo kama vile; za kuzaliwa kwa mtoto, kuongoa, watoto wachezapo, tohara, mapenzi, harusi, kazi, matanga na nyinginezo. Wamitila (2003) anafafanua kwamba ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Na tungo hizi huundwa kwa njia ya mkato, picha na mapigo ya silabi. Katika *Shujaaz* kuna matumizi ya nyimbo kama ifuatavyo.

- Malaika! Nakupenda malaika! Nami nifanyeje? Ningekuoa malaika...! CHAPTA78 uk 22-23.
- Happy birthday to you! Happy birthday to you! Happy birthday dear Esther!... CHAPTA 93 uk 15.

- **Tawasifu**

Madumulla (2009) anafafanua tawasifu kuwa nathari inayohusu maisha ya mtunzi

mwenyewe au mhusika katika kazi ya fasihi kama ilivyo katika *Shujaaz*. Katika *Shujaaz* mwandishi katika sehemu za CELEB katika matoleo tofauti amewapa wahusika ambao ni watu halisi lakini akitumia picha zao nafasi ya kutoa tawasifu ya maisha yao tangu utotoni, utu uzima na matarajio yake ya baadaye kwa njia ya safari, huku akitaja matukio aliyokutana nayo na athari za matukio hayo kwa mtazamo wake maishani. Katika *Shujaaz* hali hii inatikea kwa njia ya mahojiano san asana baina ya mhusika na DJ Boiye. Picha za wahusika hawa mashuhuri wengi wakiwa wasanii huwepo katika sura ya matoleo husika.



Katika *Shujaaz*, Wahuska mashuhuri katika jamii wamehusishwa na kupata fulsa ya kujitambulisha na kuelezea maisha yao hadi kuafanikiwa kwao. Kwa mfano:

- Katika sehemu ya CELEB, uk 16-17, kuna tawasifu ya msanii wa kutoka Kingstone Jamaica ALAINE
- Tawasifu ya Victoria Kimani CHAPTA 68 uk 16-17.
- Tawasifu ya Liz Marami, CHAPTA 78, uk 8-9.
- Tawasifu ya Ronald Tunoi CHAPTA 88, uk 24-25
- Tawasifu ya Dr, Ofweneke, CHAPTA 109, uk 21-22
- Tawasifu ya Esther Chebet, CHAPTA102, uk 8-9.
- Tawasifu ya Govi au Lemuel King Malik, CHAPTA 98, uk 16.
- Tawasifu ya Phy Ngetich, CHAPTA 93, uk 8-9.

(v) **Matumizi ya daiolojia**:


Jambo la kuzingatia hapa ni namna mwandishi ametumia diolojia kwa kiasi gani na ni kwa kiasi gani daiolojia husimulia hadithi? *Shujaaz* inahusu mazungumzo baina ya wahusika. Maneno ya wahusika yamefunziwa katika vibofu na yameandikwa kwa herufi kubwa.

*Shujaaz* kama vitabu vingine vya katuni au vibonzo na fotonovela wahusika huzungumza maneno yao yakiwekwa ndani ya vipofu vya maneno. Ni katika sehemu za matangazo au maelezo ya mambo tofauti ambapo maandishi ya nadhari hutumika. Kwa mfano katika SPECIAL EDITION 03/03 uk 8 -9, kuna sehemu ya maswali na majibu kuhusu pendekezo la katiba. Katika CHAPTA 93, katika uk 32 , pana mifano ya 'Mchongoano' na 'Ujinga Ni?', uk 29 pana maelezo ya kazi za MCA na uk 16, pana matangazo ya wadhamini.

Ifuatayo ni mifano ya namna daiolojia inavyojitokeza katika CHAPTA 88 uk 25, namna maelezo kwa maandishi ya nadhari yanavyotokea mfano katika CHAPTA 88 uk 16 na CHAPTA 93 uk 29 na jinsi mahojiano ya maswali kwa majibu yalivyotumika katika SPECIAL EDITION 03/03 uk 9.




**Kielelezo cha 72 kutoka Chapta 88 uk 25**



Q HOW WILL DA CONSTITUTION MSG BE RECEIVED AND UNDERSTOOD ESPECIALLY IN DA PASTORAL COMMUNITIES? WILL THERE BE VOLUNTARY YOUTH GROUPS AVAILABLE?

A COMMITTEE OF EXPERTS INA CORDINATORS WALIOWEKWA KWA KILA CONSTITUENCY NA WAFANYA KAZI WA COMMUNITY-BASED ORGANIZATIONS NA KUHAKIKISHA WAKENYA WAMEFUNDISHWA JUU YA CONSTITUTION KABLA YA REFERENDUM.
- COE

Q JE CONSTITUTION NI MRADI WA SERIKALI? MBONA BASI KUNA 'YES' NA 'NO'?

A CONSTITUTION NI PROJECT YA KENYA NA YA WAKENYA WOTE. REFERENDUM INAPATIA WANANCHI OPTION YA KUKUBALI AU KUKATAA CONSTITUTION KWA KU-VOTE YES AU NO.
- COE

Q HIYO NI POA BT SAGA YA KUPATA ID UKIFIKA 16 ILIENDAJE?
- THOMAS TJ MBOGHO.

A HAKUKUWA NA PROPOSAL KAMA HIYO.
- COE


Q MBONA WATA TOA PUBLIC HOLIDAYS?
- JEFF, NAIROBI.

A PROPOSED CONSTITUTION ITABAKISHA NATIONAL DAYS LAKINI PARLIAMENT INA MAMLAKA YA KU-ANNOUNCE PUBLIC HOLIDAYS.
- COE

Q JE COMMITTEE IMEPITISHA MA-YOUTH WATENGEWE DOOH ZA KUBORESHA MIRADI YAO?

A ARTICLE 55 INA-PROVISIONS ZA KU-ALLOW YOUTH KUPATA TRAINING, KUAJIRIWA NA KUPATA NAFASI YA KU-PARTICIPATE KISIASA, KIUCHUMI NA MAISHA YA WATU WOTE.
- COE

**Kielelzo cha 73 Kutoka Special Edition 03/03  uk 9**




**Kielelezo cha 74 kutoka Chapta 88 uk 16**




**Kielelezo cha 75 kutoka CHAPTA 93 uk 29**

**(vi) Namna ya usimulizi [zama zaidi]**

Katika kipengele hiki ni muhimu kuchunguza ikiwa mwandishi anatumia nafsi ya kwanza, ya pili, ya tatu au nafsi mbalimbali zinazopishana katika usimulizi wake. Katika *Shujaaz* masimulizi yanatolewa katika kauli ya usemi halisi. Masimulizi ni kwa njia ya mazungumzo au mahojiano baina ya wahusika waliomo. Kama ilivyo mtindo wa tunzo za katuni/vibonzo na fotonovela wahusika huendeleza masimulizi ya hadithi kwa kuzungumza baina yao huku maneno yao

yakiwekwa kwenye vipofu vya maneno huku wakipishana na kuendelea. Kwa hivyo nafsi inayotumika hutegemea iwapo wanaozungumza wanazungumzia kujihusu (nafsi ya kwanza

hutumika), au wanazungumzia wale wanaozungumza nao (nafsi ya pili hutumika), au wanazungumzia watu wengine ambao hawapo kati yao (nafsi ya tatu hutumika). Kwa mfano katika CHAPTA 93, sehemu ya MARIA KIM, uk 2- 7, katika wazungumzo kati ya wafanyikazi wa hoteli, nafsi zilizotumika zinategemea mrejelewa. DOREEN anapomrejelea Mose anasema 'WEWE NI BAE KABISA! THANKS KWA KUNI-ESCORT MPAKA HAPA KWA JOB' nafsi iliyotumika hapa ni ya kwanza. Mhusika CHUXX katika uk 4 kuna mahali anawambia DOREEN, 'UNABEBANA NAZO KILA MAHALI, WEWE NI PUBLIC TOILET!' nafsi iliyotumika hapa ni ya pili.




CS Scanned with CamScanner

**Kielelzo cha 76 kutoka Chapta 78 uk 2**

(vii) **Toni na Hisia**

Katika kipengele hiki la muhimu ni kuchunguza mtunzi ianibua hisia zipi na zinaonekanaje katika hadithi? Je, ni mwenye za dhihaka? Ni mwenye mapenzi, ni mwenye matumaini, ni mwenye hasira na ukali, ni mwenye kejeli, furaha, huzuni au anaibua hisia zipi? Katika *Shujaaz*, toni hutegemea matukio husika hasa wakati wahusika wanaonyesha hisia zao ambayo hudhihirika katika jinsi walivyochorwa na maneno yao yalivyo wasilishwa. Mfano katika sehemu ya CHARLIE PELE

katika CHAPTA 27 uk 25, 26 na 27 ambapo hisia za mshangao, furaha, maumivu na hasira




zionekana katika kanakali za sauti zilizotumiwa na wahusika

**Kielelezo cha 77 kutoka Chapta 27 uk 25**

**Kielelezo cha 78 Kutoka Chapta 27 uk 26**






**Kielelezo cha 79 kutoka Chapta 27 uk 27**

Katika CHAPTA 27, uk4-9, toni iliyopo ni ya kughadhibika kwa BJ BOIYE na vijana wenzake kutokana na tabia ya vijana kuuza kura zao na hapo kupoteza nafasi ya kutumia haki yao ya ili kuhakikisha wamewashinda wapinzani wao kwa njia isiyo ya haki. Uk25-30 CHARLIE PELE na wanakijiji wenzake wanahasira ya kuuziwa mbegu bandia na nmatapeli wanaojifanya kuuzia wakulia mbegu zilizo idhinishwa.

Katika CHAPTA 98, sehemu ya MALKIA ya #BAEMILELE, uk 8-9, hisia zilizopo ni za mapenzi baina ya vijana husika kwa namna walivyo kumbatiana na maneno yao. Kila sehemu

kutegemea mada husika inaibua toni tofauti




**Kielelezo cha 80 kutoka Chapta 98 uk8**

Kama aelezavyo Adungo (2019) kuhusiana na uwasilishaji wa hisia katika fasihi, mwandishi wa *Shujaaz* ameandika kuhusu yale anayoyaishi kuona, kusikia, kuonja, kunusa au kuhisi katika maisha yake ya humu duniani. Kila hisia ina umuhimu wake kutokana na mazingira ya tukio linalohusika au kusimuliwa. Katika *Shujaaz* msomaji ana nafasi ya kushirikiswa kwa hisia zake zote kutokana na matukio yanaendelea katika kila tukio kwani matukio yanajitokeza kwa njia ya utendaji wa wahuska. Wahusika wenyewe wakiweza kumwaathiri msomaji kutokana na jinsi wao wanavyo dhihirisha hisia zao katika vitendo vyao na kutokana na maingilianao yao na wahusika wengine. Kwa mfano, katika CHAPTA 102, sehemu ya MARIA KIM, uk 5, mwandishi amefaulu kuibua hisia ya kuona wahusika wakidhihirisha hisia ya hasira na

kughadhibika. Uk 6, mwandishi anaibua hisia ua kunusa pale mhusika anapochafua hewa kutokana na wasiwasi aliokuwa nao.

e) **Matumizi ya tanzu nyingine za fasihi**

Ni muhimu kutaja yafuatayo kuhusu *Shujaaz*. kuwa *Shujaaz* ni upatanisho wa mitindo tofauti kwani kuna matumizi ya michoro ya katuni. Kuna matumizi ya picha halisi za wahusika amba ni watu halisi katika jamii, zinazoifanya *Shujaaz* kuonekana kama fotonovela katika baadhi ya sehemu zinapotumika.

Kuna matumizi ya lugha ya vipera vya utanzu wa fasihi simulizi iliyoandikwa yaani 'Mchongoano' na 'Ujinga ni?' (Mifano katika CHAPTA 27, uk 31. CHAPTA 40, uk 24. CHAPTA 93, uk 32. CHAPTA 57, uk 32), inahusisha kupitia matumizi ya jumbe fupi za simu katika mwisho wa kila sehemu.

Vilevile kuna matumizi ya tawasifu ambazo ni za vijana hashuhuri na wasanii nchini Kenya na hata kutoka nje ya nchini ya Kenya. Kwa mfano katika sehemu za CELEB katika CHAPTA 93, uk 8-9. CHAPTA 57, uk 16-17, CHAPTA 68, uk16-17, CHAPTA 102, uk 8-9. CHAPTA 88, uk 24-25. CHAPTA 109, uk21-22. CHAPTA 98, uk 16-17.

f) **Mandhari / mazingira**

Mtunzi wa kazi ya fasihi akiwemo mtunzi wa *Shujaaz* hutunga kazi yake katika mandhari fulani. Wamitila (2008) anaelezea kuwa, mandhari hurejelea wakati na mahali pa hadithi au kazi ya kifasihi. Katika kuchunguza mandhari katika *Shujaaz* ni vyema kuchunguza mazingira yaliyohusishwa katika utungo kama ni ya kihistoria (ni ya lini?), kijiografia (yalitukia wapi?), kijamii (yalihusihs akina nani) na /au kiutendaji (yalitukia vipi?) kama anavyopendekeza Njogu na Chimerah (2008). Kwa hivyo, katika kuchunguza maandhari katika *Shujaaz* ni muhimu kuzingatia wakati unaorejelewa na matukio yalitukia wakati gani katika historia ya jamii. Kwa mfano, mandhari ya *Shujaaz* iliandikwa katika kipindi kabla ya ukoloni au wakati wa ukoloni au baada ya ukoloni au ni wakati wa sasa. Maudhui ya *Shujaaz* yamesaidia kuelewa wakati husika. Ni muhimu kuchunguza matukio yanatokea wapi? Yanatukia pwani, mashambani, mijini,

sehemu za mabanda au katika sehemu gani? Mahali matukio yanatukia katika utungo yatasaida kujenga maudhui ya mtunzi na uwelewa wa jumuiya husika. Utungo unahusu jamii au jumuiya wa watu gani na utamaduni na kaida zao za maisha ni zipi? Ni watu wa mjini au mashambani vijijini? Hali zao za maisha kijamii kisiasa na kiuchumi ni zipi? Ni wakulima, ni wavuvi, ni wanafunzi au wafanyakazi? Kisiasa ni watawala /viongozi au ni watawaliwa? Imani ya jumuiya husika ni ipi? Ni wakristo au waislamu? Mazavi yao, vyakula vyao, makazi yao, mila na desturi zao ni zipi? Kisha ni muhimu kuchunguza utendaji wa wahusika na uhusika wao katika mazingira husika. Matendo yao yanauhalisia au la, yameadilika au la, yanaibua hisia zipi na vipi, yanakisi jamii vipi?


Kwa kuzingatia maswali hayo yaliyotajwa hapo juu kihistoria au kiwakati *Shujaaz* ni kazi ya kisasa. Inahusu wakati wajamii ambayo inajitawala na ambayo inashughulika katika kujiimarisha kiuchumi kisiasa na kijamii miongo kadhaa baada ya kupata uhuru wake. Kiwakati kazi hii katika muktadha wa nchi ya Kenya ni katika miaka ya 2000 hadi sasa. Sababu ya kusema hizi ni kutokana na yaliyomo katika matoleo maalum yani SPECIAL EDITION 01/03, uk 8-9 na 03/03, uk8-9 na sehemu ya MARIA KIM katika 01/03, uk13-15 yana maelezo kuhusu shughuli ya uundaji ya katiba na kuhusu kura ya maoni kuhusiana na katiba hiyo jambo lililotokea nchini Kenya mwaka wa 2010. Katika CHAPTA 93, uk 29-30, mtunzi anazungumzia kuhusu majukumu ya wawakilishi wa maeneo ya ugatuzi katika mbunge la gatuzi. Maelezo haya yanadhihirisha usasa wa kisiasa ulipo katika *Shujaaz*. Masuala ya kisiasa yanayoakisiwa na mtunzi yanaangazia yanayoendelea katika jamii kisiasa hivi sasa. Mtunzi anajaribu kuonyesha nafasi ya vijana katika siasa hizi.

Ama kwa upande wa kijamii, kazi ya *Shujaaz* ni ya kisasa kwani jamii lengwa ni jamii ya kisasa kutokana na hali yao ya maisha na shughuli zao za kijamii za kila siku. Mavazi ya vijana ni ya kisasa kiasi vilevile. Tunakutana na wasichana kuvaa suruali ndefu kama fashoni au mitindo yenye athari za kimaghari. Kadhalika , mazingira ya shule ni ya kisasa kama vile majengo na mandhari ya shule kwa jumla. Kwa upande wa matumizi ya lugha kwa vijana iliyokithiri ni Sheng. Hii ni lugha wa kisasa kwani haikuwepo hapo awali. Ushahidi waonyesha kuwa mtunzi wa *Shujaaz* ameifahamu jamii ya vijana waliowengi hasa wanaoishi mijini wa kutumia lugha ya Sheng katika shughuli zao kila siku. Ndio mtunzi baada ya kufahamu kuwa hadhira yake

aliyoikusudia ni vijana walioathiriwa na lugha ya Sheng hivyo *Shujaaz* ilikuwa rahisi kufahamika na vijana.

Mtunzi anonyesha maisha wa wakazi wa mijini hasa maenyeo yaliyo na wakazi wengi ya mabadani. Maisha ya mabandani ni maisha ya yaliyona changamoto nyingi kuanzia majengo yaliyosongamana tena ya hali duni. Ukosefu wa huduma na mahitaji ya kimsingi kama maji safi, miundo msingi ya kuondoa takataka zilizotapakaa kila mahali na ukosefu wa vyoo safi na miundo msingi ya kuongoa uchafu wa vyoo hivyo ni baadhi tu ya changamoto hizo.

Matimizi ya teknolojia ya simu, tarakirishi, mitandao ya kijamii ni mamabo ya kisasa. Mtunzi wanashirikisha hadhira yake kupitia teknolojia ya simu pale amefungua mwanya wa wasomaji kuchangia katika mada husika kupitia jumbe fupi za simu kwa kutumia numbari 20308 bila ya gharama yoyote. Mtunzi ameamua kutumia mbinu hii ya kuwasiliana na vijana kwani kila wakati vijana huwa na simu zao mkononi na wanapenda kuwasiliana kwazo. Vijana hawapendi kusema mengi hivyo jumbe fupi huwafaa zaidi. Mtunzi anafahamu kuwa vijana wengi hawana pesa hivyo basi anawapa nafasi kuwasiliana naye bila malipo na zaidi ya hivyo anachochea mawasiliano haya wakati mwingine kwa kuwapa zawadi za pesa wanapowasiliana naye kwa kutumia jumbe fupi. Mfano upo katika kilelezo kutoka Chapta 88 uk 7. Mambo haya




yanajitokeza katika matoleo yote ya *Shujaaz*. Baadhi yakiwa na hizo ahadi za pesa.

**Kielelezo cha 81 kutoka Chapta 88 uk 7**

Kichumi, kazi ya Shujaaz inaangazia nyakati za kisasa ambapo kinahimizwa kilimo biashara. Kwa mfano katika CHAPTA 102, uk 25, CHAPTA 68, uk10-15 na CHAPTA 33, uk 30-31 inaeleza mbinu za kisasa za kilimo ambazo vijana wanahimizwa kuzishiriki. Vile vile sehemu zote za CELEB katika matoleo yaliyo na sehemu hii, maelezo ya tawasifu ya vijana mashuhuri yanahimiza vijana kuwa wanaweza kufaulu kiuchumi kwa kufuata mikondo mbali mbali ya kujiendeleza kama vile talanta za usanii na taaluma. Kuna kazi nyingine ambazo ni za kisasa ambazo mtunzi na wahimizia vijana katika sehemu zote za HUSTLE FITI. Kwa mfano CHAPTA109, uk 2-7 anapoelezea kuhusu biashara ya upishi na kama vile ususi wa nywele, CHAPTA 57, uk 19-24,

Katika kuchunguza matukio yanatokea wapi na jumuiya ya maeneo hayo matukio katika *Shujaaz* yanatukia kutegemea maudhui ya tukio husika yakiongozwa na wahusika wakuu wanowasilisha maudhui hayo. Mhusika CHARLIE PELE matukio yake yanatukia katika sehemu za mashambani. Kwa mfano, katika CHAPTA 27, uk 25-30 tukio latokea mashambani na linahusu kuchagua mbegu zifaazo kupandwa na wakulima. CHAPTA 33, uk 23- 28, tukio latokea mashambani na la husu lishe bora ili kuepokana na janga la kuangukia upofu. CHAPTA 57, uk 19-24, tukio latokea katika sehemu ya Sotik sehemu gatuzi la Bomet na linahusu uwajibikaji wa wanabiashara katika maeneo ya vijijini. SPECIAL EDITION 01/03, uk10-12, inahusu hatari za uchochezi wa kikabila ambao unaweza kusababisha vita vya kikabila nakuleta vifo na uharibifu wa mali. CHAPTA 68, uk10-15, tukio linatokea Narok katika shamba la viazi la mkulima kijana. Jumuiya husika hapa inahusu watu wanaoishi vijijini, vijana wakiwepo katika kila tukio, shughuli za mashamba na ufugaji, uwepo wa soko za vijijini, uwepo wa misitu na mashamba makubwa na kutokuwepo kwa msongamano wa majengo kama ilivyo katika CHAPTA 33.

Mhusika MARIA KIM ni mhusika anayeishi sehemu ya mjini hasaa sehemu za mabanda ya Jongo. Kwa hivyo mandhari hapa ni ya sehemu ya makazi duni yenye msongamano wa majengo na watu wengi. Kupitia kwake tunapata mandhari ya shule kwani alikuwa ni mwanafunzi katika shule ya upili ya JONGO HIGH SCHOOL. Akiwa mtaani yupo katika sehemu za kawaida katika maeneo ya mabanda; dukani, hotelini, sehemu za burudani n.k. CHAPTA 68, uk 18-23, MARIA baada ya shule wamejazana katika chumba chake na marafikize hali ya kawaida ya

Maisha katika sehemu wanamoishi. CHAPTA 98, uk 10-15, mandhari ni shuleni JONGO HIGH SCHOOL. Katika SPECIAL EDITION 03/03, MARIA yuko nyumbani sehemu ya mabandani siku ya kuamkia upigaji wa kura ya maoni kuhusu katiba mpya. CHAPTA 93, uk17-21, MARIA na BRUCE wanazungumzia kuhusu biashara ya kilimo cha uyoga. ambayo haihitaji shamba au eneo kubwa. Jumuiya ya hapa ina wingi wa vijana na shughuli nyingi za vijana mtaani. Majengo ya hapa mabandani yamesongamana na wazi ni wengi. Tabia na mavazi ya vijana hapa ni ya watu waliokengauka. Vijana hapa wanahangaishwa na suala la anasa na mahusiano ya kimapenzi na hatari zake. Kama ilivyo katika CHAPTA 88, uk 9-14.

Mhusika MALKIA ni mhusika ambaye anapatikana katika mandhari tofauti tofauti. Mara yumo mjini, mara mashambani sehemu ya pwani na pia ni mwanafunzi shuleni. Katika SPECIAL EDITION 01/03, uk 5-7 MALKIA yumo shuleni na wenzake. CHAPTA 78, uk 10-15, yuko mashambani sehemu ya pwani kuliko na minazi. CHAPTA 109, MALKIA uk 13-20, yumo mtaani kwenye ufuo wa bahari na wenzake na kisha kwenye burudani ya harusi yay a Kiswahili. Jumuiya inayoshughulikiwa hap ani ya vijana wa pwani na changamoto zao za maisha. Japo matukio yanatokea pwani ambapo kuna wingi wa waumini wa dini ya Kiislamu, yaelekea mwandishi hajatilia hili maanani, na jamii husika ianaonekana kukengeuka kutokana na mitindo ya mavazi yao. Sherehe ya harusi katika CHAPTA uk 19, inadhihirisha mavazi ya uswahilini yaliyovaliwa na maharusi. Jumuiya hii ya vijana inakumbwa na changamoto tele za anasa na panda shuka za masuala ya mapenzi miongoni mwao. Katika uk 13-17, mwandishi anadhihirisha changamoto hizi za mahusiano ya kihorera ya kimapenzi na matokeo yake pale mhusika CHEEZY FRESHI anapochiwa watoto watatu aliyozaa na wasichana watatu tofauti na kukweka jukumu la kuwalea.

DJ BOIYE ni kijana wa mjini. Katika CHAPTA 27, uk 4-8, yupo mtaani na vijana wenzake tuko likihusu namna wanasiasa hutumia vijana vibaya wakati wa usakaji kura kuvua fujo na kutatiza amani mitaani. CHAPTA 33, uk 3-7, BOIYE, hupo sehemu ya pwani kufuatilia hali ya upigaji kura miongoni mwa vijana wa sehemu ya pwani. Mandhari ya uwepo wa bahari na minazi ni ushahidi tosha. CHAPTA 57, uk 3-9, BOIYE, yuko katika sehemu ya Kibera na Shujaa wa mtaani Bw. Odhiambo wakizungumzia mradi wa kuzoa taka ulioanzishwa na Bw. Odhimbo na wenzake kama njia ya kutoa huduma ya kujitolea kwa jamii na mafanikio ya mradi huo. DJ

BOIYE, yaelekea mwandishi hajampa makazi maalum kama ilivyo na wahusika wao wengine japo ni Dhahiri anaishi mjini Nairobi lakini haijabainishwa ni wapi. Mwandishi amemtumia sana katika kutoa matanzazo na katika ufafanuzi wa masula aina aina kwa wasomaji. Katika CHAPTA 109, uk 2-3, BOIYE na kijana NICK wanazungumzia kuhusu HUSTLE FITI, yaani biashara ya mtaani hasa ya upishi, katika SPECIAL EDITION 01/03 na 03/03, uk 8-9, anafafanua kuhusu suala la pendekezo la katiba. Katika karibu kila toleo matanzazo yote ni yeye anahusika. Kwa mfano CHAPTA 88, uk 15, 23. CHAPTA 98, uk 17-22 na 32. Jumuiya anayoilenga katika shughuli zote alizoshirikishwa ni jumuiya ya vijana. Jambo la kimsingi katika jumuiya hizi zote ni kuwa wanajamii wote wanatumia lugha ya Sheng. Wale wa mashambani, mjini, sehemu za mabanda na pwani wote wameunganishwa na lugha moja ya Sheng.

**5.5 Hitimisho**

Jambo linalojitokeza dhahiri ni kuwa *Shujaaz* ni fasihi inayojumuisha tanzu nyingine za fasihi na vipera mbalimbali vya tanzu hizi kama anavyo sema Pamela (2018) anapoeleza kuwa *Shujaaz* hubeba fasihi yote, kwa kuwa ndani mwake kuna *michongoano*, tawasifu, na hata tamthilia inayoigizwa kwa njia ya vibonzo. *Shujaaz* pia huwa na matumizi ya picha halisi za watu mashuhuri, huhusisha hadhira kupitia jumbe fupi za simu. Kutokana na matumizi ya vijana kama wahusika wakuu na maudhui yanayolenga Maisha ya vijana ni muhali kusema kuwa Shujaaz ni fasihi inayohusu vijana na inatosha kuinishwa kama fasihi ya vijana. Bila shaka baada ya uhakiki huu ni bayana kuwa Shujaaz ni kazi ya fasihi ya Kiswahili inayokidhi mahitaji na vigezo vyote vya uhakiki wa kazi ya fasihi.

# SURA YA SITA

## UPEKEE WA *SHUJAAZ* KAMA KAZI YA FASIHI

### 6.1 Utangulizi

Sura hii imejibana katika kuthathmini na kufafanua upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya kifasihi. Kila kazi ya fasihi ina upekee wake. Upekee kwa mujibu wa Kamusi Elezi (2016), ni hali ya kutokuwa na ingine kama hiyo. Kila mtunzi wa kazi ya fasihi huwa na upekee wake wa jinsi anavyoiandaa kazi yake na kuifanya iwe tofauti na ya watunzi wengine. Vigezo ambavyo vilivyofanikisha nia hii ya kutathmini sifa za kipekee katika *Shujaaz* vikiwa ni: maudhui, wahusika, ploti, mtindo, umbo, mandhari na lugha. Mihimili ya nadharia ya Metausasa ya upatanisho, kuporomoka kwa masafa, kubadilishana mawazo na ushirikiano na mwingiliano wa taaluma imetumiaka kuongoza utafiti ili kufanikisha madhumuni ya sura hii.

### 6.2 Maudhui

Maudhui katika *Shujaaz*, yako kama anavyoeleza Senkoro (1982) kuwa ni mawazo na mafunzo mbalimbali yaliyompa msukumo mtunzi au msanii hadi akaitunga kazi hiyo. Katika *Shujaaz* maudhui ni ujumbe wa msanii kwa hadhira kwa jinsi ambavyo msanii mwenyewe nanvyo kusudia hadhira yake wapate mafunzo na mawazo hayo. Katika uhakiki wa *Shujaaz* maudhui yameibua upekee ambao umejitokeza katika matoleo yake yote. Hasaa maudhui ya maisha ya vijana, changamoto katika maisha ya vijana, vijana na elimu, nafasi ya vijana katika jamii kisiasa, kijamii na kiuchumi, umuhimu wa vijana katika jamii, vijana na teknolojia ya mawasiliano na kadhalika.

Upekee uliopo hapa ni kuwa, wawasilishaji wa maudhui haya ni vijana ambao wao ndio wahusika wakuu na wasaidizi . Wahusika wengine ambao si wa umri wa ujana aidha wawe wazee au watoto wamapewa nafasi ndogo sana. Matoleo yote yanahusu vijana katika aidha masomo shuleni (MARIA KIM na MALKIA). Au mtaani (DJ BOIYEE, MARIA KIM, MALKIA na CHARLIE PELE). Au katika biashara (sehemu za HAUSTLE FITI na HUSTLA). Pia katika mahusiano ya kimapenzi na tamaduni za ndoa (MARIA KIM na MALKIA). Vilvile katika talanta mbalimbali za usanii au kazi (sehemu za CELEB, SHUJAA WA MTAA NA SHUJAA). Ama katika harakati za kisiasa na uongozi (DJ BOIYE, CHARLIE PELE). Katika ukulima na maisha ya mashabani na utamaduni wa jamii (CHARLIE PELE). Katika siasa (DJ


BOIYE, CHARLIE PELE na MARIA KIM) na katika matumizi ya teknolojia ya mawasiliano (DJ BOIYE). Jambo ambalo mtunzi wa *Shujaaz* hajalizingatia kwa hali yeyote ile ni suala la dini.

Upekee wa *Shujaaz* upo katika jinsi kazi hii zaidi inatumia wahusika wake. Karibu wote ni vijana. *Shujaaz* inalenga zaidi maisha vijana na kupatia wahusika wengine ambao huwepo katika jamii; watoto, wazee, maisha ya unyumba, maisha na nafasi za watu wa makamo na wazee au dini na itikadi za kidini nafasi ndogo sana. Hali hii nitofauti na ilivyo katika jamii na katika kazi kazi nyinginezo za fasihi zinazolenga vijana na kwa mfano, riwaya za Walibora kama vile *Kufa Kuzikana, Ndoto ya Almasi* na *Kidagaa Kimemwozea* au *Rosa Mistika* zake Kezilahabi. *Shujaaz* ina upekee wake.

Sababu ya upekee huu ni kuwa kazi hizi nyingine zilizotajwa na kazi nyingine kama hizo huwa ni fasihi zinazojumuisha maisha ya jamii kwa ujumla na kulenga wanajamii wote kuanzia watoto, vijana watu wa makamo na wazee. Lakini, katika *Shujaaz,* dhamira au nia na kusudi la mwandishi zinahusu vijana pekee. Kwanzia mwanzo hadi mwisho wa matoleo yote. Hadhira yake lengwa ni vijana. Ujumbe wake unahusu vijana, msimamo wake unahusu vijana, wahusika wake ni vijana, matazamo wake unahusu vijana, falsafa yake inahusu vijana, mafunzo anayoyatoa yanahusu vijana na lugha iliyotumiwa ya Sheng ni ya vijana, mbinu za lugha kama vile Mchongoano na Ujinga ni? zinahusu vijana. Karibu kila kitu kuhusiana na *Shujaaz* kinahusu vijana na mambo ambayo vijana hupenda au hujihusisha nayo. Rangi alizotumia bila shaka ni za kuvutia nadhari ya vijana. Mada anayo ishughulikia inahusu vijana.

Mwandishi wa *Shujaaz*, ameakisi maisha ya vijana kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika masuala ya kisiasa, mwandishi anaonyesha nafasi ya vijana katika siasa. Mfano ukiwa katika SPECIAL EDITION 01/03 na 03/03, na CHAPTA 27 ambapo ujumbe wa mwandishi ni kuwa vijana wanafaa kuchukua jukumu la kujihusisha katika siasa za nchi, iwe ni uundaji wa katiba au upigaji kura. Upekee uliopo katika *Shujaaz* ni kuwa mjadala kwa mfano kuhusu kubadilishwa kwa katiba nchini Kenya unawasilishwa siotu kwa njia ya ubunifu mbali pia katika hali halisi ya maswala ya mojakwa moja kama yalivyo kwenye pendekezo la katiba hiyo. SPECIA EDITION 01/03 na 03/03 uk 8-9 katika matoleo yote mawili kuna maswali ya hadhira kuhusu pendekezo la

marekebisho ya katiba na majibu kutoka kwa Kamati ya Wajuzi wa Marekebisho ya katiba nchini Kenya (Committee of Experts on Constitution Review). Katika mfano huu mambo kadha ya upekee wa kimaudhui katika kazi hii yanaibuka. Kwanza ni mwandishi kufanikisha maudhui yake ya vijana kuchukua nafasi yao katika siasa za nchi kwa kuwahusisha katika zoezi halisi la kuuliza maswahi moja kwa moja kwa wajuzi wa masuala ya kikatiba nchini. Pili, mwandishi amebomoa masafa yaliyopo baina yake na hadhira yake ambao ni vijana na masafa yaliyobaina ya vijana na taasisi za kiserikali na kuleta upatanisho unao lenga kufanikisha kuhusika kwa vijana katika kuirekebisha nakuimarisha nchi kisiasa.




**Kielelezo cha 82 kutoka SPECIAL EDITION 03/03 uk 8 na 9**

Kiuchumi, mwandishi wa *Shujaaz* amedhamiria kuhamasisha vijana kujituma bila ya kuchagua kushiriki katika kazi zozote hata zisizo kwa kuajiriwa kama vile kufungua vibanda vya vyakula, duka, saluni, kukuza talanta za mziki, uigizaji kuchora n.k, kushiriki katika kilimo biashara kati ya kazi nyinginezo. Mtazamo, msimamo na falsafa ya mwandishi ikiwa ni kuwa vijana wana uwezo wa kujiinua kiuchumi na kuinua jamii yote kwa jumla. Upekee wa *Shujaaz* hapa

unatokea katika matumizi ya wahusika halisi kama mifano ili kufanikisha maudhui haya. Kwa mfano, katika sehemu za CELEB na SHUJAA katika matoleo ya CHAPTA 57, 68, 78, 88, 93, 98, 102 na 109, mwandishi ametumia vijana mashuhuri katika jamii ili kufanikisha maudhui yake ya nafasi ya vijana katika kujitambua, kujituma na kufanikisha ndoto zoa zakuimarika kiuchumi kupitia talanta zao. Katika CHAPTA 109 sehemu ya HUSTLE FITI, CHAPTA 68 sehemu ya HUSTLA, mwandishi ametumia wahusika vijana walio hai kwa kutumia picha zao wakiwa katika maeneo yao ya kazi ili kuwapatia vijana mfano hai kwa nia ya kufanikisha ujumbe wake kwa vijana kuwa wanaweza kufaulu kiuchumi. Upekee huu haupo katika kazi nyingine za fasihi ambazo huzina mifano hai kwa hadhira. Matumizi ya picha za watu waliohai ni mtindo unao ipa kazi ya *Shujaaz* upekee kwani uhalisia wa mada husika unajitokeza wazi




wazi kwani hata mandahari yanayoandamana na picha hizi ni mandhari halisi wala si ya kubuni kama ilivyo katika ka nyingine za kibunifu.


**Kielelezo cha 83 kutokaChapta 57 uk 23**

Katika mfano huu uliopo katika CHAPTA 57, mwandishi ametumia wahiska wa kuchorwa na


wale walio hai. Uhalisia wa masimulizi unaonekana, vitendo hai na halisi vinaonekana, mandhari halisi yanaonekana kwa hivyo anayoyawasilisha msanii wa *Shujaaz* ni mambo yenye idhibati halisi katika maisha yakitendeka hivi kwamba msomaji habaki akitunga taswira ya mambo, anayaona waziwazi.

Kijamii, *Shujaaz* inadhihirisha masuala ya nayo wakabili vijana katika jamii katika maingiliano na mahusiano yao na wanajamii wengine hasa katika mazinjira ya kijamii, ujirani, kijijini au mataani na katika taifa mzima. Namna wanavyoishi, namna wanavyovaa, imani yao, tamaduni zao na itikadi. Kama anavyoeleza Msokile (1992), mawazo ya mwandishi kuhusu masuala ya kijamii yanadhihirisha msimamo, falsafa, mtazamo na ujumbe wake kuhusiana na jamii ya *Shujaaz* iliyo. Jumuiya zinazohusishwa katika *Shujaaz* ni zile za vijijini vikiwakilishwa ya Charlie Pele na wanakijiji chake mashambani, ya mtaa wa mabanda mjini ikiwakiliswa na Maria kim na DJ Boiye na wanajumuiya zao na jumuiya ya Pwani ikiwakilishwa na Malkia na jumuiya yao wakazi wa maeneo ya pwani. Katika jumuiya hizi mwandishi amejikita katika maisha ya vijana pekee. Katika matoleo ya Shujaaz yote mwandishi hajaangazia suala la unyumba. Maisha ya familia kamili ya baba, mama na watoto. Uwepo wa jamaa za wahusika (dada, kaka, ami, shangazi, babu, nyanya n.k) na kushirikishwa kwao katika masimulizi au matukio haupo. Huu ni upekee wa kazi hii. Suala la dini halijapewa nafasi kama ilivyo katika jamii ya kawaida.


Mwandishi amezamia zaidi katika mahusiano ya vijana ya kimapenzi na changamoto zake kama vile mimba ya mapema nje ya ndoa. anapendekeza mbinu za kuepukana na chamgamoto hii kwa kupendekeza matumizi ya mbinu za kupanga uzazi kama mbinu ya kuzuia mimba za mapema kwa vijana kwa kutembelea vituo vya ushauri na nasaha kuhusiana na mambo ya uzazi kama vile T- SAFE, FUTURE FAB na AMUA FAMILY PLANNING CLINIC.



**Kielelezo cha  84 kutoka Chapta 88  uk 13**




**Kielelezo cha 85 kutoka CHAPTA 33 uk15**



**Kielelezo cha 86 Chapta109 uk 11**

### 6.3 Wahusika

Huck (1979), wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika si lazima wawe binadamu. Wanaweza kuwa wanyama, mizimu, majitu, pepo, vibonzo au hata picha za watu halisi wanaopatikana katika kazi za kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika pia wanaweza kutambulishwa na maelezo ya mhusika msimulizi. Katika kuwatambua wahusika wake, mwandishi anaweza kutumia mbinu mbalimbali kama vile: kutueleza kuhusu mhusika huyo kupitia usimulizi, kurekodi mazungumzo ya mhusika huyo na wenzake, kueleza fikira za mhusika, kuonyesha fikira za wengine kuhusu mhusika huyo au kuonyesha mhusika akitenda mambo fulani.

Wahusika katika *Shujaaz* wametumika kwa njia ya kipekee iliyotofauti katika kazi nyingine za kifasihi. Sababu ikiwa ni kwamba, katika shujaaz kuna wahusika binadamu walio hai wanaokukilishwa na picha zao, kuna wahusika wa wakuchorwa na kunawahusika hadhira hai inayoshirikishwa katika kazi ya fasihi andishi. Hali hii ni tofauti na ilivyo katika fasihi nyingine kwani kwa mfano; katika tamthilia, riwaya, hadithi fupi, ushairi na hata novela, wahusika huwa wa kubuni na hutambulika kwa majina tu. Katika fotonovela wahusika huwa wahusika picha za watu, katika vitabu vya vibozo/ katuni, wahusika huwa wa kuchorwa. Lakini katika *Shujaaz* kama inavyopendekezwa na muhimili wa upatanisho katika nadharia ya metausasa imepatianishawahusika picha, wahusika wa kuchorwa na wahusika hadhira katika kazi moja. Hii ni hali inayoipatia hii kazi upekee wa kifasihi.

Kwa mfano katika Chapta 68 uk 12, ambapo wahusika walipo ni Charlie Pele ambaye amechorwa na Mhusika Joseph Barasa ambaye ni Mhusika picha. Barasa ni kijana anayefanya kazi ya ukulima kule Narok. Mhusika hai. Mwandishi hapa amekuza upekee wa kazi yake kwa kuunganisha sanaa tatu; ya picha, ya uchoraji na fasihi. Anafanya hivi pengine kuleta uhalisia katika kazi yake na kuchochea ukubalifu wa maudhui ya kazi kwa vijana kuwa ikiwa mwenzao anaweza nao pia wanaweza. Matumizi haya ya sanaa hizi tatu yanafanikisha juhudi za mtunzi za kuwasilisha maudhui kwani upatanisho huu na mwingiliano huu wa sanaa tofauti unafanya kazi iweze kuwa hai. Uhalisia wa kazi unajitokeza wazi zaidi. Yanayosawiriwa na kuakisiwa kutoka jamii ya mtunzi yanaonekana vyema na ujembe kueleweka kwa urahisi.


Matumizi ya sanaa hizi tatu yakiunganishwa na kuhusishwa kwa matumizi ya teknolojia kupitia mitandao ya kijamii na jumbe fupi za simu yanaipa kazi hii upekee usikuwepo katika kazi nyingi




za fasihi.

**Kielelezo cha 87 Kutoka Chapta 68 uk 10**

Mfano huu unapatikana katika Chapta 78, uk 8. Mtunzi amewaatumia wahuskia wawili; Dj Boiye ambaye ni mhusika wa kuchorwa na mhusika Liz Marami ambaye ni mhusika picha na mbaye vilevile mtunzi amembadilisha mhusika wa kuchorwa. Kuna upekee wa mtunzi hapa




kwani anambadilisha mhusika picha na kumfanya mhusika mchoro.

**Kielelezo cha 88 kutoka  Chapta 78 uk 8**

Mwandishi kupitia tukio hili anaonyesha ufundi wa kutumia picha na michoro katika kuwasilisha tawasifu ya mhusika kwa kutumia sanaa ya picha, michoro na maneno. Huu ni upekee unao boresha kazi kwa njia inayoonyesha weledi wa mtunzi katika Sanaa zote husika.

Mfano huu unapatikana katika Chapta 57, uk 5. Wahusika hapa ni DJ Boiye ambaye ni mhusika wa kuchorwa na Bw. Dalton Odhiambo ambaye ni mhusika picha. Tukio likiwa la kuhimiza vijana kuona uhalisia na uwezakano wa kujitolea mhanga kutoa huduma ya bure kwa jamii ili kuiboresha jamii bila kutarajia malipo. Mchangayo wa picha na mchoro hapa unafanya kazi ivutie na kukoleza upekee wake kuwa wahusika sio lazima wawe wa kubuni bali hata watu halisi katika jamii wanaweza kupewa nafasi ya uhusika katika kazi ya fasihi. Kazi ikiwa hivi



inavutia.

**Kielelezo cha 89 Chapta 57 uk 5**

Mfano huu nao unapatikana katika Chapta 93, uk 5. Mtunzi hapa amewatumia wahusika wa kuchorwa.  Tukio likihusu uwajibikaji kazini na umuhimu wa kujiepusha na unyayapaa dhidi ya matumizi ya mipira ya kuonana kimwili katika mapenzi kwani hali hii huhatarisha maisha ya




vijana kwa kuwafanya waogope kuitumia. Michoro hii na vitendo vya wahusika vinasisitiza ujumbe na akidhihirisha wake wa kuchora michoro wahusika ambao maneno yao yanashahibiana na vitendo vyao. Mchanganyo wa rangi ya mavazi ya wahusika unaipa kazi mvuto wa kipekee.

**Kielelezo cha 89 kutoka Chapta 93 uk 5**

Inabainika wazi kuwa mtunzi kwa kiwango fulani hutumia picha za watu halisi kwa masuala mengi ya kuhamasisha jambo kufanywa na anatumia michoro zaidi kupitisha jumbe za kuasa au kuonya mambo ambayo yanaonekana ni ya aibu au maovu katika jamii.

Mfano mwingine upo katika Chapta 27, uk 16 na umeendelea katika uk 17. Ambapo maoni ya hadhira



yapo.

**Kielelezo cha 90 kutoka Chapta 27 uk16-17**

Hapa kuna maoni ya wasomaji wa *Shujaaz* kuhusu mada anuai kama vile: uchaguzi wa amani, Partner mpoa ni yupi?, farming bila shamba, maji ni haki, mbona ujipate na partner player na nitahakikisha amani Kenya. Wahusika wakuu katika kazi ya *Shujaaz* ambao ni DJ Boiye, Maria Kim, Charlie Pele na Malkia wanapokea maoni ya mashabiki wao ambao kwa kufanya hivi wanashiriki uhusika wa kukuza ujumbe wa mtunzi wa kazi hii. Hadhira hii ambayo inatunukiwa uhusika inafanya hivi kupitia kutuma maoni yao kupitia teknolojia ya mawasiliano ya simu kwa kutuma ujumbe kupitia numbari 20308 bila kugharamika kwani hawalipi kutuma ujumbe. Upekee hapa unajitokeza katika kuhusisha hadhira kuendeleza maudhui kupitia teknolojia. Kwa hivyo mtunzi ametumia wahusika wa kiteknolojia.

## 6.4 Ploti

Wamitila (2002), ploti ni mpangilio ya vitendo katika hadithi. Hiki ni kipengele muhimu cha kimuundo katika hadithi yoyote ile. Huwa ni mfuatano wa matukio yanayopatikana katika kazi ya kifasihi kwa kutegemea uhusiano wake kiusababishi. Ploti hueleza kile wanachotenda wahusika na kile kinachotendeka kwao. Ni uzi ambao huunganisha hadithi pamoja kuanzia mwanzo hadi mwisho na ndio humfanya msomaji atake kuendelea kusoma hadi hatima yake. Ploti iliyoundwa vizuri ni hai na inaingiliana, hukua kimantiki kutokana na matendo na uamuzi wa wahusika katika hali fulani.

*Shujaaz* kama ilivyo kazi nyingine za fasihi kama vile ya riwaya, tamthilia, ushairi, novela au hadithi fupi huwa na ploti yake. Kila toleo au Chapta huwa na sehemu kadha tofauti mfano wa diwani ya hadithi fupi kula sehemu ikiwa na wasuhika wake tofauti na matukio tofauti. Kila sehemu hata ingawa inahusu mhusika mkuu yule yule huwa ni tofauti. Kwa mfano katika Chapta 58, kuna sehemu saba: sehemu ya Charlie Pele inayohusu *KU-SOLVE GHARAMA YA MAI*, sehemu ya Malkia inayohusu *#BAE MILELE*, sehemu ya Maria Kim inayohusu *LOVE LETTER SHULENI*, sehemu ya tawasifu ya msanii Govi au Lemuel King Malik, sehemu ya DJ Boiye inayohusu *#LIGISAFI, JANTA CHALLENGE na JIACTIVATE*, sehemu ya Maria Kim inayohusu *MSEE WA MAANA CHALLENGE*, sehemu ya Maria Kim nyingine inayo husu *WAREMBO WA CHUXX*. Katika mfano huu kuna sehemu tatu tofauti za Maria kim katika toleo moja. Mhusika mkuu ni yule yule katika sehemu hizi tatu lakini matukio na maudhui ni tofauti lakini yote hayo katika toleo lilelile moja na haya husiani. Huu ni kupekee wa mtunzi. Upekee mwingine ni kuwa katika mwisho wa kila sehemu mtunzi anatoa fursa kwa msomaji au hadhira

kujumuika katika usimulizi kwa kutoa maoni yake kuhusu mada husika katika kila sehemu kupitia kutuma ujumbe mfupi wa simu kupitia 20308 au 22699. Kwa mfano uk 7, 9, 15, 21, 25 na 31. Kila toleo huwa na hali hii ya kutokuwapo kwa matukio ya toleo moja ambayo yanaendelezwa katika toleo linalofuta. Matoleo yote yanajisimamia kimatukio na hata kiwahusika hivi kwamba si lazima kila toleo lishirikishe wahusika wale wanne wakuu. Mkunzi hawezi kutabirika ni yapi na ni mhusika yupi mkuu atahusisha katika toleo linalofuata. Hali hii inadhihirisha upekee ambao ni tofauti na ilivyo katika matoleo mengine ya fasihi ambayo hutumia wahusika walewale mfano ukiwa kitabu cha vibonzo cha *Juha kalulu* au *TinTin.*

Ni katika matoleo maalum  Special Editions 01/03 na 03/03 ambapo matukio yanaendelea kutoka toleo moja hadi lingine.  Matoleo haya mawili pia yanasehemu ya kipekee inayohusu maswali ya wasomaji kuhusu maswali ya uundaji katiba mpya na majibu yanayotolewa na wataalam ya kikatibu katika uk 8-9 katika matoleo hayo mawili. Katika jalada la matoleo haya kuna michoro ya wahusika wale wakuu wanne. Sehemu ya kwanza ni ya BOYIE (uk2-4) katika matoleo yote mawili. Sehemu ya pili katika matoleo yote mawili ni ya MALKIA (uk 5-7). Kisha inafuata sehemu kuhusu masuala na maoni kuhusiana na pendekezo la katiba mpya 2010 (uk 8-9). Sehemu inayofuta katika matoleo haya mawili ni ya CHARLIE PELE (uk 10-12). Kisha inafuata sehemu ya MARIA KIM (uk 13-15) katika matoleo yote mawili. Katika ukirasa wa mwisho kuna tangazo la kampuni ya Safaricom katika matoleo yote mawili.  Upekee uliopo hapa ni kuwa matoleo haya yana idadi sehemu sawa, kila sehemu ikiwa na idadi sawa ya kurasa, kila sehemu ikihusu wahusika wakuu sawa, kila sehemu ikihusu mada sawa, na matoleo yote mawili yakiwa na idadi sawa ya kurasa 15. Hali hizi si jambo la kawaida katika kazi za fasihi.

### 6.5 Mtindo

Wamitila (2002), anaelezea mtindo kama dhana inayotumiwa katika uchambuzi wa fasihi kuelezea jinsi au namna mwandishi anavyounda kazi yake. Anaongezea kuwa mtindo hurejelea mazoea ya mwandishi au msanii fulani ya kuandika ambayo huhusisha: usimulizi wake, uteuzi wa msamiati, tamathali anazotumia, lugha yake, jinsi anavyomalizia hadithi yake, mpangilio wa matukio, taswira, usawiri wa wahusika na majina yao. Mtindo huaakisi njia ya mwandishi au msanii anayehusika ya kutazama masuala: ni njia ya kuiwasilisha na kuifumbatia tajriba yake, kuupanga na kuuwasilisha uelewa au ung'amuzi wake. Mtindo mzuri ni ule unaooana na ploti, maudhui, mandhari na  wahusika.  Arbothnot  na  Sutherland  (1974),  mtindo huhusu uteuzi

wa maneno, aina za sentensi, mpangilio wa maneno katika sentensi, ruwaza katika sentensi na matumizi ya tamathali za usemi.

Katika *Shujaaz* mtindo uliotumika ni ule wa paneli za vibonzo uliochanganywa na sehemu zifuatazo:

(i) Sehemu za fasihi simulizi kama vile ‘Mchongowano’ na ‘Ujinga ni’.

(ii) Sehemu za kamusi ya Sheng (Sheng Dictionary).

(iii) Sehemu za matangazo ya kibiashara


(iv) Kuna sehemu za CELEB ambazo zinahusu tawasifu za vijana ambao ni watajika katika jamii kutokana na talanta walizo nazo na ni mfano bora wa kuigwa na vijana

(v) Kuna sehemu za SHUJAA au SHUJAA WA MTAA, sehemu ya HUSTLE FITI na ile ya HUSTLA ambazo zinahusu vijana waliofaulu kwa kushiriki biashara, kilimo biashara au kushiriki katika huduma za kujitoa mhanga katika jamii

(vi) Kila sehemu inayohusu wahusika wakuu BOYIE, MALKIA, CHARLIE na MALKIA zinamwisho maalum unaohushisha hadhira kwa kuwaomba washiri mada ya tukio husika kupitia jumbe fupi za simu zisizo lipiwa.

(vii) Katika baadhi ya matoleo kuna sehemu za maoni ya hadhira kuhusu mada tofauti.

Mambo haya hayapatikani katika riwaya, tamthilia, hadithi fupi, ushairi, foto novela au kazi




nyingine za fasihi. Ni dhahiri kuwa *Shujaaz* inaupekee wake kimtindo.

**Kielelecho cha 92 kutoka Chapta 93 uk 32**





**Kielelezo cha 93 chapta 109 uk 23**



**Kielelezo cha 94 Chapta 33 uk 20**




**Kielelezo 95 kutoka Chapta 93 uk 31**



**Kielelzo cha 96 kutoka Chapta 57 uk 25**

### 6.6 Umbo la *Shujaaz*

Cass (1967), Umbo la kitabu linarejelea jinsi kitabu hicho kinavyoonekana; wajihi wa kitabu hicho. Umbo la kitabu hujumlisha mambo kama vile ukubwa wake, muundo/ umbo, vielezo, taipografia, ubora wa karatasi na ujaladashaji unaotumiwa ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi. Shujaaz ina upekee wa umbo kwani umbo lake ni tofauti na lile la tanzu nyingine za fasihi andishi ambazo huwa na mpangilio maalum na kuhusisha sehemu kama utangulizi, yaliyomo, orodha ya wahusika na kadhalika.




**Kielelezo cha 97 kutoka Chapta 109 uk 1- Jalada**

Kila toleo la Shujaaz huwa na jalada tofauti hata anwani ilibadilika kutoka [www.Shujaaz.fm](www.Shujaaz.fm) hadi *SHUJAAZ.* Kilicho dhahiri katika jalada ni matumizi ya picha za watu mashuhuri ambao tawasifu zao hutolewa katika sehemu za ndani mwa toleo husika hasaa katika sehemu ya CELEB. Katika mfano huu wa Chapta 109 mhusika mashuhuri aliyetumika ni Dr. Ofweneke mwigizaji mashuhuri wa michekesho. Jalada huwa na mada zinazojadiliwa katika sehemu tofauti katika

toleo husika. Kuna matumizi ya rangi anuai tofauti katika kila toleo japo rangi katika anwani imekolezwa wekundu kama inavyo onekena katika mfano wa Chapta 109 uliotumika hapa.

Mbali na upekee wa jalada katika *Shujaaz*, upekee mwingine unajitokeza katika ukubwa wa matoleo. Kuna yale yenye kurasa 24 na kuna yale yenye kurasa 32. Ukubwa huambatana na idadi ya sehemu katika toleo husika. Matoleo ya kurasa 24 yaweza kuwa na sehemu sita kama ilivyo katika Chapta 109 au sehemu tano kama ilivyo katika Chapta 78. Matoleo ya kurasa 32 yaweza kuwa na sehemu nane au saba kama ilivyo katika Chapta 98 na 78 mtawalia. Yaani Shujaaz haina idadi maalum ya sehemu zilizomo. Huu ni upekee anaoutumia mtunzi kuondoa uradidi wa mambo na kuifanya kazi isiwachoshe hadhira hasa ambao ni vijana. Kila toleo pia halina sehemu ambazo lazima ziwepo katika kila toleo. Kuna matoleo yaliyo na sehemu zote za wahusika wakuu yaani sehemu za; Maria Kim, DJ Boiye, Charlie Pele na Malkia. Matoleo mengine kama Chapta 78 na 109 hazina sehemu ya Charlie Pele. Katika Chapta 98 Maria Kim amepatiwa sehemu tatu.

Lugha ilimepangwa katika vibofu wa maneno kama ilivyo katika kazi ya katuni na fotonovela. Maneno yakiwa wameendelezwa kwa herifu kubwa. Rangi tofauti na maumbo tofauti ya vipofu vya maneno kutegemea msisitizo na kiimbo hisia mtunzi anayotaka kuwasilisha. Mfano ukiwa katika Chapta 103 uk 12. Kuna sehemu ambapo maelezo yanatolewa bila matumizi ya vipofu vya maneno na maadishi ya nadhari kutumika. Kwa mfano katika Chapta 93 uk 23. Na katika Chapta 88 uk 16.


**6.7 Mandhari**

Cass (1967), Matendo yoyote ambayo hutokea katika kazi za kifasihi hufanyika mahali fulani na wakati maalumu. Hiki ndicho kinachoelezwa kama mandhari. Ni muhimu kuwa matendo yanatendeka katika uelewa na tajriba ya hadhira. Kila sehemu katika *Shujaaz* huakisi mandhari maalum inayoafiki jumuiya lengwa katika wakati maalum. Kuna mandhari ya kubuni na mandhari halisi katika *Shujaaz*. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya mandhari ya kubuni kama ilivyo katika sehemu zinazohusiana na wahusika wakuu wa *Shujaaz.*

Kwa mfano, DJ Boiye huwakilisha jumuiya na mjini katika makazi ya mabanda au viunga vya miji. Kwa mfano, katika Chapta 27 uk 4-9 mandhari ni viunga vya mji kwani majengo ni

machache, Wakati ni wa kampeni za uchaguzi na hadhira ni vijana ambao sana sana hujitokeza katika karakati za kampeni. Viongozi waomba kura wakiwa juu ya magari yao ya kifahari kuwahutubia wafuasi na umma uliojongea kuwasikiza. Mfano mwingine ni katika SPECIAL EDITION 03/03 UK 2-3 ambapo BOIYE yupo katika mazingira ya mjini na vijana wenzake.




**Kielelzo cha 98 na 99 kutoka SPECIAL EDITION 03/03 uk2 na 3**

Mhusika Malkia sehemu zake hutukia sehemu ya pwani kwani kuna minazi na mavazi ya wahusika pia huashiria utamaduni wa watu pwani. Kwa mfano katika Chapta 109 uk 18 – 20. Matukio yakiashiria maisha ya jamii ya kisasa iliyokengeuka japo imedumisha mila kama za ndoa za kitamaduni. Mifano mingine inayodhihirisha mandhari ya pwani ni yale ya MALKIA akiwa shuleni (CHAPTA 88 uk 6) na pia sehemu ya ufuo wa bahari (CHAPTA 109 uk 15). Mandhari haya ya pwani yanaashiria maisha ya raha na anasa na maadhi ya matokeo ya kushiriki raha hizo. MARIA KIM anasawiliwa akiwa mkazi wa sehemu za mabanda na sehemu zake zinatokea akiwa katika mitaa ya mabanda au akiwa shuleni Jongo High School ambayo ipo katika sehemu za mabanda. Majengo mengi yaliyosongamana yanaonekana maeneo amamoishi. Kwa mfano katika Chapta 98 uk 10- 15 MARIA KIM yuko shuleni na mandhari ni ya shuleni kwani wanafunzi wamevaa

sare za shule na wako Jongo High School. Matukio yaliyopo ni ya jumuiya ya wanafunzi kwani migororo iliyopo kama ya barua za mapenzi ni jambao la kawaida katika shule za upili, uwepo wa walimu wakitoa maagizo pia huonyesha urasmi wa mambo. Wahusika vijana wanapitia




changamoto za kimapenzi wangali shuleni jambo ambalo hutatiza umakini wao masomoni. Katika sehemu yake uk 23-25 na 26-31 Maria kim yu mtaani na mambo anayoshughulikia yanahusu changamoto za jumuiya husika ya vijana na matatizo yao kuhusiana na maswala ya mapenzi na mbinu za kupanga uzazi za kuzuia ujauzito kabla ya ndoa.


**Kielelezo cha 100 kutoka Chapta 88 uk 6**



**Kielelezo cha 101 kutoka Chapta 109 uk 15**




**Kielelezo cha 102 kutoka CHAPTA 98 uk12**



**Kielelezo cha 103 kutoka CHAPTA 57 uk13**

Sehemu za Charlie Pele zinatokea sehemu za mashambani ambapo shughuli za ukulima na sherehe za kitamaduni hutokea huku mazingira yakiwa na makazi machache yaliyotawanyika. Jamii ya mashambani hushirikiana na hata huhusisha chifu wa eneo. Kwa mfano katika Chapta 98 uk 4-7. Matukio mengi yakihusu ufugaji na ukulima kwa mfano Chapta 27 uk 25-30 ambapo jamii husika inahangaishwa na uuzaji wa mbegu ambazo hazijadhibitishwa na kupitishwa na mashirika ya kiserikali kuwa na ubora ufaao. Jambo hili likiashiria ukosefu wa maafisaa wa kilimo ambao wangeweza kuwachukulia hatua watu wanaowalagai wakulima kwa kuwauzia mbegu bandia. Uwepo wa nyumba za udongo zilizoezekwa kwa nyasi zikiashiria hali ya umaskini katika sehemu za mashambani. Ukosefu wa maendeleo unadhihirika wazi. Hali ya maisha ya watu hapa ni ya chini mno. Umaskini umekita mizizi hapa. Pia kuna uwepo wa shughuli za kilimo na mahusioano ya ushirika wa wanajamii. Mifano mingine ipo katika SPECIAL




EDITION 03/03 uk 10 na CHAPTA 12 uk 24.


**Kielelezo cha 104 kutoka SPECIAL EDITION 03/03 uk 10**





**Kielelezo cha 105 kutoka CHAPTA 12 uk 24**

Upekee ya mandhari unajitokeza katika mandhari halisi ambayo yanawasilishwa kwa njia ya picha za mazingira halisi ya pale matukio yanapotokea. Picha hizi vile vile uhusisha uwepo wa watu halisi huku wakizungumza na mhusika wa kuchorwa. Huu ni upekee ambao haupatikani katika fasihi za kubuni. Mfano ni katika CHAPTA 57 uk 3-8, mandhari hap ani hali halisi katika sehemu ya mabanda ya Kibra katika viunga vya Mji mkuu wa Nairobi. Vyumba vya mabanda vilivyosongamana vinaonekana, uchafu uliotapakaa kwoke unaonekana wazi wazi. Si mambo ya kufikirika au kupigia taswira unayaone kama yanavyosimuliwa na wahusika.

Mfano mwingime ni uliokatika CHAPTA 68 katika uk 10-15, mandhari ni katika picha halisi ya shamba la viazi kule Narok. Mhusika mkulima aliyepigwa picha na mhusika wa kuchorwa wanaeleza kuhusu ukulima wa viazi. Picha halisi ya shamba na pia viazi vilivyovunwa vinaonekana. Ua la shamba pia linaonekana kama ilivyo shambani. Huu ni upekee ambao huwezi kuwapo katika mandhari ya kubuni.




**Kielelezo cha 106 kutoka CHAPTA 57 uk8**




**Kielelzo cha 107 kutoka Chapta 68 uk14**

## 6.8 Lugha

Coobes (1953), Fasihi haiwezi kuchunguzwa bila kuzingatia matumizi ya lugha. Mwandishi ni lazima azingatie vipengele vinavyofanya kazi ya sanaa iwe ya kuvutia kwa kutumia lugha kwa ustadi. Ni kupitia lugha ambapo umaarufu wa mwandishi unakadiriwa. Mwandishi wa *Shujaaz* ametumia lugha ya Sheng ambayo vijana hujitambulisha kwayo na hivyo kutokuwa na taabu wanapoitumia. Wahusika karibu wote wadogo kwa wakubwa  wanatumia Sheng katika kuwasiliana. Lugha yenyewe ni nyepesi isiyo na matumizi ya tamathali za usemi sana ili kudumisha wepesi wake. Wepesi huu unanuia kuepuka kuchosha hadhira lengwa. Sehemu kadha wa kadha kuna matumizi ya lugha sanifu na kuchanganya Kiswahili sanifu na Kiingereza sanifu. Kwa mfano katika Chapta 27 uk 4- 9 hali hizi zinadhihirika.

Upekee wa *Shujaaz* katika lugha iliyotumika ni kuwa hakuna kazi nyingine ambayo huenda imeandikwa kwa lugha ya Sheng. *Shujaa*z ni ya kipekee. Kwa kuandikwa kwa Sheng na hata kuwepo kwa kamusi ya Sheng ni jambo ambalo ni la kipekee katika utunzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili. Sheng iliyotumika inajumuisha maneno au msamiati wa mtaani usiolazimishwa, Kiswahili kilichochanganywa na kiingereza na uhamishaji wa msimbo katika sehemu mbali mbali. Matoleo yote ya *Shujaaz* ametumia lugha ya Sheng kuwasilisha ujumbe wake. Ifuatayo ni mifano ya jinsi lugha ilivyotumika katika Shujaaz. Kuna kuhamisha na kuchanganya msimbo




na sheng.

**Kielelezo cha 108 kutoka CHAPTA 109 uk 11**



**Kielelezo cha 109 kutoka CHAPTA 27 uk 20**

Katika mifano hii wahusika wanachanganya msimbo kwa kuchanganya Kiswahili sanifu na maneno ya Kiingereza ka vile : Oh! No!, please, hard, late, food, sanitary towels, hard, walk, aunt, life first born, dropout na fees. Bali na kuchanganya na Kiingereza wahusika hawa wamatumia maneno ya Sheng kama vile: Keja yake (chumba chake), sijui kama niko na ball (sijui kama nimeshika mimba), siz sasa nta do nini (dadangu sasa nitafanya nini), Ilikuwa hard sana (hali ilikuwa ngumu sana), time zingina alikam late na lala bila food (wakati mwingine alikuja amechelewa sana usiku na nililala bila kula chakula), ningepata za madem (ningepata vitu wanazohitaji wasichana) ilibidi siste (ilibidi dadangu). Huenda ikawa *Shujaaz* ndiyo kazi pekee ya fasihi yenye upekee huu ambapo lugha inayotumiwa na wahusika ni hii iliyochanganya Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

**6.9 Dhana ya Ujanibishaji wa upekee wa *Shujaaz*.**

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), ujanibishaji ni mchakato wa kubadilisha au kurekebisha kazi fulani ili iwiane na mazingira, tamaduni, lugha na hulka za jamii husika. Ni dhana au mbinu ya fasihi inayohusu kujibainisha kwa lugha, tamaduni na mazingira ya kijamii ya jamii husika. Pamela Ngugi (2016) anaongeza kuwa ujanibishaji wa fasihi ya Kiswahili ni kitendo cha kufanya maandiko yaeleweke na yakubalike kijamii kupitia lugha na wahusika wanaoakisi jamii. Kutokana na maelezo hay ani wazi kuwa dhana ya ujanibishaji ni kigezo mwafaka cha kudhihirisha upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ya Kiswahili.

*Shujaaz* hujanibishwa kama fasihi ya Kiswahili kwa kutumia wahusika, lugha na mtindo, mandhari, maudhui na dhamira, muundo na wingimuundo (multimodality) na ushirikishi wa wasomaji na athari za kijamii. Vigezo hivi ndivyo vinafanikisha udhihirishaji wa upekee wa fasihi kama kazi ya fasihi kwa namna ifuatavyo:

**1. Wahusika**

Katika fasihi, wahusika ndio roho ya kazi yoyote ya kifasihi kwa sababu kupitia wao simulizi hufanyika na ujumbe huwasilishwa. Msokile (1992) anasisitiza kuwa ujenzi wa wahusika hutegemea mahusiano yao na jamii, lugha wanayotumia na nafasi wanazochukua katika simulizi.

Katika fasihi ya Kiswahili ya kiasili, wahusika mara nyingi hujengwa kama vielelezo vya maadili au mifano ya tabaka maalumu la kijamii. Kwa mfano, katika riwaya za Shaaban Robert kama *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*, wahusika hujengwa ili kuakisi falsafa na maadili ya jamii, na si lazima waonekane kama watu wa kawaida wa mitaa au maisha ya kila siku. Vivyo hivyo, katika tamthilia za Penina Muhando kama *Hatia* au *Mashetani* ya Ebrahim Hussein, wahusika hujengwa kwa misingi ya mgongano wa kijamii na kisiasa, na mara nyingi hubeba ujumla wa fikra za jamii badala ya maisha ya mtu mmoja mmoja.

Hata hivyo, *Shujaaz* hujitokeza kwa upekee kupitia ujanibishaji wa wahusika wake. Wahusika wa *Shujaaz* ni vijana wa kawaida, wanaopambana na changamoto za kijamii na kiuchumi katika mazingira yanayofahamika na vijana wa Kiswahili. Kwa mfano, DJ BOYIE anawakilisha kijana wa mtaa mwenye ndoto kubwa ya kuwa msanii lakini anayeishi maisha ya kawaida yenye changamoto za ajira na mitandao ya kijamii. Boyie ni mfano wa kijana anayechangamkia biashara ndogo ndogo ili kujikimu, huku Malkia akionesha changamoto za wasichana wa mijini katika kusawiri nafasi ya elimu na uhuru wa kiuchumi.

Kwa mujibu wa Pamela Ngugi (2018), ujanibishaji katika wahusika wa fasihi ya vijana hupatikana pale wanapowekwa karibu na maisha ya kila siku ya hadhira inayolengwa. Wahusika wa *Shujaaz* si vielelezo vya falsafa ya jumla, bali ni kioo cha maisha ya vijana wanaosoma magazeti hayo. Hii huwafanya washiriki moja kwa moja katika simulizi kwa sababu wanaona maisha yao yakionekana hadharani.

Tofauti kuu kati ya *Shujaaz* na kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili ni kwamba wahusika wake huchorwa kwa lugha ya mtaa na tamaduni za sasa. Wamitila (2002) anabainisha kuwa ujanibishaji wa fasihi hujidhihirisha kupitia lugha, tabia na mitindo ya wahusika. Katika *Shujaaz*, wahusika huongea Sheng, huvaa mitindo ya kisasa, hutumia simu za mkononi na mitandao ya kijamii, na hukabiliana na changamoto zinazofanana na zile za wasomaji wao. Hii inawaweka karibu zaidi na msomaji kuliko wahusika wa riwaya za kihistoria kama *Utengano* (Said Ahmed Mohamed) ambao mara nyingi huonesha vijana kama wahanga wa mabadiliko ya kijamii lakini si kama washiriki wa kila siku wa maisha ya mtaa.

Kwa hivyo, ujanibishaji wa wahusika katika *Shujaaz* huibua upekee wake kwa njia zifuatazo:

1. **Wahusika kama watu wa kawaida** – si vielelezo vya falsafa au mifano ya maadili tu, bali watu wa mitaa wanaoishi changamoto na furaha za kila siku.
2. **Lugha na tabia za uhalisia** – wahusika huongea Sheng, huishi mitaa inayojulikana, na kushughulika na mambo yanayowagusa wasomaji (ajira, mitandao, muziki).
3. **Wingimuundo (Multimodality)** – wahusika hawa hawapatikani kwenye maandiko pekee, bali pia huishi kwenye redio na mitandao ya kijamii, jambo linalowafanya waonekane "halisi" zaidi.
4. **Ushirikishi** – wasomaji wanaweza kuwasiliana na wahusika kupitia SMS, WhatsApp au Facebook, na mara nyingine kupata majibu, hali ambayo hufuta mipaka kati ya "mtunzi" na "msomaji."

Kwa kulinganisha, wahusika katika fasihi nyingine za Kiswahili (riwaya, tamthilia) mara nyingi huchorwa kama mifano ya kijumla ya jamii au kama vielelezo vya maadili. Upekee wa *Shujaaz* unadhihirika kwa kuwa wahusika wake hawajengi "mfano wa kijumla" tu bali huonekana kama vijana wa kweli wanaoishi katika mitaa ya leo.

**2. Lugha na Mtindo**

Lugha na mtindo ni nyenzo kuu katika kazi yoyote ya fasihi kwa sababu ndizo hufikisha ujumbe, kuunda wahusika na kuibua hisia za hadhira. Kwa mujibu wa Senkoro (1982), lugha ya fasihi hujengwa kwa umbo la kisanaa na mara nyingi huchaguliwa ili kuendana na maudhui, wahusika na mazingira ya kazi husika. Katika fasihi ya Kiswahili ya jadi, hasa riwaya na tamthilia, lugha ya Kiswahili sanifu imepewa nafasi ya juu kama ishara ya kuonesha umakini wa kifasihi na kuimarisha heshima ya lugha. Kwa mfano, katika riwaya za Shaaban Robert, lugha ni ya fasihi ya juu, yenye methali na semi za kifalsafa ambazo zilibeba mafunzo ya kijamii. Vilevile, katika tamthilia za Ebrahim Hussein, lugha hubeba mijadala ya kifalsafa na kisiasa kwa Kiswahili sanifu na kwa mtindo wa kisanaa unaojikita katika utendaji wa jukwaa.

Hata hivyo, *Shujaaz* hujitokeza kwa upekee kwa kutumia lugha ya mtaa (Sheng) pamoja na Kiswahili cha kila siku kama sehemu ya ujanibishaji. Pamela Ngugi (2018) anaeleza kuwa fasihi ya vijana hupata nguvu pale inapojenga lugha kwa msingi wa uhalisia wa vijana wenyewe. Hii ni kwa sababu lugha ndiyo ishara kuu ya utambulisho wa kijamii. Kwa kutumia Sheng, *Shujaaz*

hujanibisha maisha ya vijana wa mijini, hususan wale wanaoishi mitaa ya Nairobi, Mombasa na Kisumu, ambapo Sheng ni lugha ya mawasiliano ya kila siku.

Upekee wa *Shujaaz* ni kwamba Sheng hutumika si kama kionjo tu, bali kama lugha kuu ya kufanikisha simulizi. Wahusika huzungumza Sheng katika mazungumzo ya kawaida, na maneno hayo hubeba vicheko, utani, majonzi na changamoto zao. Kwa mfano, msichana anapojadili changamoto ya mapenzi, hatumii Kiswahili sanifu, bali Sheng na maneno ya mtaa yanayofanya msomaji ajione yumo katika mazungumzo hayo.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mtindo katika fasihi hujidhihirisha kupitia uchaguzi wa lugha, sauti na muundo wa simulizi. Katika *Shujaaz*, mtindo wake ni wa kipekee kwa sababu:

1. **Ni wa kijana kwa kijana** – simulizi huonekana kana kwamba vijana wanaongea na wenzao, si kama mtu mzima anawahubiria vijana.
2. **Ni wa haraka na wa picha** – maandiko ni mafupi, yanayoambatana na katuni na picha, jambo linalolingana na utamaduni wa usomaji wa vijana wa karne ya 21 ambao huchagua taarifa fupi na za haraka.
3. **Ni wa mchanganyiko wa lugha** – Sheng, Kiswahili sanifu, na hata Kiingereza cha mitaani huunganishwa, hali inayoakisi mawasiliano ya kila siku ya vijana.

Tofauti kuu na fasihi ya Kiswahili ya kiasili ni kwamba lugha ya *Shujaaz* haijengi heshima ya kifasihi ya "lugha ya juu," bali hufuata uhalisia wa lugha ya kila siku. Msokile (1992) anabainisha kuwa ujanibishaji unamaanisha kufanya fasihi izingatie utamaduni, lugha na mitindo ya jamii inayolengwa. Hivyo basi, kutumia Sheng na Kiswahili cha mitaani si kuipunguzia fasihi hadhi, bali ni kuipa nguvu ya uhalisia na ushirikishi.

Zaidi ya hapo, mtindo wa *Shujaaz* hubuniwa kwa mfumo wa katuni na mazungumzo ya moja kwa moja. Kwa mfano, badala ya maelezo marefu ya kinarratori, simulizi huoneshwa kupitia mazungumzo mafupi kati ya wahusika, yaliyoambatanishwa na michoro ya katuni. Mtindo huu hujanibisha utamaduni wa vijana wa sasa wanaotumia mitandao ya kijamii, ambapo ujumbe hufikishwa kwa maandiko mafupi, picha, emoji na video.

Kwa hivyo, lugha na mtindo wa *Shujaaz* huonesha upekee wake kwa njia zifuatazo:

- **Kipekee kwa kutumia Sheng kama lugha ya fasihi** – si kama “kivuli” cha lugha ya Kiswahili, bali kama lugha yenyewe ya kazi.
- **Mtindo wa mazungumzo mafupi na picha** – unaolingana na mienendo ya mawasiliano ya vijana wa karne ya 21.
- **Mchanganyiko wa lugha** – Kiswahili, Sheng na Kiingereza huunganishwa kama ishara ya ujanibishaji wa mtaa wa sasa.

Kwa kulinganisha, fasihi ya Kiswahili ya awali hutumia Kiswahili sanifu, lugha yenye methali, semi na hoja ndefu, huku mtindo wake ukijikita katika simulizi za kifalsafa au ujenzi wa hoja za kisiasa. *Shujaaz*, kupitia ujanibishaji wa lugha na mtindo, hubadilisha mkondo huu na kuonesha upekee wake wa kisanii na kijamii.

**3. Mandhari**

Katika fasihi, mandhari (setting) ni kipengele cha kimsingi kinachoamua uhalisia wa kazi ya kifasihi. Kwa mujibu wa Msokile (1992), mandhari hujumuisha mazingira ya kijamii, kijiografia na kihistoria ambapo wahusika huishi na matukio hutendeka. Mandhari hubeba falsafa ya jamii na hulisha uhalisia wa kazi. Katika riwaya na tamthilia za Kiswahili za awali, mandhari mara nyingi yalikuwa ya kijijini au miji ya kihistoria (kama vile Lamu, Zanzibar, Mombasa), yakiwa yamezungukwa na bahari, dini na utamaduni wa Kiswahili wa mwambao. Shaaban Robert, kwa mfano, alitumia mandhari yenye rangi ya kifalsafa na mazingira ya kidini, huku Ebrahim Hussein akichora picha ya jamii ya miji inayopambana na migongano ya kisiasa na kijamii.

*Shujaaz* hujitokeza kwa upekee wake katika mandhari kwa kutumia miji na mitaa ya sasa – yaani maeneo halisi ya vijana wa Kisasa. Mtaa wa Nairobi, Mombasa, Kisumu na hata mitaa midogo midogo yenye changamoto za ajira, mitandao ya kijamii, muziki wa kizazi kipya, na biashara ndogondogo ndizo maeneo ambayo hadithi hufanyika. Pamela Ngugi (2018) anasisitiza kuwa fasihi ya vijana lazima ijanibishe uhalisia wa vijana hao kwa kuchukua mandhari wanayoishi na kuyafanya kuwa sehemu ya kazi ya fasihi.

Upekee wa mandhari katika *Shujaaz* ni kwamba:

1. **Ni ya kisasa na ya kila siku** – sehemu zinazotumika si za kigeni wala za kifalsafa, bali ni nyumba ndogo za mitaani, studio za muziki wa wasanii chipukizi, vijiwe vya boda boda, sokoni, kwenye mitandao ya kijamii, na hata mitaa ya geto.
2. **Ni mandhari ya teknolojia na mitandao** – *Shujaaz* huchukua simu janja, WhatsApp, YouTube, na Facebook kama sehemu za matukio ya hadithi. Mazungumzo ya wahusika mara nyingi hutokea kupitia simu na mitandao ya kijamii.
3. **Ni mandhari ya kijamii yenye changamoto halisi** – ajira, mapenzi, elimu, ukosefu wa pesa, uhalifu mdogo, na muziki wa kizazi kipya.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mandhari hubeba alama (symbolism) na maana pana zaidi ya eneo la hadithi. Katika *Shujaaz*, mandhari ya mitaa hubeba maana ya mapambano ya vijana, ubunifu wao, na matumaini ya maisha bora licha ya changamoto. Mandhari haya yanajenga "uhalisia wa kijana wa leo," tofauti na riwaya au tamthilia za awali ambazo mara nyingi zilihusisha watu wazima au jamii kwa mtazamo wa kifalsafa na kisiasa.

Hivyo basi, upekee wa *Shujaaz* kwa mujibu wa mandhari ni kwamba:

- Hutumia mitaa ya kisasa (miji na vitongoji) badala ya mazingira ya kihistoria au kifalsafa.
- Huchanganya mandhari halisi ya kimwili (geto, soko, studio) na mandhari pepe *(Facebook, WhatsApp, YouTube*).
- Huweka vijana kama sehemu kuu ya mandhari badala ya watu wazima pekee.

Kwa hivyo, kupitia ujanibishaji, *Shujaaz* hufanikisha mandhari yake kwa kuakisi mazingira ambayo vijana wa Kiswahili wa karne ya 21 huishi, kufanya kazi na kushirikiana.

### 4. Maudhui na Dhamira

Katika fasihi, maudhui ni jumla ya mawazo makuu yanayobebwa na kazi, ilhali dhamira ni mitazamo ya mwandishi kuhusu masuala hayo. Kwa mujibu wa Senkoro (1982), maudhui huchota uhalisia wa kijamii wa jamii husika na kuyapeleka kwa hadhira kwa namna ya kisanaa. Katika riwaya na tamthilia nyingi za Kiswahili za awali, maudhui makuu yalihusu mapambano ya kisiasa, mshikamano wa kijamii, dini, mapenzi ya kifalsafa, au masuala ya ukoloni na ukombozi wa mwanadamu (taz. Hussein, 1970; Shaaban Robert, 1940–60).

Hata hivyo, *Shujaaz* hujitokeza kwa upekee wake kwa sababu maudhui yake yamejanibishwa kwa mazingira na changamoto halisi za vijana wa Kiswahili wa karne ya 21. Badala ya mijadala mikubwa ya kifalsafa, *Shujaaz* hujikita katika maisha ya kila siku ya kijana wa mtaa.

**Vipengele vya Upekee katika Maudhui ya *Shujaaz***

1. **Ajira na Ujasiriamali wa Vijana**
    - Moja ya dhamira kuu ni kupambana na changamoto za ajira. Vijana huonyeshwa wakitafuta njia mbadala za kuishi – kwa mfano, kupitia biashara ndogondogo, muziki, filamu, au kilimo cha kisasa.
    - Msokile (1992) anaeleza kuwa fasihi hujanibishwa kwa kuonesha matatizo yanayoikabili jamii kwa wakati husika. *Shujaaz* hufanya hivyo kwa kuonesha changamoto za ajira kwa vijana, tofauti na riwaya za awali ambazo mara nyingi zilielekeza zaidi kwenye mapambano ya kisiasa au falsafa za kijamii.
2. **Mapenzi na Mahusiano**
    - Maudhui ya mapenzi katika *Shujaaz* yamejanibishwa kwa kuakisi changamoto za vijana wa sasa: mapenzi ya mitaani, shinikizo la rika, mahusiano kupitia mitandao ya kijamii, na hata changamoto za mimba za utotoni.
    - Hii ni tofauti na riwaya za mapenzi za Kiswahili (mf. *Utengano* na *Kusadikika*) ambazo zilikuwa na mitazamo ya kifalsafa au kidini.
3. **Teknolojia na Mitandao ya Kijamii**
    - *Shujaaz* huonesha jinsi vijana wanavyotumia simu janja, WhatsApp, YouTube, na Facebook kama sehemu ya maisha yao. Hili ni janibisho jipya kwani riwaya na tamthilia za awali hazikuweza kuhusisha ulimwengu wa kidijitali kwa namna hii.
    - Pamela Ngugi (2018) anabainisha kuwa fasihi mpya za vijana hutegemea zaidi teknolojia, jambo linaloipa nguvu ya uhalisia na ushirikishi.
4. **Elimu na Ndoto za Maisha**
    - Wengi wa wahusika hujipambanua kwa kusaka elimu, kujaribu kuboresha maisha yao, au kupambana na changamoto za kushindwa kuendelea kielimu.
    - Maudhui haya huakisi changamoto halisi za vijana barani Afrika Mashariki leo.
5. **Changamoto za Kijamii (Ulevi, Uhalifu, Mimba za Mapema, Ukosefu wa Ajira)**

- Dhamira za kijamii huibuliwa kwa namna ya waziwazi kupitia wahusika wanaoishi mitaani. Kwa mfano, kijana anaweza kushawishiwa kuingia uhalifu, lakini kupitia simulizi tunapata funzo la athari za hatua hizo.
- Hili hujanibisha uhalisia wa mitaa na changamoto zinazokumba vijana moja kwa moja.

**Tofauti na Fasihi Nyingine za Kiswahili**

- Fasihi ya jadi ya Kiswahili ilibeba maudhui ya "kizazi kizima" (mtu mzima, familia, taifa).
- *Shujaaz* hujikita kwenye maudhui ya vijana, yakiwasilishwa kupitia sauti zao wenyewe.
- Hili linaonyesha upekee wake kwani linasogeza fasihi karibu na vijana, na hivyo kuipatia nafasi katika jamii ya sasa.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), maudhui ya fasihi huwezi kuyaelewa nje ya jamii yake. Upekee wa *Shujaaz* uko katika kuonesha kwamba fasihi ya Kiswahili si lazima ibebe tu falsafa za watu wazima, bali pia ndoto, vicheko, na changamoto za vijana wa mitaa.

**5. Ujanibishaji wa Fomu na Mbinu za Multimodality**

Katika fasihi, fomu humaanisha namna kazi inavyojengwa kimtindo na kimuundo, ilhali wingi muundi (multimodality) huashiria matumizi ya njia nyingi za kuwasilisha maana – maandishi, picha, sauti, au hata video. Kwa mujibu wa Hutcheon (2002), fomu ni kiini cha mawasiliano ya kisanaa, na kila mabadiliko ya kifomu huashiria mabadiliko ya kijamii na kihistoria.

Katika riwaya na tamthilia za Kiswahili za awali, fomu ilikuwa ni maandishi pekee (prose au ushairi), iliyoambatanishwa na mtindo wa moja kwa moja wa kusimulia. Fasihi simulizi ya kale, kwa upande wake, ilitegemea sauti na tamaduni za kijamii: ngoma, nyimbo, methali na vitendawili.

*Shujaaz* hubeba upekee wake kwa kutumia fomu mchanganyiko (multimodal), na hii ndiyo sehemu muhimu ya ujanibishaji wake:

**Vipengele vya wingi mtindo-Multimodality katika *Shujaaz***

1. **Maandishi + Katuni**
    - Simulizi huwasilishwa kupitia maandiko mafupi yanayofanana na mazungumzo ya mitaani, kisha huambatanishwa na katuni zenye rangi na picha.
    - Kwa mujibu wa Arnot & Sutherland (1974), katuni kama fasihi hubeba lugha ya picha ambayo huongeza nguvu ya maandiko. Katika *Shujaaz*, picha si mapambo tu, bali ni sehemu ya simulizi – zinaeleza hisia na matendo ya wahusika.
2. **Maandishi + Teknolojia ya Kidijitali**
    - *Shujaaz* si kijitabu pekee, bali pia huendelezwa kupitia mitandao ya kijamii (Facebook, YouTube, WhatsApp). Wahusika kama DJ B huchukuliwa kana kwamba wanaishi nje ya kijitabu, wakiongea na mashabiki moja kwa moja.
    - Hii hujanibisha mawasiliano ya vijana wa sasa ambao wako zaidi kwenye mitandao.
3. **Maandishi + Muziki na Utamaduni wa Vijana**
    - Mara nyingi simulizi huambatana na mazingira ya muziki wa kizazi kipya (hip-hop, reggae, gengetone). Lugha na mtindo wake hufuata mitindo ya muziki, jambo linaloonyesha kuwa fomu yake imejengwa kwa kutegemea *intertextuality* na *intermediality*.
4. **Maandishi + Ushirikishi (participatory form)**
    - Watazamaji (wasomaji) hawabaki kuwa wapokeaji pekee. Kupitia SMS, mitandao ya kijamii na kampeni za kijamii, wao hushiriki kuunda simulizi.
    - Hii ni tofauti na riwaya za awali ambapo mwandishi ndiye aliyekuwa msemaji mkuu.

**Upekee wa muundo wa *Shujaaz***

Kwa mujibu wa Huck (1979), fasihi za vijana hujipambanua kupitia muundo wa ubunifu zinazochukua njia za mawasiliano wanazopendelea vijana. Hivyo basi, upekee wa *Shujaaz* uko katika:

- **Kuchanganya maandishi, picha na mitandao** kama sehemu ya simulizi.
- **Kubadilisha jukumu la hadhira** – wasomaji si wapokeaji pekee, bali washiriki.

- **Kujenga muundo/ umbo ya kijana kwa kijana** – sio simulizi refu za kifalsafa, bali vifungu vifupi vinavyolingana na mitindo ya kijana wa mtaa na kidijitali.

Kwa kulinganisha, riwaya za Kiswahili za awali (mf. *Utengano* wa Hussein au *Siku Njema* ya Ken Walibora) ziliandikwa kwa maandiko pekee, zikiwa na msisitizo mkubwa katika simulizi ndefu na hoja za kifalsafa. *Shujaaz* kwa upande mwingine, hujanibisha fasihi kwa kutumia muundo wa katuni, mitandao na lugha fupi – jambo linaloifanya iwe ya kipekee.

### 6. Ushirikishi wa Wasomaji na Athari za Kijamii

Moja ya upekee wa *Shujaaz* ni nafasi inayotolewa kwa ushirikishi wa wasomaji. Katika nadharia za usomaji, Iser (1978) anaeleza kuwa maandiko huwa hayakamiliki bila mchango wa msomaji – msomaji ndiye anayejaza mapengo ya simulizi na kuipa maana ya kijamii. Riwaya nyingi na tamthilia za Kiswahili huacha msomaji katika nafasi ya kupokea tu ujumbe wa mwandishi. Hata hivyo, *Shujaaz* hujanibisha dhana hii kwa namna mpya.

### Vipengele vya Ushirikishi

1. **Hadhira kama Wahusika Wenza**
    - Katika *Shujaaz*, mashabiki hupewa nafasi ya kushiriki simulizi. Kupitia nambari za simu, mitandao ya kijamii (*Facebook, WhatsApp, YouTube*), na kampeni za kijamii, vijana huchangia mawazo yao, kueleza changamoto zao, au hata kupendekeza suluhisho.
    - Wahusika kama **DJ Boyie** huwasiliana na mashabiki kana kwamba anaishi nao – akijibu maswali, akiomba maoni na kusambaza simulizi zao. Hili hujanibisha fasihi ya Kiswahili kwa kuifanya iwe fasihi ya kijamii na ya kidemokrasia.
2. **Uhamasishaji na Elimu ya Jamii**
    - *Shujaaz* si burudani pekee, bali pia chombo cha kubadilisha mienendo ya vijana. Kwa mfano, hutoa kampeni kuhusu afya ya uzazi, uwezeshaji wa kiuchumi, au kushirikiana katika miradi ya kijamii.
    - Wamitila (2002) anaeleza kuwa fasihi lazima izingatie mabadiliko ya kijamii kwa wakati wake. *Shujaaz* hufanikisha hili kwa kuwa si simulizi ya kufikirika tu, bali ni jukwaa la uhamasishaji.

3. **Kujenga Utambulisho wa Kijana**
    - Kupitia ushirikishi, vijana hujiona wamo katika hadithi – kwamba maisha yao, lugha yao na changamoto zao zimetambuliwa.
    - Kwa mujibu wa Pamela Ngugi (2018), fasihi inayowashirikisha vijana huimarisha hisia zao za thamani na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika maisha ya kijamii.

**Upekee wa Ushirikishi**

- Tofauti na riwaya za Kiswahili za kiasili, *Shujaaz* hutumia ushirikishi wa moja kwa moja kupitia mitandao ya kijamii.
- Wasomaji si wapokeaji tu, bali ni washiriki na washairi wenza wa simulizi.
- Ushirikishi huu hujanibisha fasihi kwa kuifanya iwe sehemu ya maisha ya vijana badala ya kubaki kama maandiko yaliyotengwa na maisha yao.

**Athari za Kijamii**

- Vijana hupewa nafasi ya kushiriki mijadala ya kijamii kwa lugha yao na kwa mitindo yao.
- Huchochea mshikamano wa kijamii (mfano: miradi midogo ya ujasiriamali inayohamasishwa kupitia *Shujaaz*).
- Hupunguza pengo kati ya fasihi na vijana – kwa kuwa vijana wanahisi fasihi inazungumza nao, si kuwahubiria.

Kwa maneno ya Hutcheon (2002), fasihi ni kioo cha kijamii kinachoishi tu pale kinaposhirikiana na hadhira. Hivyo basi, *Shujaaz* huonesha upekee wake kama fasihi ya Kiswahili kwa kuipa hadhira nafasi ya kushiriki moja kwa moja katika kuunda maana na katika kuleta mabadiliko ya kijamii.

Kwa mujibu wa uchambuzi huu, upekee wa *Shujaaz* kama fasihi ya Kiswahili unadhihirishwa kwa dhana ya ujanibishaji. Tofauti na kazi nyingi za kifasihi zilizotangulia, *Shujaaz* hujanibisha maisha ya vijana wa Kiswahili wa karne ya 21 kwa kuakisi lugha, wahusika, mandhari, maudhui na hata fomu ya fasihi inayokubaliana na ulimwengu wao wa kila siku

### 6.10 Hitimisho

Ni wazi kuwa kazi ya *Shujaaz* ni kazi yenye upekee wake kama kazi ya fasihi. Upekee ambao unaipa kazi hii sifa zake bainifu zinazoiweka katika hali tofauti na kazi nyingine za fasihi. Haya yanathibitishwa kwa ule uteuzi wa mtunzi kutumia ubunifu wake hasa kutokana na matumizi ya Sheng, kuchangaya kwa sanaa tofauti, kuchangaya tanzu tofauti za fasihi na kutumia mtindo huru wa uwasilishaji kazi yenyewe. Kazi yenyewe ni kielelzo cha mihimili ya nadharia ya metausasa ya upatanisho na ushirikiano wa taaluma mbali mbali. Vilevile kazi yenyewe imefaulu katika kuporomoshwa kwa masafa baina ya mtunzi wa kazi ya fasihi andishi na hadhira. Mtunzi amedhirisha kuwa katika fasihi andishi hadhira inaweza kushirikishwa. Mtunzi amedhirisha kuwa kwa kutumia teknolojia ya mitandao ya kijamii kwa kutuma ujumbe mfupi hadhira inaweza kutoa maoni na mchango wao kuhusiana na mada anayowasilisha mtunzi. Upekee wa *Shujaaz* kama fasihi ya Kiswahili unadhihirishwa kupitia dhana ya ujanibishaji.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.1 UTANGULIZI

Katika sura hii, ndiyo sehemu ya mwisho ya tasnifu inayohusu *Shujaaz* kama fasihi Sehemu ya pili ya 7.2 inatoa muhtasari wa kila sura ya tasnifu huu kwanzia sura ya kwanza hadi ile ya sita. Sehemu ya tatu ya 7.3 inahusu hitimisho na muhtasari wa matokeo kwa kurejelea maswali ya utafiti kuhusu ubainishaji wa sifa bainifu za *Shujaaz,* uhakiki wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi na utathmini wa upekee wa *Shujaaz* kama fasihi. Sehemu ya nne ya 7.4 inaweka bayana mapendekezo ya utafiti wa baadaye. Utafiti huu uliongozwa na mihimili ya nadharia ya metausasa.

## 7.2 MUHTASARI

Sura ya kwanza ya utafifi huu ilihusu usuli wa mada ya utafiti na pia malengo ya utafiti. Utafiti huu ukuwa na lengo lake kuu ambalo ni kuonyesha kuwa *Shujaaz* ni kazi ya fasihi. Malengo yake mahususi yalikuwa ni matatu. Lengo la kwanza likilenga kutambulisha na kubainisha sifa bainifu za Shujaaz kama kazi ya fasihi, lengo la pilli likiwa ni kuhakiki shujaaz kwa kutumia vigezo vya uhakiki wa fasihi ya Kiswahili na la tatu likiwa ni kubainisha na kutathmini upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi.

Sura ya pili ikihusu mapitio ya maandishi ambapo utathmini wa tafiti za wasomi mbalimbali waliyoshughulikia mambo yanayohisiana na utafiti huu umefanywa. Mapitio haya kimahususi ni maandishi yanayohusu *Shujaaz* kama toleo la kila mwezi la kampuni ya *Well Told Story* na *Shujaaz* kama kazi ya fasihi. Katika sehemu hizo mbili mapengo yaliyopo kuhusiana na utafiti huu yalionyeshwa. Mawazo ya wasomi mbalimbali ambayo yanashahibiana, yanayotofautiana na yaliyosaidia kuendeleza kazi hii kuhusu *Shujaaz* kama kazi ya fasihi. Sehemu ya pili ya sura hii ya pili ikihusu msingi wa nadharia. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ikiwa ni ile ya Metausasa.

Sura ilishughulikia maswala kuhusiana na mbinu za utafiti zilizofanikisha utafiti huu yalishughulikiwa. Katika sehemu hii, vipengele vya muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, sampuli lengwa, njia ya kukusanya data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo umejadiliwa

Sura ya nne ilichunguza *Shujaaz* ni nini, ina sifa zipi bainifu na kuzieleza. Ili kufanya hivi matoleo teuliwa ya *Shujaaz* yalisomwa. Kisha uchunguzi wa sifa za Shujaaz ukafanywa kwa

kuzingatia vigezo vya kubainisha sifa za kazi ya fasihi( fasihi kuwa ni sanaa, kazi yake ikiwa ni kusawili vipengele vya maisha mahusianona hisia za watu, hutumia ufundi wa lugha kuwasilisha ujumbe wake na huweza kutolewa maelezo ya fani na maudhui). Mifano anuai ilitolewa moja kwa moja kwenye matoleo yaliyochaguliwa kimaksudi ili kukidhi mahitaji ya dhumuni la kwanza na ufasili kutolewa.

Matokeo ya utafiti yaliweza kutambulisha na kubainisha sifa bainifu za *Shujaaz* kadhaa ambazo ni kama vile:

a) Matumizi ya lugha ya kisasa ya vijana ya Sheng. *Shujaaz* inatumia lugha ya mtaani iliyochangaya Kiswahili sanifu, Kiingereza na Sheng. Lugha hii huifanya kazi hii kuwa ya kweli, rahisi kueleweka nay a kuvutia kwa walengwa.

**b)** *Shujaaz* ina wahusika hai na halisi. Wahusika wa wakuchorwa na wa picha ni vijana wa kawaida wenye changamoto, doto na Maisha kama ya wasomaji wake. Wahusika hawa wanawakilisha tabaka mbalimbali kama wanafunzi, wanaotafuta kazi, mashujaa watambulika kwa ufanisi waokatika kazi zao na talanta zao. Wahusika katika *Shujaaz* ni sauti ya vijana na wanatafsiri matukio katika jamii kwa mtazamo wao ili kuwasiliana na jamii kwa jumla.

c) *Shujaaz* ina maudhui yenye mguso wa kijamii. Baadhi ya maudhui yanayoshughulikiwa katika *Shujaaz* yakiwa ni: Ujasirimali, afya ya uzazi/changamoto za uzazi, uongozi na nafasi ya vijana katika uongozi, usawa ya kijinsia, ushiriki wa vijana katika maendeleo ya jamii, mapambano dhidi ya dawa za kulevya na talanta na umuhimu wa kukuza talanta hizo. Maudhui haya huakisi maisha ya vijana katika jamii.

d) Ushirikishaji wa hadhira/ msomaji. Wasomaji wa *Shujaaz* hushiriki kwa kutuma ujumbe, kutoa maoni au hata kutoa hadithi zao. Wasomaji wa Shujaaz si wapokezi tu bali ni washiriki katika uwasihishaji. Shujaaz ni fasihi inayoshirikisha jamii moja kwa moja.

e) *Shujaaz* ina mbinu ya kipekee ya uwasilishaji. Mbali na kutumia maandishi, *Shujaaz* inatumia katuni/vibonzo, picha halisi za watu na pia mitando ya kijamii. Yaani ni fasihi mseto inayounganisha Sanaa mbali mbali na tanzu za fasihi simulizi na andishi huku ikishirikisha hadhira kidigitali. Sifa hii inaipatia *Shujaaz* upekee unayoifanya kufaa kizazi cha sasa.

f) *Shujaaz* ina sifa ya kudhamiria kuelimisha, kuhamasisha na kuleta mabadiliko. Hivi kwamba mbali na kuburudisha kazi hii inalenga kuinua fikra za vijana na kuwazindua ili wachukue hatua zifaazo kuboresha maisha yao na jamii kwa jumla. Kazi hii inawafundisha vijana kuhusu maisha na changamoto zake na namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

g) *Shujaaz* ina uhalisia na huwakilisha jamii ilivyo. Inawakilisha jamii kwa usahihi, ikionyesha maisha ya vijana wa kawaida (changamoto zao za maisha, mafanikio yao na matumaini yao) Shujaaz inaakisi ukweli na uhalisia wa maisha katika jamii ya kisasa.

Sura ya tano inajishughulisha na uhakiki wa *Shujaaz* kwa kutumia vigezo vya uhakiki wa kazi ya fasihi ya Kiswahili. Ilikufanikisha haya vipengele vya maudhui na fani katika *Shujaaz* vinafafanuliwa kwa mifano kutoka matoleo 13 ya *Shujaaz* yaliyoteuliwa ambayo ni: matoleo maalum- SPECIAL EDITION 01/3 na 03/03, CHAPTA 27, 33, 40, 57, 68, 78, 88, 93, 98, 102 na 109. Vigezo au vipengele vya kimaudhui vikiwa ni Kipengele hiki hujumuisha: dhamira, ujumbe/maadili, mitazamo, migogoro, msimamo na falsafa na itikadi. Huku vya fani vikiwa ni wahusika, mitindo, muundo, mandhari na matumizi ya lugha. Maelezo yaliyoandamana na mifano kkutoka katika matoleo yalitolewa.

Matokeo ya utafiti huu kuhusiana na uhakiki wa *Shujaaz* ya bainisha kuwa ni kazi inayoweza kuhakikiwa kama fasihi. Baadhi ya matokeo ya uhakiki wake ni kama vile:

a) Maudhui: Shujaaz hujikita kwenye maudhui muhimu ya kijamii, kisiasa na kichumi. Baadhi ya maudhui haya yakiwa ni uongozi wa jamii, maswala ya afya ya uzazi, maisha ya vijana na changamoto zake, ujasirimali na nafasi ya teknolojia ya kidigitali katika fasihi.

b) Dhamira: Shujaaz ina dhamiria mambo kadhaa yakiwemo:
    (i) Kuzindua na kuhamasisha vijana kuleta mabadiliko katika jamii yao
    (ii) Kuelimisha vijana kuhusu maisha
    (iii) Kuhimiza tabia njema miongoni mwa vijana
    (iv) Kuhimiza uwajibikaji na kujituma hasaa katika ujasirimali
    (v) Kujenga matumaini kwa vijana kwa njia ya burudani

c) Fani na mbinu za kisasa:

(i) Shujaaz ina muundo wa kisasa au muundo mseto kwani ni mchanganyiko wa vibonzo, picha halisi, maandishi na matumizi ya dijitali.

(ii) Shujaaz hutumia lugha ya vijana ya Sheng ambayo ni mchanganyiko wa Kiswahili sanifu, Kiingereza na Sheng

(iii) Mtindo wake usimulizi ni ule wa mbinu ya mazungumzo, masimulizi ya kwanza, mafumbo na misemo ya vijana. Matumizi ya vipera vya fasihi simulizi vya 'Mchongoano' na 'Ujinga ni' vimehusishwa kunogeza masimulizi.

(iv) Wahusika: Shujaaz ina wahusika wakuu wanne: DJ BOYIE, CHARLIE PELE, MALKIA, MARIA KIM. Hawa na kundi la wahusika wasaidizi ni wahusika wa kuchorwa vilevile kuna wahusika picha halisi za watu halisi. Wahusika wengine wamechukuliwa kutoka kwa maisha halisi ya vijana wakileta mseto wa tabia changamoto, mafanikio na matumaini ( katika sehemu za CELEB na SHUJAA WA MTAA na HUSTLE FITI). Wahusika hawa wana uhalisia unaoweza kufanya wasomaji kujitambulisha au kujifunza kutoka kwao.

(v) Mandhari katika *Shujaaz* inaendana na muktadha wa sasa wa fasihi. Kazi hii ni mfano wa fasihi ya kizazi kipya inayotumia teknolojia kufikia hadhira kubwa. Shujaaz inaakisi jamii ilivyo kama fasihi ya kijamii inayolenga kuleta mabadiliko halisi kupitia sanaa.

Sura ya sita ilijibana katika kutathmini na kufafanua upekee wa *Shujaaz* kama kazi ya kifasihi. Kila kazi ya fasihi ina upekee wake. Vigezo ambavyo vilivyofanikisha nia hii ya kutathmini sifa za kipekee katika *Shujaaz* vikiwa ni: maudhui, wahusika, ploti, mtindo, umbo, mandhari na lugha. Utafiti umedhihirisha kuwa *Shujaaz* kama kazi ya fasihi ina upekee mkubwa. Upekee wake unajitokeza ifuatavyo:

a) *Shujaaz* ni fasihi inayovuka mipaka ya kitabu cha kawaida cha fasihi na kutandaa kwenye majukwaa ya kiteknolojia ambayo vijana hutumia. Ina muundo wa kiubunifu unaotumia vibonzo na picha halisi na mitandao ya kijamii. Upekee huu huifanya kuwa fasihi hai na shirikishi.

b) *Shujaaz* ina upekee wa kuchanganya aina tofauti za fasihi na Sanaa. Ni fasihi andishi kwani ina maandishi ambayo ndani mwake mna fasihi simulizi (Mchongoano na Ujinga ni). ina mchangayiko Sanaa ya kuchora (vibonzo) na sanaa ya picha halisi. Vilevile kuna matumizi ya teknolojia inayowezesha kushirikisha hadhira katika

usimulizi wake. Upekee huu huifanya *Shujaaz* kuwa mfano wa fasihi mseto ya karne ya 21.

c) Upekee wa ushirikishwaji kwa wasomaji au hadhira ya *Shujaaz*. Tofauti na hadhira ya kazi nyingi za fasihi andishi, hadhira ya *Shujaaz* inashiriki kikamilifu kwa kutuma mawazo, maswali, maoni au hata kusimulia hadithi zao kupitia matumizi ya jumbe fupi za simu.

d) Upekee wa matumizi ya lugha ya Sheng. *Shujaaz* imeandikwa na kuwasilishwa kupitia lugha ya Sheng. Kiswahili sanifu kimechanyanywa na Kiingereza na lugha ya mtaani kuwasilisha maudhui ya *Shujaaz.* Maneno ya mitaani, mafumbo na misemo ya vijana huifanya kazi hii kuwa ya kweli, ya kuvutia nay a kueleweka kirahisi na walengwa wake.

e) Upekee wa kuchangaya burudani na elimu. *Shujaaz* inachanganya usimulizi wa hadithi unaovutia na masomo muhimu ya maisha, na kuifanya kuwa ya kuburudisha na kuelimisha.

f) Upekee wa kuwa na mada zinazoakisi maisha halisi ya jamii. Shujaaz inashughulikia masuala muhimu kama vile elimu, afya, na haki ya kijamii, kuzua mazungumzo na kuhamasisha mabadiliko chanya. Hasaa inagusa maisha ya vijana wa kawaida yaani changamoto, ndoto, mapambano na mafanikio yao

g) Kwa mujibu wa uchambuzi huu, upekee wa Shujaaz kama fasihi ya Kiswahili unadhihirishwa kwa dhana ya ujanibishaji. Tofauti na kazi nyingi za kifasihi zilizotangulia, Shujaaz hujanibisha maisha ya vijana wa Kiswahili wa karne ya 21 kwa kuakisi lugha, wahusika, mandhari, maudhui na hata fomu ya fasihi inayokubaliana na ulimwengu wao wa kila siku.

Vipengele hivi vya kipekee vinaifanya *Shujaaz* kuwa na mchango mkubwa katika fasihi ya Kiswahili na nyenzo muhimu ya kukuza mabadiliko na elimu ya kijamii.

## 7.3 HITIMISHO

Utafiti huu umebaini wazi kuwa *Shujaaz* ni kazi ya fasihi ambayo imekidhi mahitaji na sifa zote za kazi ya fasihi. Kama kazi ya fasihi, *Shujaaz* imedhihirisha sifa kadha bainifu zikiwemo; kwamba ni fasihi inayotumia lugha mseto ya Kiswahili kilichochanganywa na Kiingereza na Sheng, sifa ya wahusika wake wote wakuu kuwa vijana na wasaidizi pia, sifa ya kuchangnya Sanaa tofauti na tanzu tofauti za fasihi katika kazi moja kati ya sifa nyinginezo. Yaelekea pia

hadhira yake pia ni vijana kwa hivyo kimsingi ni haki kutoa kauli kuwa *Shujaaz* ni fasihi ya vijana. Kutokana na vigezo hivi vya sifa za fasihi ni bayana kuwa *Shujaaz* imeafiki sifa hizo na bila shaka ni kazi ya fasihi inayowakilisha sifa mpya ya fasihi kama inavyopendekezwa na nadharia iliyoongoza utafiti huu. *Shujaaz* inadhihirisha wazi sifa bainifu za fasihi ya kijamii ya kisasa, inayojenga daraja kati ya sanaa na maisha ya vijana katika jamii.

Utafiti huu vilevile umedhahirisha kuwa *Shujaaz* ni fasihi ambayo inaweza kuhakikiwa kwa kutumia vigezo vya uhakiki wa kazi ya fasihi. Hata hivyo ina mapya ambayo hayapo katika fasihi zilizopo yaani riwaya, tamthilia, hadithifupi, novela au ushairi ndani mwake muna '*michongoano'*, 'Ujinga ni?', tawasifu, masimulizi ya kinathari, foto novela na hata kamusi ya Sheng. *Shujaaz* pia huwa na matumizi ya picha halisi za watu mashuhuri, huhusisha hadhira kupitia jumbe fupi za simu. Kutokana na matumizi ya vijana kama wahusika wakuu na maudhui yanayolenga maisha ya vijana ni muhali kusema kuwa *Shujaaz* ni fasihi inayohusu vijana na inatosha kuinishwa kama fasihi ya vijana. Bila shaka baada ya uhakiki huu ni bayana kuwa *Shujaaz* ni kazi ya fasihi ya Kiswahili inayokidhi mahitaji na vigezo vyote vya uhakiki wa kazi ya fasihi. *Shujaaz* ni mfano bora wa fasihi bunifu ya kijamii inayoendana na mazingira ya sasa ya kidijitali.

Ni wazi kuwa kazi ya *Shujaaz* ni kazi yenye upekee wake kama kazi ya fasihi. Upekee ambao unaipa kazi hii sifa zake bainifu zinazoiweka katika hali tofauti na kazi nyingine za fasihi. Haya yanathibitishwa kwa ule uteuzi wa mtunzi kutumia ubunifu wake hasa kutokana na matumizi ya Sheng, kuchangaya kwa sanaa tofauti, kuchangaya tanzu tofauti za fasihi na kutumia mtindo huru wa uwasilishaji kazi yenyewe. Kazi yenyewe ni kielelezo cha upatanisho na ushirikiano wa taaluma mbali mbali. Vilevile kazi yenyewe imefaulu katika kuporomoshwa kwa masafa baina ya mtunzi wa kazi ya fasihi andishi na hadhira. Mtunzi amedhirisha kuwa katika fasihi andishi hadhira inaweza kushirikishwa. Mtunzi amedhirisha kuwa  kwa kutumia teknolojia ya mitandao ya kijamii kwa kutuma ujumbe mfupi hadhira inaweza kutoa maoni na mchango wao kuhusiana na mada anayowasilisha mtunzi. Kupitia dhana ya ujanibishaji, *Shujaaz* hubainisha upekee wake kwa kugeuza fasihi ya Kiswahili kuwa ya vijana, ya kisasa na ya kijamii zaidi. Ni fasihi

inayojibadilisha, ikikubali Sheng, mitaa, mitandao na changamoto za kijana wa sasa. Kwa kufanya hivyo, *Shujaaz* hudhihirisha kuwa fasihi ya Kiswahili si turufu ya historia pekee, bali pia chombo cha uhalisia na sauti ya vizazi vipya.

### 7.4 MAPENDEKEZO

Kutokana na matokeo ya utafiti huu yafuatayo ndiyo mapendekezo kuhusiana na *Shujaaz* kama fasihi ambayo wataalam wa fasihi wanaweza kuyazingatia.

a) Kufanya tafiti za kutathmini juu ya athari ya kazi ya *Shujaaz* kwa walengwa ili kubaini iwapo wasomaji wa *Shujaaz* wanaelewa ujumbe au la na inaathiri vipi mitazamo yao kuhusu kazi, Maisha jinsia siasa na maendeleo ya jamii.

b) Uchunguzi ufanywe kuhusiana na matumizi ya teknolojia na fasihi ya kidijitali kwa kuzingatia namna ambavyo *Shujaaz* inatumiwa mitandaoni ya kijamii, katika redio na tovuti kuwasilisha fasihi. Ni vyema pia kuchunguza umuhimu wa *Shujaaz* kama mfano wa fasihi ya kidijitali.

c) Uchunguzi ufanywe kwa nia ya kuhalalisha nafasi ya *Shujaaz* katika taaluma ya fasihi kwa nia ya kuifanya kazi ya kiada na kupata mwongozo wa kuifundishia shuleni na vyuoni.

## MAREJELEO


Anderson, J. A & Meyer, T.P (1988). *Mediated Communication: A Social interaction perspective*. Newsbury Park, CA: Sage

African Digital Art (2018) *Shujaaz*: Interview with Comic Artist Daniel Mule. file:///H:/Shujaaz Interview with Comic Artist Daniel Muli – AFRICAN DIGITAL ART.htm

Arnot, M. L., & Sutherland, Z. (1974). Children and books (3rd ed.). Glenview, IL: Scott, Foresman and Company.

Barbara M. (2011, 26 January) Shujaaz: Interview with comic artist Daniel Muli. Retrieved on April 2, 2019 from H:\Shujaaz Interview with Comic Artist Daniel Muli – AFRICAN DIGITAL ART.htm

Barthes, R. (1970). *Writing degree zero and elements of semiology* (A. Lavers & C. Smith, Trans.). Boston: Beacon.

Ciprian na wenzake (2015) *Metamodernism –A Conceptual Foundation* Cluj-Napoca, Romania Colombia University.

Collection Headquarter (2020) *Are comics considered Literature?*

https://collectorsheadquarters.com/are-comics-considered-literature/ Corcoran et al (1987) *Readers, Texts, Teachers*. Portsmouth:Co.Publisher

Dayo, O. (2014) *Shujaaz Kenyan Comic Book that is Transforming Education in Africa The New Republic.* Excerpt from The Bright Continent. Mifflin Harcourt Publishing Company

DIAL & Echo Mobile (2018) *Case study - Well Told Story*. http://www.digitalimpactalliance.org Retrieved on 22.07.2019

Dylan C. G. (2020), *"The Comic Book Conundrum: Defining Comic Books as a Literary Genre"*.

Honors Theses. 724. https://encompass.eku.edu/honors_theses/724

Eliezer F.K, Habwe J. Chimerah R., Kaoneka M. Yahaya R. Attas R. (2016) *Kamusi Elezi ya Kiswahili*. The Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

Emeka O. (2013) Shujaaz FM and Comics: New Agriculturist Profiles Radio and Comic Publishing Enterprise, Shujaaz. Retrieved on January 11, 2019 from H:\Shujaaz FM and Comics Timbuktu Chronicles.htm

Githinji, P. (2007). "Mchongoano Verbal Duels: A Risky Discourse," katika Njogu K. na G. Oluoch-Olunya (wahariri). *Cultural Production and Social Change in Kenya: Building Bridges- Art, Culture and Society. Vol 1.* Nairobi: Twaweza Communications.

Gunda (2014) *Katuni ni nini? Ufasihi wa Katuni. Mbinu za Kufundishia Kiswahili kwa Walimu na Ualimu*. Retrieved on 20.06.2019

Huck, C. S. (1979). Children's literature in the elementary school (3rd ed.). New York: Holt, Rinehart and Winston

Hutcheon, L. (2002). A poetics of postmodernism: History, theory, fiction. New York, NY: Routledge.

Hutchinson P., Mirzoyants A., Leyton A. (2018) "*Empowering youth for social change through the Shujaaz multimedia platform in Kenya*." Routledge. International Juournal of Adolescence and Youth.

Iser, W. (1978) *"The Rudiments of a Theory of Aesthetic Response", The Act of Reading: A Theory of Aesthetic Response*. Baltimore: Johns Hopkins University Press,

Jauss, H. R. (1982) *Toward an Aesthetic of Reception*. Translated by Timothy Bahti. Minneapolis: University of Minnesota Press.

Kimani, C.P. (2013). "On Mchongoano and Riddles" katika *Journal of Pan African Studies Vol. 6 No.6 Dec 2013* (on-line).

Kimani W.(2018) *The Histoty and Deveropment of Kenyan Comics.*H:\The History and Development of Kenyan Comics - AwaaZ Magazine.htm Retrieved on 12.06.19

Kombo D.K & Tromp D.L.A(2006) *Proposal and Thesis Writing. An Introduction*. Nairobi. Pauline Publication Africa.

Massamba, D.P.B. (2004). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es-Salaam

McConnell, T. (2009). *"New comic strip, Shujaaz, promises young Kenyans a fresh outlook"*. London: The Times. Retrieved 3 March 2010.

Msokile, M. (1992). Uhakiki wa fasihi. Nairobi: Heinemann Kenya.

Mugenda,O.M and Mugenda,A.G (1999) *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi Acts Press.

Mukhwana, A. (1988). Ukuzaji wa Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Kwanza (B.A.) isiyochapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mushumbwa A. R (2018) *Uhusiano wa Fasihi na Jamii waweza Kutazamwa kwa Fasuli ya Mitazamo Ifasiliyo Fasihi.* http://kiswahihili.blogspot.com/2018/03/uhusiano-wa- fasihi-na-jamii-katika.html. Retrieved on 03.03.2020

Mwazemba, J. (2006). "The Futility of Fighting *Sheng*" katika *The Daily Nation*. Uk 8.8.10-2006. New Agriculturist (2011) *Shujaaz FM* – inspiring Kenya's young entrepreneurs'

Ngugi, P.M. (2010). "*Nafasi ya Ubunifu katika Mchezo wa Watoto wa "Michongoano*," katika *Kioo cha Lugha*, Juz. 8. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Kur. 67-79.

Ngugi P. (2018) Fasihi katika Lahaja Ibukizi. *Mifano kutoka Chapisho la "Shujaaz".* Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya presented at the Afrikanistentag, 19-21 Sept 1994, Cologne

Njogu, K. na Chimerah, R . (2008) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Otuoma, D.A (2015) *Mitindo Na Maudhui Katika Uchanganuzi Wa Vibonzo Kwenye Gazeti La Tifa Leo*. Tasnifu. Nairobi. Nairobi University

Peirce, C. S (1894) *"What is a Sign?"* Peirce Edition. Project Eprint.

Robinson, A (2019) *The Nine Literary Elements You'll Find in Every Story.*

https://blog.prescholar.com/literary-elements-list-examples

Romero J. A. (2013) *"Comic Books and Graphic Novels in Their Generic Context. Towards a Definition and Classification of Narrative Iconical Texts."* Atlantis, vol. 35, no. 1, pp. 117–135. JSTOR, www.jstor.org/stable/43486043 Samantha C. (2021) *Comic Books*. Scholastic Inc.

https://www.scholastic.com/teachers/articles/teaching-content/comic-books/ Seth A. [2015] *Metamericana*. Ist Edition. Wesleyan University Press.Amazon

Senkoro, F. E. M. K. (1982). Fasihi na jamii. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Sheehan, K. K. (2018) *"Graphics Are Novel." Voices from the Middle* vol.26, no. 2, Dec. pp. 57

67.EBSCOhost.search.ebscohost.com/login.aspx?direct=true&AuthType=shib&db=eue AN=133712980&site=eds-live&scope=site

Smith, S. T. (2017) *"Comic Book Kid." The Year's Work in Nerds, Wonks, and Neocons*, edited by Jonathan P. Eburne and Benjamin Schreier, Indiana University Press, Bloomington, Indiana, pp. 249–274. JSTOR, www.jstor.org/stable/j.ctt20060h2.14.

Tabachnik, S.E. (2007) "*A Comic-Book World*." World Literature Today, vol. 81, no. 2, p.24.

EBSCOhost, search.ebscohost.com/login.aspx?direct=true&AuthType=shib&db=edsjsr AN=edsjsr.01592&site=eds-live&scope=site.

Timotheus V. na Robin A. *(2010). "Notes on metamodernism". Journal of Aesthetics & Culture.*

***2** (1): 5677. doi:10.3402/jac.v2i0.5677. ISSN 2000-4214.*

Tompkins, J. (1980). *Reader – Response Criticism*. Baltimore and London: John Hopkins

Trudier. H. L (2003) *"Genre." Eight Words for the Study of Expressive Culture*, edited by Burt

Feintuch, University of Illinois Press, Urbane; Chicago; Springfield. pp. 99 120. JSTOR, www.jstor.org/stable/10.5406/j.ctt2ttc8f.8.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* .Dar es Salaam: TUKI/UNESCO/SIDA.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

____________ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

____________(2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide ~Muwa Publishers.

____________(2010) *Kanzi ya Fasihi 1*: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi* Nairobi: Vide ~Muwa Publishers.

Well Told stories (2010-2021) *Shujaaz-* Machapisho mbalimbali. Nairobi: Twaweza, Hewlett Foundation, Bill and Melinda Gates Foundation& Eshe

Wilson world (2021) *5 Essential Qualities of Good Literature*. https://5Essential -Qualities-of -a Good-Literature-wilsonworld.html.

https://www.encyclopedia.com/social-sciences/encyclopedias-almanacs-transcripts-and-maps/fotonovelas